Ikiwa umeolewa, uko salama kupata maambukizi ya VVU. Kweli si kweli?

Ndoa si kinga dhidi ya VVU.

Katika ulimwengu wote wa nchi zinazoendelea, idadi kubwa ya wanawake wataolewa katika umri wa miaka 20 na wana maambukizi makubwa ya VVU kuliko wenzao wa rika sawa ambaa hawajolewa na wenye mwamiko wa kujamiihana. **Kauli Mbiu ya "ABC"** – acha ngono, uwe mwaminifu, tumia kondomu wakati wote - ni mhimili wa programu nydingi za kuzuia maambukizi ya VVU. Lakini kwa wanawake wengi na wasichana, ujumbe huu hauna nguvu. Pale ambapo ukatili wa kijinsia umeeneea, kuacha ngono, au kuhimiza matumizi ya kondomu si chaguo halisi. Kutokana na kutokua na uwezo wa kijamili na kuchumi,

Sehemu ya 2

wanawake wengi na wasichana wanashindwa kushauriana katika mahusiano yanayohusu kuacha kabisa ngono, uaminifu na matumizi ya kondomu.

Vijana wavulana wanafahamu kila kitu juu ya ngono. Kwelli au si kwelli?

Wavulana na vijana mara nyingi wanatarajiwa kufahamu juu ya ngono na ujinsia – lakini hawafahamu.

Matokeo haya yanawazuia wengi wao kutafuta habari kuhusu VVU na UKIMWI kwa hofu ya kuonekana wajinga. Habari na elimu inayohusu VVU na UKIMWI inaweza kuwasaidia wavulana na vijana kufanya maamuzi ya muhimu juu ya maendeleo yao ya kiafya na kuwa watu wazima wenye kuwajibika. Tafiti zinaonyesha ya kwamba wakati vijana wanapokosa elimu ya afya (ambayo inaweza kuwapatia ufahamu wa milli yao, mimba na maambukizi kwa njia ya kujamiiiana), wanakuwa na hatari kubwa ya kupata VVU.⁶

Imani za kijadi na matarajio ya aina hii pia yanaongeza hatari ya wanaume kuambukizwa VVU. Wanaume hawatatafuta huduma za kiafya zaidi ya wanawake, na hutarajiwa kujihusisha na mienendo – kama vile kunywa, kutumia madawa au kuendesha bila uangalifu – ambayo huweka afya zao hatarini.

"Wakati mwiningine tunafikiri: ama kwelli ni mashoga tu wanaowea kupata (VVU) – hii haiwezi kutokea kwangu. Na hapa nipo nikisema kuwa inaweza kutokea kwa mtu yeyote, hata kwangu Magic Johnson."

Magic Johnson, mchezaji wa Mpira wa Kikapu wa Chama cha Kitaifa cha Mpira wa Kikapu Marekani (NBA) alipokuwa akitangaza kuwa amepimwa na kupatikana ana VVU mwaka 1992.

⁶ UNAIDS, Wavulana, Vijana wa kiume za VVU/UKIMWI, Nisajili... Na wewe je? Kampeni ya UKIMWI Danisi 2001.

Sehemu ya 3

Nini kilichomo ndani?

Kitabu hiki kinatoa ushauri unaoweza kutekelezwa kwa Kamati za Olimpiki za Mataifa, vilabu nya michezo na shirkisho za michezo, mameneja, watawala, waajiriwa, makocha, na wakufunzi na wanariadha, ambao wanapaswa kushughulika na masuala mengi yaliyo magumu yanayohusu VVU na UKIMWI yanayoibuka nye na ndani ya uwanja wa michezo. Kitabu hiki kinaienga kuhusu kazua maambukizi ya VVU, na huduma na tiba kwa parmoja, k.m. kutoa habari kuhusu kuzuia maambukizi ya VVU wakati huo huo kuandaa mazingira ambayo watu wanaoishi na VVU wanaweza kutoa mchango wao wa kimaisha na pia kupata tiba inayoboresha maisha.



Sehemu ya 4 Nini unachopaswa kujua inatoa habari za msingi za VVU na UKIMWI ambazo kila mmoja anahitaji kuzifahamu, zikiwemo, fafanuzi za maneno, ukweli juu ya maambukizi, namna ya kuzuia maambukizi, kupima, huduma na tiba. Imeandikwa katika lugha rahisi, kwa kutumia maneno ya kisayansi kuelezea na kufafanua mambo yanayoweza kuamsha hisia za kitamaduni.



Sehemu ya 5 Michezo na VVU inalenga uhusiano uliopo baina ya michezo na VVU, ikizungumzia masuala kama vile athari za VVU kwa mazoezi na hali kadhalika athari za mazoezi kwa VVU; kupunguza hatari za kupata maambukizi katika uwanja wa michezo, ikiwemo hatua za kuchukua pale mtu anapojeruhiwa na kupata kidonda kinachotoa damu; wanamichezo wa kike na klume kama mifano ya kuigwa, hasa jukumu wallio nalo wanariadha wanaoishi na VVU; na makocha na wanariadha wanavyochukuliana na wanariadha wengine wanaoishi na VVU.




Sehemu ya 6 Mashirika ya Michezo yanavyohusika na VVU na UKIMWI inalenga KOT, vilabu nya michezo na shirkisho kama waajiri na majukumu wallyo nayo ya kuwalinda watumishi wao kutokana na maambukizi ya VVU na pia kutengeneza mazingira yenye msaada na yasiyo na ubaguzi. Maelekezo ya msingi juu ya kutunga sera ya UKIMWI ya mahali pa kazi yanatolewa, ikiwemo nyenzo zinazohitajika. Mfululizo wa shughuli zikiwemo matumizi ya kondomu, ushauri nasaha (wa siri) na upimaji wa hiar, unyanyapaa na ubaguzi, na kutengeneza mazingira yenye msaada, zinazotolewa kwa ajili ya kutoa mafunzo juu ya VVU na UKIMWI kwa marmeneja na waajiriwa. Hizi zinapaswa kufanyika kwa kushirikiana na **Sehemu ya 4 Nini unachopaswa kujua**, **Sehemu ya 5 Michezo na VVU** na **Kiambatanishi cha 4 Kondomu**.

Sehemu ya 3



Sehemu ya 7 Mwitikio wa makocha wa michezo, wakufunzi na wasimamizi kuhusu VVU na UKIMWI inahusu majukumu ya makocha na wakufunzi katika kuwaelimisha wanamichezo na viongozi wa michezo kuhusu VVU na UKIMWI. Idadi ya mipango ya mafunzo na rasilmali zimedhihirishwa. Wakati makocha, wakufunzi, na wasimamizi wanajihuisha juu ya wanavyoweza kuwalinda wachezaji wao, viongozi wa michezo na wale

wanaojitolea wasipate maambukizi ya VVU ni lazima pia wajilinde wenyewe kwanza wasipate maambukizi ya VVU. Zaidi, wakati wakishughulikia kuwalinda wale ambao hawajaambukizwa VVU ni lazima wazilinde haki za watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Hii ina maana ya kupambana na unyanyapaa kwa na ubaguzi juu ya watu walioambukizwa na walioathirika kwa VVU popote pale unapofanyika, hata kama ni ndani au nije ya viwanja vya michezo. Masuala haya yote yameelezwu katika sehemu hii.



Shughuli kwa ajili ya vikundi vya watu wenyewe umri tofauti (kumi hadi kumi na mbili, kumi na tatu hadi kumi na tano, na kumi na tano na zaidi) zimeandalia kutoa taarifa kwa rika husika kwa lengo la kuwasaidia vijana

- kupata habari sahihi kwa ajili yao wenye ambazo wanaweza kuzishirikisha familia zao na marafiki;
- kuongeza ujasiri katika masuala ya afya ya kujamiiiana, kuahirisha tendo la kwanza la ngono na kushauriana juu ya ngono salama;
- kujifunza juu ya matumizi ya madawa ya kulevyia na athari zake;
- kujifunza juu ya rasilmali zilizopo katika jurnua zao, k.m. watu wanaoweza kuongea nao kama wanahitaji taarifa au msaada;
- kutafiti masuala ya ubaguzi na uonevu na vile yanavyouhusiana na VVU na UKIMWI; na
- kutafiti njia ambazo zinaweza kuleta mabadiliko katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI.



(Shughuli hizi zinapaswa kufanyika kwa kushirikiana na Sehemu ya 4 Nini unachopaswa kujua, Sehemu ya 5 Michezo na VVU na Kiambatanishi cha 4 Kondomu)

Maswalli ya kawaida **Juu ya VVU na UKIMWI** kupima ufahamu wa msingi juu ya VVU na UKIMWI yanatolewa. Maswalli haya yanaweza kufanywa na kila mitu anayesoma elimu ya VVU na UKIMWI – mameneja na wasimamizi, waajiriwa, makocha

wakufunzi, na wanariadha.

Sehemu ya 3

Faharisi inakupatia taarifa sahihi na za kisayansi juu ya maneno ya kawaida yanayohusika na VVU na UKIMWI

Viambatanishi ni pamoja na:


- **Kiambatanishi cha 1:** maandishi ya Sera ya KOK juu ya VVU na UKIMWI, inayoorodhesha majukumu maalum ya KOT.
- **Kiambatanishi cha 2:** mchanganuo wa kushamiri kwa janga la UKIMWI jimbo kwa jimbo.
- **Kiambatanishi cha 3: taarifa zinazotokana na Mtandoao**, zinatoa taarifa za tovuti za mashirika ikielezea maelezo mafupi ya kile kilichomo ndani ya tovuti hizo. Tovuti zilizochaguliwa ni pamoja na zile zinazotoa habari na taarifa juu ya VVU na UKIMWI, ujinsia na masuala husika, kampeni chididi ya uryanyapaa pamoja na vifaa vya kufundishia kwa ajili ya walimu wa michezo na nyenzo zingine muhimu. Habari zinazotokana na Mtandoao ni lazima zitumike kusaidia rasilimali za ndani zilizotolewa na Mabaraza ya UKIMWI ya Taifa, KOT na vyama vingine vya michezo, mashirika ya UKIMWI pamoja na mashirika ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, mashirika ya Umoja wa Mataifa, Vyama vya Kitaifa vya Msalaba Mwekundu na Mwezi Mwekundu na Mashirika yanayotoa huduma za UKIMWI.
- **Kiambatanishi cha 4:** inazungumzia elimu ya msingi ya kisayansi juu ya kondomu, hekaya na dhana potofu zilizopo, sababu za kutumia kondomu, dondoo za kujenga kujihamini, na mazungumzo juu ya matumizi ya kondomu pia na michoro ya namna ya kutumia kondomu za kiume na za kiume.

Sehemu ya 4



Sehemu ya 4

Nini unachopaswa kujua



"VVU UKIMWI. Ni jukumu la kila mtu."

Sanath Jayasuriya, Timu ya Kriketi ya Sri Lanka,
Balozi wa Nia Njema wa UNAIDS

4.1 VVU na UKIMWI

4.1.1 VVU ni nini?

VVU inasimama kwa Virusi Vya UKIMWI. Hivi ni virusi ambavyo hatimaye husababisha UKIMWI au - Ukosefu wa Kinga Mwilini. VVU vinashambulia na kuangamiza mfumo wa kingamwili - mfumo unaopambana dhidi ya maambukizi.

4.1.2 UKIMWI ni nini?

UKIMWI – Ukosefu wa Kinga Mwilini – ni hatua ya mwisho ya maambukizi yanayosababishwa na Virusi Vya UKIMWI (VVU). Mtu anayeishi na VVU anaweza kuonekana na kujisikia mwenye afya kwa muda mrefu. Hata hivyo, VVU hudhoofisha mfumo wa mwili wa kujilinda hadi pale unaposhindwa kupambana na kuyashinda magonjwa na maambukizi kama vile kichomri, kuhara, uvimbe wa mwili, kansa mbalimbali na magonjwa mengine.

4.1.3 Je, ipo tiba ya maambukizi ya VVU?

Hapana, hakuna tiba kwa maambukizi ya VVU. Kasi ya ugonjwa inaweza kupunguzwa lakini halwezekani kuisimamisha kabisa. Mchanganyo sahihi wa dawa za kuboresha maisha na kupunguza kasi ya VVU, unaweza kupunguza uharibifu unaosababishwa na VVU katika kingamwili na kuchelewesha kufikia hatua ya UKIMWI.

4.1.4 Je, ni nani muathirika?

VVU havibagi: mtu ye yeyote anaweza kuambukizwa VVU

Kila siku watu 12,000 wanaambukizwa VVU. Nusu ya hawa ni vijana.

4.1.5 Je, unaweza kumtambua mtu anayeishi na VVU kwa kumwangalia tu?

Huwezi kutambua kama mtu fulani ana VVU au UKIMWI kwa kumwangalia tu. Mtu aliyeambukizwa VVU anaweza kuonekana mwenye afya na mwisho kujisikia vizuri lakini bado anaweza kuambukiza virusi. Kipimo cha damu ni njia pekee ambayo mtu anaweza kugundua kama amepata maambukizi ya VVU.



"Ni mchezo mgumu wakati unapokabiliwa na ugonjwa usiotibika. Hasa slo mchezo wa hak. Lakini ushindwe au ushindwa, sote tunajua mchezo unaendolea."

Gheorghe Hagi, Mcheza mpira wa miguu maarufu kuliko yeyote aliywahidi kutokea nchini Romania.

Sehemu ya 4



Ukweli kuhusu UKIMWI. Julisha wengine...



International Federation
of Red Cross and Red Crescent Societies

Sehemu ya 4

4.2 Maambukizi ya VVU

4.2.1 Je, ninaweza kupata UKIMWI kwa njia ya kugusana na mtu aliye na maambukizi ya VVU?

VVU havienezwi kwa njia ya kugusana kimwili. Hii ina maana ya kwamba ni salama kucheza na kufanya kazi pamoja, kushikana mikono, kukumbatiana au kubusiana na mtu anayeishi na VVU au mwenye UKIMWI. Unaweza kuishi katika chumba kimoja, kuvuta hewa ile ile, kutumia vyombo vile vile kwa kunywa na kulia chakula, kutumia chanzo kile kile cha maji kwa matumizi yoyote na hata kuogelea katika maji hayo hayo. VVU havienezwi angani kama ilivyo kwa vijidudu ya horna ya mafua. Mbu au wanyama hawaenezi VVU. Huwezi kupata VVU kutokana na kutemate au mate, machozi, au mkojo.

4.2.2 Je, ninapaswa kuwa na tahadhari nisiambulukizwe VVU ninapocheza michezo?

La, hakuna ushahidi uliotolewa kwamba VVU vinaweza kuenezwu wakati wa kucheza michezo. Katika tukio la kujueruhivi linaloambatana na utokwaji wa damu, tahadhari za kimataifa za kushughulika na damu zitumike.

4.2.3 VVU vinaambukizwa kwa namna gani?

Kwanza lazima VVU viwepo – maambukizi yanaweza kutokea tu kama mtu mmoja aliyeo katika mazingira hatarishi ana maambukizi ya VVU. Watu wengine wanadhania ya kwamba tabia au mazingira fulani yanaweza kusababisha maambukizi ya VVU hata kama VVU havipo. Hii si kweli.

Lazima kuwepo na virusi ya kutosha – na wingi wa VVU ndio unaoamua kama maambukizi yatafanyika. Katika damu kwa mfano idadi ya virusi VVU ni kubwa, kiasi kidogo tu cha damu kinatosha kumuambukiza mtu mwengine. Pia, wingi wa virusi hivyo katika damu au maji maji mengine unaweza kubadilika, ndani ya mtu yule yule baada ya muda kupita.


Unaweza kupata maambukizi ya VVU ikiwa utajihuisha katika matendo yatakayo ruhusu idadi ya kutosha ya virusi kupenya katika mkondo wa damu yako. **Kuna maji maji ya mwilini ya alia nne tu ya mtu aliyeambukizwa na VVU ambayo yana VVU vya kutosha kuambukiza wengine;**

- Manii
- Majimaji ya ukeni
- Damu
- Maziwa ya mama

Maji maji Yasiyoambukiza

- **Mate HAYADHANIWI** kuwa na uwezo wa kuambukiza VVU. Wakati pekee ambapo mate yanaweza kuwa hatari ni pale yatakapokuwa na damu ndani yake. Hakuna matukio ya maambukizi ya VVU kwa njia ya mate, yaliyowekwa kwenye kumbukumbu. Kuna protini katika utando telezi uliopo kwenye nyama za mdomoni kwa kiasi cha kutosha kupunguza makali ya VVU katika mate hadi viwango visivyo hatari kwa maambukizi. Protini hii imejilambata katika uso wa chembe chembe za damu na hivyo kuzua maambukizi ya VVU.
- **Mkojo na Machozi** havidhaniwi kuwa na uwezo wa kuambukiza. Japokuwa VVU vinapatikana katika mkojo na machozi, idadi yake halfiki kiwango kinachotakiwa kusababisha maambukizi.

Sehemu ya 4



Sehemu ya 4

- **Jasho, Kinyesi na Matapishi** HAVIDHANIWI kuwa na uwezo wa kuambukiza. VVU havijawahi kupatikana katika vitu hivi. Hatari moja pekee ni ikiwa damu imo ndani ya vitu hivi.

VVU lazima viingie katika mkondo wa damu – kugusana na maji maji yalio na VVU haipolekei kupata maambukizi ya VVU. Ngozi yenyne afya na iyo imara hairuhusu VVU kupereni mwilini.

Zaidi ya asilimia 70 ya maambukizi ya VVU ulimwenguni yanakadiria kusababishwa na migusano katika kujamiihana baina ya wanaume na wanawake. Asilimia 10 inaweza kutafutwa kupatikana katika maambukizi yanayotokana na kujamiihana kunakofanyika baina ya wanaume, na asilimia 5 ya maambukizi ni kutokana na kuchangia sindano, sirinji na vifaa ya kuandaa madawa ya kulevyia kunakofanywa na watu wanacijdunga madawa hayo. Wanne kati ya watano wanaojidunga sindano zenyne madawa ni wanaume.

4.2.4 Maambukizi kwa njia ya ngono

Ngono penyezi inafanyika paie uumé wa mwanaume unapoingia kwenye uke au mnikundu (wa mwanamke au mwanamume). VVU vinaweza kusambazwa kwa njia ya ngono penyezi isyo na kinga (yaani, pasipo na kinga ya kondomu). Ni vigumu kufahamu uwezekano wa kupata maambukizi kwa kuitia njia ya ngono; hata hivyo inrafahamika kwamba uwezekano wa kupata maambukizi kwa njia ya ngono ya uke ni mnikubwa. Maambukizi kuitia ngono ya mkunduni imeripotiwa kuwa mara 10 zaidi ya ngono ya ukeni. Mtu aliye na maambukizi ya magonjwa ya zinaa ambayo bado hayaatibiiwa, hasa yanayotoka majimaji au yenyne michubuko, anaweza kwa wastani wa mara 6-10 zaidi, kuambukiza au kupata maambukizi ya VVU wakati wa kufanya ngono.

Ngono ya mdomoni (kutumia mdomo kusisimua uume au uke wa mtu) inachukuliwa kuwa ni tendo la ngono lenye hatari ndogo kulingana na maambukizi ya VVU. Hatari inaweza kuongezeka iwapo kuna michubuko au vidonda ndani au kuzunguka mdomo na kama umwagaji wa manii utafanyika mdomoni.

4.2.5 Wanawake wanaofanya ngono na wanawake wenzao (WW)

Ngono baina ya mwanamke na mwanamke ina hatari kidogo ya maambukizi ya VVU. Vitendo vingine ya kujamiihana karma vile ngono ya mdomoni vina hatari kidogo ya kuenzea VVU. Hata hivyo, baadhi ya wanawake wanaofanya ngono na wanawake wenzao pia wanafanya ngono isyo salema na wanaume, na baadhi ya wanawake wanaofanya ngono na wanawake wenzao wanadunga madawa ya kulevyia na kuchangia sindano.

"Ni vema kuwa bingwa, lakini mchezo muhimu zaidi ni ule unaochezwa nje ya mistari minne. Usichezee malsha yako. Ushinde UKIMWI."

Luis Figo, Mcheza Mpira wa Miguu Mashuhuri wa Kimataifa Mreno



4.2.6 Maambukizi kwa njia ya kudunga sindano za madawa ya kulevyia

Kutumia kwa kurudia au kuchangia sindano, sirinji na vifaa ya kutengenezea madawa ya kulevyia inaonyesha njia ya ufanisi mnikubwa ya maambukizi ya VVU na maambukizi mengine karma vile hepatitisi. Hatari za maambukizi zinaweza kupunguzwa miongoni mwa watumiaji wa madawa ya kudunga kwa kutumia sindano na sirinji mpya kila mara na siyo kuchangia vifaa hivyo, kwa kufisha kwa makini sindano na sirinji zinazoweza kutumika tena kabla ya kuzitumia kwa mara nyalingine, na kutokuchangia vifaa ya kutengenezea madawa.

Sehemu ya 4



Sehemu ya 4

4.2.7 Madawa ya kuongeza nguvu mwilini

Matumizi ya madawa ya kuongeza nguvu mwilini na madawa mengine ya kuongeza ufanisi yamepigwa marufuku katika michezo kwani yanadhoofisha burdani ya msingi ya michezo na juhud zetu za pamoja za kufuatilia ubora katika michezo na utu. Pia yamepigwa marufuku ili kuwalinda wanamichezo kutokana na:

- nafasi isyo na haki inayoweza kupatikana na wanariadha wanaotumia madawa ya kuongeza ufanisi yaliyopigwa marufuku; na
- madhara mabaya yanayoweza kuleta na baadhi ya madawa haya.

Kwa nyongeza, ikiwa wanamichezo wanajidunga madawa haya ya kuongeza nguvu, au dawa nyininge zozole za kuongeza ufanisi, kwa kutumia sindano hiyo hiyo wanaweza kwa urahisi kabisa kuambukizana VVU ikiwa mmoja wao atakuwa anaishi na VVU.

4.2.8 Maambukizi kupitia Damu na vitokanavyo na Damu

Ipo hatari kubwa (zaidi ya asilimia 90) ya kupata VVU kupitia damu na vitokanavyo na damu yenyé maambukizi. Hata hivyo, utekelezaji wa viwango vya usalama vya damu vinahakikisha upatikanaji wa damu na vitokanavyo na damu iliyo salama, ya kutosha na bora kwa wagonjwa wote wanachitaji kuwekewa damu. Usalama wa damu unajumuisha uteuzi makini wa mtoaji damu pamoja na kuplima damu yote iliyotolewa ili kubaini virusi vinavyobebwa katika damu pamoja na VVU.

4.2.9 Maambukizi kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto

VVU vinaweza kuambukizwa kwa mtoto wakati wa uja uzito, wa uchungu, na kujifungua, na pia wakati wa kunyonyesha. Mama mja mzito au mwanamke anayepanga kubeba mimba anapaswa azingatia kupimwa VVU. Ikiwa atapimwa na kujikuta ameambukizwa VVU, madawa ya kuboresha maisha na kupunguza kasi ya VVU yanaweza kutolewa kusaidia kuzuia maambukizi ya VVU kwenda kwa mtoto wakati wa kujifungua.


4.2.10 Matumizi ya pombe na VVU

Katika nchi nyinyi, kwa wote wasichama kwa wawulana umri ambao walipata uzoefu wa kwanza wa kujamiliana unahusiana na umri walipata uzoefu wa kwanza wa kunywa pombe na/au vitu vingine vinavyopumbaza akili. Unywaji mwingu hufanyika kwenye mabaa, katika sherehe na katika vilabu vya starehe vya usiku kucha ambapo watu Mara nyinyi hutafuta wenza wa ngono. Utafiti unapendekeza kuwa matumizi makubwa ya pombe na madawa mengine, ikiwemo kile kinachoitwa "madawa ya sherehe", Mara nyinyi imethusishwa na ngono isyo salama (ngono penyezi bila matumizi ya kondomu) na unywaji umehusishwa na watu kuwa na wenza wa ngono zaidi ya mmoja.⁷ Kulewa mara zote hutoa nafasi ya kisingizio cha lazima kwa ajili ya mwenendo uslofaa, uslo wa kistaarabu au ulio wa hatari, kama vile kufanya ngono isiyokusudiwa au isyo salama au kuwa na matumizi ya nguvu kufanya ngono. Wana rika wanaweza kuwashinikiza wenzaao kufanya ngono isyo salama. Ubakaji au aina nyininge za ukatili wa kimpenzi unaweza kusababishwa na ulevi mkub.

Vilabu vya michezo mara nyinyi ni vituo vya starehe za jumuia zinazofuatia mechii. utolewaji wa tuzo na uchangishaji wa fedha. Pombe imepewa nafasi kubwa katika starehe zinazotolewa hapo. Kunywa katika shangwe ya ushindii au katika kujiliwaza baada ya kushindwa kunaweza kukapitiliza. Unywaji wenye kuwajibika lazima uhimizwe na uwe sehemu ya maadili ya msingi ya kilabu cha michezo. Hata hivyo si kushinda mechii kunakohesabiwa bali uwanamichezo bora.

⁷ UNAIDS, Wawilaya, Vijana na VVO/OKIMWI, Nisajili... Na wewe je? Kamposi ya UKIMWI Dar es Salaam, 2001

Sehemu ya 4



Sehemu ya 4

"VVU vinaweza kumuathiri mtu yeyote mahali popote. Kama wanariadha, tupo katika nafasi ya pekee kusalidia kupeleka ujumbe, namna ya kuweza kuepuka kuambukizwa virusi. Ingawa hakuna tiba ya UKIMWI tuisishau kuwa, VVU vinaweza kuzuili.".

Yaping Deng, China, Nyota wa Mpira wa Meza na Mshindi wa medali ya Dhahabu wa Olympiki mara nne.

4.3 Je, ni namna gani nitazuia kuambukizwa VVU

"Kutumia kondomu na kutochangia sindano ni maamuzi yenye busara yanayoweza kukusaidia kuishi maisha marefu, yenye afya njema. Kwa njia ya elimu tunaweza kujifunza zaidi juu ya kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI na kwa pamoja tunaweza kusalidia kuzuia kuenea kwa janga hili."

Dikembe Mutombo, Mchezaji wa zamani wa Vikapu na Balozi wa Vijana wa Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo (UNDP).

4.3.1 Maambukizi kwa njia ya ngono

Maambukizi ya VVU kwa njia ya ngono yanaweza kuzuiliwa kwa kuacha kufanya shughuli za ngono, ndoa ya makubaliano ya kuwa na mke mmoja, na/au kutumia kondomu. Tabia hizi zinajulikana mara kwa mara kama "ABC".

- A- kwa maana ya kuacha kabisa (au ucheleweshaji wa kuanza kufanya ngono miongoni mwa vijana).
- B -kwa maana ya kuwa mwaminifu (au punguza idadi ya wenza wa ngono)
- C- kwa maana ya kutumia kondomu siku zote na kwa usahihi (Taz. Kiambatanishi cha 4.)

Kufanya ngono na mpenzi mmoja (mwaminifu) ni salama endapo:-

- nyote wawili hamjaambukizwa (Hamna VVU);
- ikiwa ninyi nyote mnafanya ngono na mwenza mmoja; na
- hakuna kati yenu anayejiweka katika mazingira ya kupata VVU kwa njia ya madawa ya kulevyta au shughuli zingine.

Hii inachukulia ya kwamba kuna uhusiano katika watu wawili. Katika baadhi ya tamaduni, kwa mfano katika imani ya Kiislamu au katika baadhi ya nchi, mtu anaweza, kuwa na mke zaidi ya mmoja. Katika hali hii, uhusiano wa kimpenzi na wake wote ni salama ikiwa wote hawana VVU na wanabakia namna hiyo. Vinginevyo, matumizi sahihi na ya kila mara ya kondomu yafanywe na wenza wote wa ngono.

Zipo shughuli nyingine za ngono mbali ya ngono penyezi ya uke au mkundu, ambazo ni salama kama vile kubusuana, kuukanda mwili kimpenzi, kupiga punyeto na kupigishana punyeto kwa makubaliano.

4.3.2 Kudunga sindano yenye dawa za kulevyta

Njia pekee ya kuwa na uhakika ya kwamba umelindwa dhidi ya VVU ni kamwe kutohudunga sindano ya madawa ya kulevyta.

Sehemu ya 4



Sehemu ya 4

Kwa watu wanaojidunga madawa, hatua kadhaa zinaweza kuchukuliwa **kupunguza hatari ya kupata maambukizi ya VVU**:

- Tumia madawa kwa njia ya kunywa (badili kutoka kutumia madawa ya kulevyta kwa njia ya kudunga sindano kwenda matumizi yasiyo ya kudunga sindano).
- Usirudie kutumia au kuchangia kabisa sindano, sirinji, maji au vifaa vya kutayarishla madawa.
- Tumia sirinji mpya (inyopatikana kutoka chanzo kinachokubalika, k.m. mkemia au kupitia programu ya kubadilishana sindano) kutayarisha au kudunga madawa kila wakati.
- Wakati unapotayarisha madawa, tumia maji yallyofishwa au maji masafi kutoka chanzo kinachotambulika.
- Tumia alkoholi safi, sugua na safisha eneo la kudunga sindano kabla ya kudunga.

Hata kama wanamichezo kwa ujumia hawatumii madawa, ni vizuri kujifunza kuhusu matumizi ya dawa za kulevyta kwa kudunga. Wapo watumiaji kama milioni 13 wa madawa ya kulevyta ulimwenguni pote huku matumizi ya madawa kwa kujidunga yakitaarifiwa katika nchi 130 na nyingi kati ya hizi zikitoa taarifa ya kuwepo maambukizi ya VVU miiongoni mwa watumiaji wa madawa ya kulevyta.⁴ Ni tatizo la kiulimwengu.

"Kuruka juu ya kiwanja katika kilele cha ukakamavu wako ni jambo la kustaajabisha. Usidanganyike, kuwa katika ulevi wa madawa kunaweza kakupa zaidi ya hisia nzuri, inaweza kuharibu afya yako, na kukuacha ukiwa na VVU."

Sergey Bubka, Ukraine, Nyota wa Kuruka kwa Uondo na mshindi wa Medali ya Dhahabu ya Olimpiki; Mwenyezekiti wa Zamani wa Kamisheni ya Wanariadha ya KOK.

4.3.3 Je, ngono "salama" ni nini?

Hakuna tendo la kujaamiihana lilio salama kwa asilimia 100. Ngono isyo salama ni ile ambapo mwiringiliano katika tendo la kujamiihana unafanyika pasipo matumizi ya kondomu. Hali hii inamuweka kila mtu katika mazingira hatarishi ya kuambukiza au kupata maambukizi ya magojwa ya zinaa ikiwemo VVU.

Ngono salama ni kuchukua tahaadhari zinazopunguza uwezekano wa kuambukiza au kupata magonjwa ya zinaa ikiwemo VVU, wakati wa kujamiihana. Kutumia kondomu kwa usahili mara kwa mara (Tazama **Kiambatanishi cha 4**) wakati wa kujamiihana huzingatiwa ya kwamba ni ngono salama.

4.3.4 Vipi kuhusu chanjo ya VVU?


Tumaini bora zaidi la muda mrefu la kudhibiti kuenea kwa janga la UKIMWI ni kutengeneza na kugawa chanjo ya kinga ulimwenguni. Chanjo zimesaidia kuzuia kuenea kwa magonjwa hatari kama vile polio na ndui. Wapo wanasyansi na mashirika yanayofanya kazi kwa bidii ili kupata na kugawa kinga dhidi ya UKIMWI iilo salama, yenyewe uwezo na inayopatikana kwa urahisi. Hata hivyo, chanjo ya UKIMWI inaonekana kuwepo miaka mingi ijayo na haidhaniwi kuwa "risasi ya kimiujiza"

4.3.5 Je, kuna kidonge cha kutumia "asubuhi inayofuata" kinachozua maambukizi ya VVU?

Inawezekana umesikia juu ya "kidonge cha asubuhi inayofuata," kwa ajili ya VVU. Kwa kweli hii ni huduma ya kuzuia maambukizi arayopewa mtu baada ya kuwa katika mazingira hatarishi.

⁴ UNODC, Taseria ya Madawa Ulimwenguni 2004 Kitabu 1, Seks 1.3, 48. Karati Madawa juu kuzua na Huduma ya Maambukizi VVU/UKIMWI miiongoni moja Wilaya la Madawa, 2002. http://www.unodc.org/pdf/WDR_2004/Chap1_Injecting_drugs.pdf

Sehemu ya 4



Sehemu ya 4

Huduma hii si ya kidonge kimoja, na haizui VVU. Huduma hii ni tiba inayochukua majuma 4 na inatakiwa ianze ndani ya masaa 72 baada ya mtu kuwepo katika mazingira hatarishi ya kupata VVU, na hii inaweza kupunguza uwerekano wa mtu kupata VVU. Zoezi hili haliondoi hatari ya kuambuidzwa. Hadi sasa huduma hili inayojilkana kama PEP (kwa klingereza yaani Post Exposure Prophylaxis) imetumika zaidi kuwetbu wafanyakazi wanaotoba huduma za afya ambao wariekutana na mazingira hatarishi kutokana na kazi yao. Huduma hii siyo nija ya kuzuia usipate maambukizi ya VVU.

"Kutumie kondomu unapofanya ngono ni njio salama zaidi ya kujilinda wenye wawepo tunapata magonjwa ya zinaz - ikhwamo VVU. Kama utafanya hivyo- uso niwangalifu na utumie kondomu."

Matthew Pinsent, Mpiga Makasia Mwingereza, na Mshindi Mara Nne wa Medali ya Dhahabu ya Olimpiki.

4.4 Kupima VVU



"Wanamichezo nyota na maarufu pia wameambukiziwa VVU. Maambukizi ya VVU yanaweza kutokea kwa mtu yeyote, kwa hiyo jili nde weewe mwenyewe na wale unaowajali. Wote tunaweza kuchukua hatun kuzua kuenea kwa VVU na kusitisha ubaguzi kwa watu wanaoishi na VVU"

Yao Ming, Mkhezaji wa Mpira wa Kikapu wa Kichina na nyota wa NBA

4.4.1 Je, kipimo cha VVU ni nini?

Kipimo kinachoonyesha kama VVU vimo mwilini. Vipimo vya VVU vinavyotumika loka kawaida mara kwa mara vinagundua kingamwili wanaotengenezwa na mfumo wa kujikinga wa mwili kutokana na kuwepo kwa VVU, kwani hivyo ni rahisi (na gharama nafluu) kugundulika kuliko virusi vyenyewe. Kingamwili hutengenezwa na mfumo wa kujikinga mwilini unapokabiliana na maambukizi. Kwa watu wengi, inachukua muda wa miezi mitatu kwa kingamwili hawa kukua. Mara chache, inaweza kuchukua hadi miezi sita.

4.4.2 Je, nsubiri muda gani kabila ya kupima VVU baada ya kuwepo katika mazingira hatarishi ya maambukizi?

Inaperdekezwa kuwa usubiri mleali miltarbi baada ya kuwa katika mazingira hatarishi kabila ya kupimwa VVU. Ingawa kipimo cha kingamwili wa VVU ni makini sana, upo muda wa majuma matatu hadi kumi na mawili tokea tukio la kujemili ana uwezekano wa maambukizo na kutoke^a kwa kingamwili wa virusi. Hivyo, kama unaifikiri umekuwa katika hal hatarishi ya kupata maambukizo ya VVU wakati wa kujamili anahtajil kusubiri majuma kumi na mawili kabila ya kupima, na wakati^b huo aidha ujitege na ngono au daima utumie kondomu tena kwa usahihi (Tazama Kiambatanish cha 4).

Sehemu ya 4



Sehemu ya 4

4.4.3 Je, ufanya nini ikiwa una mashaka ya kwamba umekuwa katika mazingira yenye kuweza kukuambukiza VVU?

Ikiwa unadhania umeambukizwa VVU, ni lazima upate ushauri nasaha na upimwe VVU. Tahadhari lazima zichukuliwe kuzuia kusambaza VVU kwa wengine. Kwa kipindi hicho uache kujamili ana au utumie kondomu kwa usahihi. (Tazama Kiambatanishi cha 4). Kama unajidunga madawa ya kulevya, usichangie sindano.

4.4.4 Kwa nini nikafanye kipimo cha VVU?

Kufahamu hali yako ya VVU kuna faida kubwa mbili. Kwanza, ikiwa unayo maambukizi ya VVU, unaweza kuchukua hatua zinazostahili kama vile kula vizuri, kupumzika vyta kutumia dawa sahihi za kupunguza kasi ya VVU, kama zipo, hivyo kurefusha maisha yako kwa miaka mingi. Pili, ikiwa unajua umeambukizwa, unaweza kuchukua hatua za muhimu kuzuia maambukizi ya VVU kwa wengine.

"Kuna kuishi kwilingi tukiwa na tiba sahihi."

Greg Louganis, Marekanu, Mtu mwenzaji kuishi na VVU, Mpiga Mbizi na Bingwa wa Medali za Olimpiki mara tano akiwaasa wasikilizaji wake wakapime VVU.

4.4.5 Ni wapi nitakapoweza kupata vipimo cha VVU?

Kuna mahali pengi unakoweza kupima VVU: katika ofisi ya daktari binafsi, idara ya afya iliyopo sehemu husika, hospitali, kliniki za afya ya uzazi, na maeneo maalumu kwa ajili ya kupima VVU. Kila wakati jaribu kutafuta huduma ya kupima inayotoa ushauri nasaha juu ya VVU na UKIMWI.

4.4.6 Je, majibu ya vipimo vyangu ni ya siri?

Watu wote wanaopimwa VVU lazima watoe ridhaa yao kabla ya kufanya hivyo. Majibu ya vipimo lazima yahifadhiwe kwa siri.

4.4.7 Ni fanya nini ikiwa nina VVU?

Tunashukuru, kwa kuwepo tiba mpya, watu wengi wenye VVU wanaishi maisha marefu na yenye afya njema. Ni muhimu sana kuhakikisha ya kwamba unaye daktari anayejua namna ya kutibu VVU. Mtaalamu wa huduma za afya au mtoto ushauri nasaha aliyehitimu wanaweza kutoa huduma za ushauri nasaha na kukusaidia kumpata daktari anayefaa. Uwasiliane na kikundi cha kusaidiana cha watu wanaoishi na VVU na UKIMWI katika eneo lako.

Kwa nyongeza unaweza kufanya haya yafuatayo kubaki na afya njema:

- fuata maelekezo ya daktari wako. Hudhuria kwa daktari kama ilivyopangwa. Ikiwa unakubaliana na ushauri wa daktari wako na kukubali kutumia dawa, basi, zitumie dawa kama daktari wako alivyoagiza;
- kama una maambukizi nenda ukatibiwe;
- pata chanjo ya kuzuia maambukizi kama vile nimonia na mafua (baada ya ushauri wa daktari);
- ikiwa unavuta sigara au unatumia dawa ambazo hazikutolewa na daktari wako, acha au punguza matumizi hayo;
- kula milio ulio kamili kwa utaratibu unaofaa;
- punguza matumizi ya pombe/vileo na kunywa kwa wingi vinywaji visivyo na kafeini;
- fanya mazoezi kila mara ili kuwa na nguvu na afya imara;

Sehemu ya 4

- pata usingizi na mapumziko ya kutosha; na
- punguza msongo.

"Uwe na VVU au la? Hailalishi. Sote tunawenza kujiunga na mapambano dhidi ya VVU."

Kipchoge Keino, Kenya, Mkimbiaji Mbio Fupi za Kati, Mshindi Mara Mbili wa Medali ya Olimpiki ya Dhahabu.

4.5 Huduma na Tiba

4.5.1 Je, ni huduma na tiba zipi zinazopatikana?

Tiba na huduma hujumulsha mambo mengi tofauti, yakiwemo ushauri nasaha na upimaji wa hiar, msaada katika kuzuia kuendelea kwa maambukizi ya VVU, ushauri nasaha wa kufuatilia, ushauri juu ya chakula na lishe, tiba kwa magonjwa ya zinaa, kuzuia na kutibu maambukizi ya magonjwa nyemelezi (OI) na utoaji wa dawa za kuboresha maisha na kupungaza kasi ya VVU (ARV).

4.5.2 Je, dawa za kuboresha maisha na kupunguza kasi ya VVU (ARV) ni zipi?

Dawa za kuboresha maisha (ARV) zinatumika kutibu maambukizi ya VVU. Dawa hizi zinafanya kazi dhidi ya maambukizi ya VVU kwa kupunguza kasi ya kuzallana kwa VVU mwilini lakini haziponyeshi.

4.5.3 Je, huduma ya aina gani inapatikana pale dawa za kuboresha maisha na kupunguza kasi ya VVU (ARV) zinapokosekana?

Aina nyingine za huduma zinaweza kusaidia kuboresha hali bora ya maisha pale dawa za kuboresha maisha na kupungusa kasi ya VVU hazipatikaniki. Hizi ni pamoja na lishe bora na usingizi wa kutosha, mazoezi, ushauri nasaha, kuzuia na kutibu magonjwa nyemelezi, na kwa ujumla kuishi katika afya bora.

4.5.4 Je, nini kuhusu lishe bora?

Lishe bora ni muhimu kwa kila mmoja. Kuwa na utayari na kucheza michezo ina maana ya kwamba unahitaji chakula cha ziada. Ulaji mzuri ni muhimu sana kwa watu wanaoishi na VVU au UKIMWI, ambao wanahitaji:

- Mafuta ya kuongeza nguvu kwa asilimia 10-15 zaidi ya mtu mzima asiye na VVU;
- Vyakula vyenye Protini kwa asilimia 50-100 zaidi kuliko yule asiye na VVU; na
- Vitaminii A, B6, B12, C, chuma, saliniamu na zinki ili kuparibania na maambukizi.

Kimsingi, lishe inapaswa iangaliwe kama tiba-mwenza yenyewe umuhimu mkubwa inayoweza kukamilisha usimamizi wa kitiba wa VVU. Kula vizuri kunaweza kusaidia:

- kuzuia au kuchelewesha kupotea kwa misuli au "kukonda";
- kuimarisha mfumo wa kujikinga mwilini;
- kupunguza kutokea na ukali wa magonjwa nyemelezi;
- kupunguza dalili za VVU na UKIMWI.

"Furahia maisha. Ishi. Kwa wale wenye VVU, toka nje mkasimulie maisha yenu na watu wengine na muwafanye wajisikie vizuri. Jitahidi kushikilia hilo mionganoni mwa wazazi, au ndugu wa kiume au ndugu

Sehemu ya 4

wa kike. Watu wanaweka msongo mwingi sana juu yao wenyewe kwa kuficha mambo yao wenyewe. Unabeba mzigo mzito sana unapozua mambo ndani yako.

Magic Johnson, Marekani, Mcheza Mpira wa Vikapu wa NBA, 1996 baada ya kurejea kucheza Mpira wa Vikapu wa Kulipwa baada ya tiba ya dawa za kuboresha maisha, na kupungusa kasi ya VVU.

Ikiwa wewe unaishi na VVU, ni muhimu sana kuepuka kupoteza uzito pasipo kkusudia, ambao unaweza kuzidi kudhoofisha uwezo wa mfumo wa kingamwili kupambana na maambukizi. Kula chakula cha kutosha – na vile viliyo sahihi – kulinda uzito wako wa kawaida na kuuweka mwili wako katika hali ya nguvu inaweza kuleta mabadiliko halisi katika kutunza afya yako. Kwa ujumla, watu wanaoishi na VVU wanapaswa kujaribu kula lishe yenye protini asilimia 30, mafuta asilimia 30 na wanga asilimia 40. Pia wanapaswa kula milio 3-5 ya mboga mboga kila siku na matunda mara 2-4 kila siku. Wapunguze kuvuta sigara, pombe na vinywaji vyenye kafeini, matumizi ya sukari na msongo.

4.5.5 Je, nitawezaje kuihudumia jumuia yangu?


Unyanyapaa na ubaguzi unaozunguka VVU na UKIMWI unaweza kuleta uharibifu mwingi kama ugonjwa wenyewe. Kwa kuwa UKIMWI unaweza kuua watu walio na maambukizi ya VVU, watu wengi wanawaogopa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Ukipanya, mliko, hekaya ambazo kawaida zinazunguka VVU na UKIMWI kwa sababu unahusika na tabia binafsi za kujamiihana au shughuli zisizo halali kama matumizi ya madawa. Katika jamii nyingi, UKIMWI unaonekana kama jambo la aibu na watu wanaoishi na VVU na UKIMWI wanaleta aibu kwa familia au jumuia zao.

UKIMWI pia umeathiri watu wanaonekana kuwa wa tofauti katika jamii zetu, wale walio wachache, kama vile wanaume wanaofanya ngono na wanaume, wanaofanya biashara ya ngono, wanaojidunga madawa ya kilevya pamoja na watu wa rangi na tamaduni nyingine mibali na za kwetu. Watu wengi hawaridhiki na hali ya kutofautiana, hivyo huogopa.

Ni muhimu kukumbuka ya kwamba: VVU havibagui, lakinini watu wanabagua. Mtu ye yeyote anaweza kuambukizwa VVU na VVU havienezwi kwa kugusana kimwili.



Sehemu ya 5



Sehemu ya 5

Michezo na VVU

5.1 Athari za VVU kwa mazoezi na zile za mazoezi kwa VVU

5.1.1. Athari za mazoezi kwa VVU

Kwa ujumla inakubalika kwamba kushiriki katika michezo kuna faida kubwa sana kwa watu wanaoishi na VVU. Mazoezi ya kiasi yanaimarisha mfumo wa kingamaradhi, yanauvezesha mwili kupambana vyema na VVU na yanaweza kuchelewesha kufikia hatua ya UKIMWI. Ukitzingatia ya kwamba asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU hawajui ya kwamba warneambukizwa, kuinua kucheza michezo na kuwezesha mazoezi kufanyika katika jamii itapandisha kingamaradhi ya watu wengi wasiojua ya kwamba wanaoishi na VVU.



Mazoezi ni sehemu ya mpango wa michezo mzima wenye lengo la kumwezesha mtu anayeishi na VVU kuishi muda mrefu. Mazoezi ya mara kwa mara si tu yana manufaa kwa mishipa ya moyo ya watu wanaoishi na VVU. Vipimo vya kisaikolojia vinaonyesha ya kwamba shughuli za michezo zinapunguza kukata tamaa, kuchoka, msongo na hasira, badala yake michezo inaongeza ushupavu na kwa uhakika inaboresha hali ya maisha ya wanaoishi na VVU. Mazoezi yanalenga afya zaidi na si ugonjwa.

Michezo pia inatoa nafasi ya **kujumuisha na kusaldia kijamii**, arbakao ni muhimu sana kwa watu wanaoishi na VVU. Zaidi, michezo inatoa kielelezo kwa jumuia na wananchi wanaoishi na VVU wasioshiriki kuwa kuishi na VVU si mwisho wa dunia.


Michezo pia inatoa nafasi arbakao maadili ya muhimu kama vile **kujitolea** yanaweza kukuzwa na kuendelezwa. Wanaojitolea katika michezo wanawakilisha nguvu ya pamoja kutokana na muda binafsi wanaoutoa na manufaa yanayopatikana. Hawa wanaojitolea wanaonyesha kujitoa kwa dhati, nia ya kutoa mchango unaomletea faida mwenyewe kujitolea, michezo kwa jumla na jumuia husika. Hili ndio thamani ya kuwa mtu anayejitlea.

Haijalishi ikiwa wewe una VVU au huna, sote tunaweza, kucheza michezo pamoja bila shinikizo la kushinda. Mchezo unapaswa kuwa mzuri kwa ajili ya afya ya akili na mwili, kukufanya ujisikie vizuri na kukupatia ujasiri.

"Walisema kucheza mpira wa kikapu kutaniua. La, si kucheza mpira wa kikapu kilichokuwa kinaniua ."

Magic Johnson, Marekani, Mchezaji wa Chama cha Mpira wa Kikapu cha Marekani (NBA) na Mshindi wa Medali ya Dhahabu ya Olimpiki baada ya kurudi kucheza wa Kikapu 1996.

Sehemu ya 5



Sehemu ya 5

5.1.2 Athari za VVU kwa mazoezi

Hivyo wewe unaishi na VVU; migeuzo ya mwili inaweza kuwa na maana tofauti na kile kinachoendelea, kwa mfano wachezaji wa timu shindani au ufahamu wa mwili. Kutoptaka na maambukizi ya VVU, mambo yenye utata kuhusu mwili yanaweza kuibuka. Dalili, hata mabadiliko kidogo, ambayo wale wanaoitwa "wenye afya" wasingeyatazama, yanaweza kuleta usumbufu. Swali, "**Nini ninachowea au ninachotaka kutegemea au kudai kutoka katika mwili wangu?**" linailizwa kwa sababu mpya kadhaa. Uchovu wa kawaida unaotokea wakati kwa wakati unaweza kuangaliwa katika njia tofauti.

Kwa watu wanaoishi na VVU kutumia dawa za kuboresha maisha na kupunguza kasi ya VVU kunaleda changamoto mpya: kuyazoea mazingira mapya yenye mashaka yanayotokana na dawa hizi na madhara yake mengine. Madhara yanaweza kuwa ya faida, kwa kufanya shughuli za mikono. Imani juu ya mwili wako inaweza kuimashwa kuititia michezo, tatio linaweza kuwa kupungua kwa misuli, mabadiliko katika hazina ya mafuta mwilini, kupanda kwa viwango vya kolesteroli, mabadiliko ya umetabolii au osteoporosi. Michezo ni mizuri kwako na ni jambo la kufaa!

Maswalli kadhaa kwa ajili yako:

- Je, UNAFIKIRI unaweza nini?
- Je, kuna fananaje kucheza katika kundi? Je, hii inapunguza hisia zako za upweke?
- Je, unajisikia vyema ndani mwako baada ya kucheza michezo?

"Katika muda huu, nimajitayarisha vema. Ninajua miruko yangu, na ninajua kuwa uchovu unaotokana na upungufu wa damu unachusiana na VVU hautapunguza kasi yangu."

Rudy Gallindo, Marekani, Bingwa wa kuteleza katika Barafu anayeishi na VVU.

5.1.2.1 Je, ni nini ikiwa sina dalili zinazohusiana na VVU?

Manufaa makubwa ya kimwili yanaweza kupatikana kutoptaka na michezo inayojenga na kuupa sura mwili wako, kwa mfano kukuza misuli kuititia mazoezi ya mara kwa mara katika programu za kinyanya vitu vyeme uzito wa kadiri, na kuimashwa ustahimilivu kuititia michezo kama vile kuendesha balskeli, kutembea, kukimbia polepole, kuogelea na mazoezi mepesi ya viungo.

Michezo ya kujiharni na kupambana kama vile masumbwi, Tae Kwon Do inaweza ikasababisha hatari kidogo ya maambukizi kwa wengine kutoptaka na kumwaga damu na inaweza isitoe falda zilizoordheshwa hapo juu.

5.1.2.2 Je, ni nini ikiwa nina dalili zinazohusiana na VVU?

Hakuna sababu ya kutoptaka kucheza michezo uliouchagua ili mradi hausababishi uchovu unaozidi. Wewe ni mwarmuzi bora wa kiasi unachowea kufanya ukizingatia kwamba juhudi zinazozidi nguvu za kawaida zinaweza kuweka mfumo wako wa kingamwili katika msongo zaidi. Kumbuka, michezo, kama vile kuendesha balskeli, kuogelea, na mazoezi mepesi ya viungo inaleta manufaa yanayohitajika. Kazi za kutumia nguvu kidogo pia zinafaa.

Michezo inayokutanisha viungo vya mwili vya juu au vya chini kama vile mpira wa miguu wa aina mbalimbali na ule wa kikapu, michezo ya aina zote ya kupambana na kujilinda inaweza kusababisha hatari ndogo ya maambukizi ya VVU kwa wengine na inaweza kuongeza hatari ya kuumizwa.

Sehemu ya 5

Ikiwa una dalili za nyurolojia, kama vile kupoteza fahamu, shida kwenye ubongo au mtukutiko wa maungo. michezo kama vile kupiga mbizi, kuruka kwa miavuli, na mbio za magari inaweza kudhochea dalili na hivyo inaweza kuwa hatari sana.

5.1.2.3 Je, ikuu michezo ambayo ina madhara kwa watu wanaoishi na VVU?

Mbali na ile iliyotajwa awali, mazoezi yenye kuhitaji nguvu zaidi ya kawaida inaweza kinga yako ya mwili katika msongo na inaweza kukudhuru. Mchezo wowote unaoweza kusababisha damu kutapanyika una uwezekano mdogo wa kuleta maambukizi yanayoambatana na damu kama vile VVU na hepatitis.

5.1.2.4 Je, ninapaswa kutangaza hali yangu ya kuwa na VVU kwa mtu yeyote anayehusika na michezo wangu?

Hautakiwi kutoa maelezo juu ya hali yako ya VVU, hata hivyo, katika mazingira ambayo mafunzo chini ya uongozi yanahitajika na nguvu inaweza kuwa kubwa kupita kiasi, inaweza kuwa kwa faida yako kumfahamisha mkufunzi au kocha. **Mtu ambaye unamueleza ni lazima aitunze habari hii kwa siri.** Hakuna uhalali wa kitabibu au kifaya ya jamii wa kuwapima au kuwachunguza wanamichezo VVU.

5.1.2.5 Nitawezaje kupunguza uwezekano wa kuambukizwa VVU?

Ikiwa una mchubuko katika ngozi, maambukizo au kidonda, ni bora kutafuta ushauri wa kitabibu. Subiri hadi kitakapopona kabla ya kucheza tena. Ikiwa umepata kidonda kinachotoka damu ukiwa michezoni, ni lazima uondoke uwanjani na kikatibiwe mara moja. Kifunike kidonda kwa kitambaa kisichopitisha maji. Tena ruhusu kidonda kipone kabisa kabla hujaanza kucheza.

5.2 Kupunguza uwezekano wa maambukizi ya VVU katika uwanja wa michezo

Hatari ya kupata maambukizi ya VVU katika mazingira ya michezo ni ndogo, na wanariadha wengi wanaoishi na VVU wamepata maambukizi hayo rje ya viwanja vya michezo. Hii ina maana ya kwamba watu wanaoshiriki katika michezo wanakibiliwa na changamoto za aina ile ile katika suala la maambukizi ya VVU. Hata hivyo, ni lazima tuhakikishe ya kwamba **tahadhari dhidi ya magonjwa yanayoambukizwa na damu** zinachukuliwa ili kupunguza hata uwezekano mdogo wa maambukizi ya VVU katika michezo.

Katika nchi nyingi ipo sera rasmi ya kutokutamka **hadharani hali ya VVU ya mtu**. Washiriki wa michezo hawatakiwi kwa namna yeyote kutoa taarifa ya hali zao za VVU, ingawa wanashauriwa sana wajlepushe na michezo kama vile mieleka na masumbwi. Matokeo ya sera hii ya kutokutoa taarifa ya hali ya VVU kwa mtu ni kuwa kilia majeruhi katika kiwanja cha michezo anachukuliwa kana kwamba ana VVU hivyo tahadhari za kimataifa za damu zinatumika.

Kuna mambo mengi yanayoweza kufanyika katika uwanja wa michezo, hasa pale panapotokea mgusano wa moja kwa moja au pale damu inapotegezemewa kumtoka mtu, ili kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU na maambukizi mengine yanayoambatana na damu wakati mtu anaposhiriki michezo. Kwa mfano:

- Maambukizi ya VVU yanawenza kurahisishwa wakati vifaa vya kujilinda vya kimechezo visipotumika, ikiwemo vya kulinda kinywa, kulinda ugoko, mabega, viatu

Sehemu ya 5

vinavyotakiwa, na kofia imara. Kuva vifaa hivi vya kimichezo kunapaswa kuhimizwa na makocha wasimamizi na maafisa wakati wa mashindano;

- Wale walio na majukumu ya kushughulika na majeraha yanayotokea katika uwanja wa michezo inapaswa wazingatia kupewa kinga dhidi ya hepatitis B;
- Ni muhimu ya kwamba yeyote anayeyashughulikia majeraha atumie tahadhari za kiulimwengu za matumizi ya damu; na
- Maeneo yote yaliyochanganyikana na damu au majimaji mengine ya mwilini yanapaswa yasafishwe kwa kutumia kemikali ya sodium hypochlorite.

Zifuatazo ni kanuni zilizopendekeswa na Baraza la Taifa la UKIMWI la Australia (ANCA) na Shirkisho la Tiba ya Michezo la Australia (ASMF) kusaidia kupunguza zaidi uwerekano mdogo wa kupata maambukizi wakati wa kushiriki michezo ambayo inahusu mili kugusana moja kwa moja au pale uvujaji wa damu unapotegejewa kutokea.


- Ikiwa mchezaji ana mchubuko katika ngozi yake, ni lazima taarifa itolewe kwa afisa anayehusika na utaratibu wa kiafya ufanyike;
- ikiwa mchubuko utajitokeza ni lazima usafishwe mara moja kwa dawa maalum na kufunikwa vizuri kwa usalama; na
- ikiwa kidonda kinachotoa damu kitatokea, ushiriki wa mhusika usimamishwe hadi kutokea kwa damu kutapozuiwa na kidonda kimesafishwa kwa maji mengi na kama ni kichafu kimesafishwa kwa sabuni na kisha kufunikwa kwa kitambaa kisichopitisha maji.

Kisanduku cha 5: Ni nini cha kufanya kuniapotokoa kuvuja kwa damu.

Taratibu zifuatazo si ngumu na si za gharama na ni vema kukubaliwa na wanariadha wote, makocha, wekufunzi, na maafisa we huduma ya kwanza. Li watu weweze kujifunza taratibu hizi, zibandikwe katika vyumba vya kubadili mavazi na karibu na sanduku la huduma ya kwanza.

- Watu wanaotaoa huduma ya kwanza wakati kuna uvujaji wa damu inapaswa wavae glavu za kinga;
- Ngozi imepenywa – safisha eneo vizuri kwa sabuni na maji, au sabuni yenyе kemikali maalum inayofaa. Tauo chafu kamwe lisitumike tena;
- Nguo zina madoa ya damu – inapaswa zibadilishwe na zingine sali zitumike mara tu baada ya kidonda kutiwa. Zishikwe kwa glavu za mpira na zichovye katika kemikali ya kuua viini vya maradhi kabla ya kuoshwa katika mashine ya kufulia nguo ya nyumbani katika mzunguko wa maji ya moto;
- Damu imedondoka katika ngozi ya mtu – bila kuzingatia kama ipo michubuko au mifasuko safisha kwa makini ukitumia maji na sabuni. Tauo chafu kamwe lisitumike tena;
- Macho yaliyodondokewa na damu – macho yakiwa yamefunguliwa wazi, safisha eneo husika ukitumia maji au maji yaliyochanganyiwa na chumvi;
- Damu kuingia mdomoni – temu damu hiyo kisha usukutue mdommo kwa maji mara nyingi;
- Kuna kujali kwa ziada juu ya maambukizi – ushauri wa kitibabu unapaswa kutafutwa kutokea kwa daktari katika hospitali inayotea mafunzo au kliniki yenyе usoefu wa kitaalamu juu ya maambukizi ya VVU.

Sehemu ya 5



Sehemu ya 5

"Nilikuwa ninamtazama Brian Wright, anayelishi na VVU, mikoregrafia wa kuteleza kimaumbo naye alikuwa ni mtu mwenye tabia ya aina yake, aliyenifanya nicheke, aliyeenwa hai kabisa akifanya kile alichopenda kufanya. Sikuweza kujizua bali kufikiri ya kwamba hamasa yake ilikuwa safi kabisa. Alikuwa akifanya kile alichotoka kukifanya, kwa sababu zote njema. Nilanza kufikiri kuwa inabidi watu kujifunza kutoka kwanke, kutokana na jinsi alivyoishii maisha yake."

Michelle Kwan, Bingwa wa dunia mara tano wa mchezo wa kuteleza katika barafu, aliyekuwa mtu wa mwisho kufundishwa na Brian Wright kablia hajafariki dunia kwa sababu zinazazohusishwa na UKIMWI, 1993.

5.3 Wanamichezo wa Kike na wa Kiume kama Mfano wa Kuigwa

Wanamichezo, na haswa wanariadha waliofanikiwa ni mfano mzuri wa kuigwa. Hakuna mtu armbaye anataka kuona kwamba kila tendo (au kila jibu la tendo) linapewa hukumu. Lakini japoikuwa kukataa kwa baadhi ya wanamichezo, wao Ni mfano wa kuigwa. Watu wanaowazunguka huwaangalia na kuwahukumu kwa lolote wanadolitenda. Wenzao, wakufunzi, na umma kwa ujumla wote wanaangalia jinsi gani mwanariadha aliyefanikwa anavyotenda na kukabili hali yoyote. Wana mfano hawa wa kuigwa wanachokifanya, wanachokisema na jinsi wanavyoweza kukabili, mrimbo yanayojitokeza inatosha kusema moja kwa moja kwa vijana kwa njia ambayo njia chache tu zingine za kleimu zinaweza. Wana mfano hawa wa kuigwa wanaweza kuwa kielelezo kwa vijana jinsi ambayo wanaweza kugundua na kutambua vipawa vyao vya kipekee na hivyo kuwatia moyo kufanya vizuri zaidi. Katika kukabiliana na UKIMWI, sauti ya wanariadha ni njia nyingine ya kufikisha ujumbe wa kuzua maambukizi na kutoe huduma.

Moja ya mkanganyiko wa unyanyapaa unaohusika na VVU na UKIMWI ni kwamba utapunguzwa tu kama kuenye kwa UKIMWI kutapewa sura ya kibinadamu badala ya kuonekana kwamba ni tatizo la kimatibabu. Moja ya mbinu zilizofaulu katika kuondosha unyanyapaa katika VVU na UKIMWI ni pale mtu mmoja anaposema, "Mimi ninaishi na Virusi vya UKIMWI". **Kuwashirikisha wanamichezo wa kiume na wa kike wanaoishi na VVU** imejithibitisha kuwa na manufaa makubwa sana katika kufanya VVU kuwa vya kawaida na pia kuwa mfano bora kwa wanamichezo, wote vijana na wazee.

Wanariadha wanaoishi au wasioishi na VVU wanaoshiriki katika shughuli za kuelimisha juu ya VVU wanatumikia jumuuia zao na hivyo kutoa mfano mzuri ulio hai wa roho ya kujitolea kwa kuruhusu majina yao yatumike katika juhudzi za kuukabili UKIMWI. Ikiwa tunautazama ulimwengu wa michezo, kuna nguvu kazi kubwa ambayo hajatumika, ya watu wanaoweza kujitolea kutoka michezo mbalimbali.

"Ninapenda kutoleza kwenye barafu. Nisingeweza kukaa nyumbani bila kufanya lolote. Kuwa pale nje kuanifanya nijisilidhe vizuri sana."

Rudy Galindo, Bingwa wa Kuteleza kwenye barafu anayelishi na VVU, Marekani.

Idadi ya mabingwa wa michezo wanaoishi na VVU wamejitoa hadharani kufanya kazi ya kuelimisha juu ya VVU na kukabili unyanyapaa unaohusika na VVU na UKIMWI, hawa ni pamoja na:

- Arthur Ashe, Bingwa wa Tenisi, Marekani.
- Greg Louganis, Bingwa wa Medall ya Olimpiki Kuruka majini Mara 5, Marekani.

Sehemu ya 5

- Magic Johnson, Mchezaji wa Mpira wa Kikapu Chama cha Mpira wa Kikapu Marekani, Mshindiwa Olimpiki wa Medali ya Dhahabu, Marekani.
- Rob McCall, Mshindi wa Medali ya Shaba Kucheza Dansi katika barafu kwa watu wawili, Canada.
- Roy Simmons, Mchezaji wa zamani wa New York Giants, Ligi ya Taifa ya Mpira wa Miguu, Marekani.
- Rudy Galindo, Bingwa wa Mchezo wa Kuteleza kwenye barafu, Marekani.
- Tommy Morrison, Bingwa wa Ngumi Uzito wa Juu, Marekani.

"Tingazo la Magic Johnson linaonyesha kuwa UKIMWI haukuwa ugonjwa wa mtu mweupe tu, wala ugonjwa wa mashoga tu. Na hilo ni la msingi sana. Yeye amekuwa mfano mashuhuri wa kuigwa, kama mwanzadamu, Mmarekani mwenye asili ya Afrika, mtu anayeishi na VVU."

Phill Wilson, mwasisi wa Taasisi ya ya Mafunzo ya Sera ya UKIMWI ya Wamarekani wenyewe asili ya Kiafrika, na Chuo cha mafunzo, Los Angeles, Marekani.

Wanamichezo wengine wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa elimu juu ya VVU na kuendeleza ujumbe kuhusu unyanyapaa wa UKIMWI na kuzuia maambukizi, wakiwemo:

- Britta Heidemann, Ujerumani, Mshindi wa Medali ya Shaba - Upanga.
- Cathy Freeman, Australia, Mshindi wa Medali ya Dhahabu, Mbio na michezo ya Uwanjani.
- Dikembe Mutombo, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Mchezaji mpira wa Kikapu na Balozi wa Vijana wa UNDP.
- Timu ya Mbio za Kupokezana Vijiti 4x400m Ujerumani: Jana Neubert, Anke Feller, Claudia Marx na Claudia Hoffmann, Mchezo ya Olimpiki Athens.
- Gheorghe Hagi, Mcheza mpira wa miguu maarufu wa Romania.
- Frank Fredericks, Namibia, Mshindi wa Medali ya Fedha mara nne, Mbio na michezo ya Uwanjani.
- Luis Figo, Mcheza mpira wa miguu maarufu wa Ureno.
- Matthew Pinsent, Uingereza, Mpiga Makasia Mshindi wa Medali ya Dhahabu mara nne.
- Nico Motchebon na Heike Henkel, Ujerumani, Washindi wa Medali ya Dhahabu ya Olimpiki Kuruka Juu.
- Ronaldo, Brazil, Mcheza Mpira wa Miguu, Balozi wa nia Njema na Mwakilishi Maalum wa UNDP katika Kampeni ya Kiulmwengu juu ya UKIMWI.
- Sergey Bubka, Ukraine, Bingwa wa Kuruka kwa Upondo Mshindi wa Medali ya dhahabu, Mwenyekiti KOM, Kamisheni ya Wanariadha.
- Sanath Jayasuriya, Sri Lanka, Mcheza Kriketi na Balozi wa Nia Njema wa UNAIDS.
- Thomas Schmidt, Ujerumani, Mshindi w Medali ya dhahabu kuendesha Mtumbwi wa Slalom.
- Yaping Deng, China, Bingwa Mpira wa Meza Mshindi wa Medali ya Dhahabu mara nne Olimpiki.
- Kipchoge Keino, Kenya, Mkimbajji mbio za kat, Mshindi wa Medali ya Dhahabu Olimpiki mara mbili.
- Nawal El Moutawakel, Morocco, Mshindi wa Medali ya Dhahabu Olimpiki Mita 400.

Ujumbe kutoka kwa wanamichezo hawa unapatikana kila mahali katika kitabu hiki

Sehemu ya 5

5.4 Je, makocha na wanariadha wataitikiaje kushirikiana na wanariadha wanaoishi na VVU?

Watu wanaoishi na VVU hawateswi na ugonjwa wowote bali tu wanaishi na VVU. Kila mara kikwazo kikubwa kwa mtu anayeishi na VVU kushiriki michezo si maambukizi walio nayo lakini zaidi ni mitazamo ya watu wanaowazunguka. Kuwa na VVU inaweza kuwa uzoefu wa upweke sana. Wote wanariadha, makocha na viongozi wa michezo wanatakiwa kuwasaldia watu wanaoishi na VVU; kuwafanya kuwa sehermu ya timu, na kuwaheshimu na kuwapongeza karna unavyoweza kufanya kwa mtu mwingine yeoyote.

Hazijakuwepo taarifa zozote zilizothibitishwa za maambukizi katika nyanja za michezo. Kwa hiyo, **hakuna kizuizi cha jumla kwa watu wanaoishi na VVU cha kutocheza michezo kwa kuwa tu wao wanaishi na VVU**. Kwa ujumla, uamuzi wa kumruhusu mtu anayeishi na VVU kushiriki michezo lazima ufanywe kwa msingi wa afya ya mtu binafsi.

- Kumbuka kwamba hatari ya kupata maambukizi ya VVU katika nyanja za michezo ni ndogo sana. Hauhitaji kujua hali ya VVU ya wachezaji wenzako; lisipokuwa tekeleza **tahadhari za kiulimwengu za damu**, kama kuna kidonda kinachotoka damu au ngozi iliyio na maambukizi. Hii itakulinda kutokana na maambukizi yanayoambatana na damu ikiwemo VVU.
- Wakati wa michezo, wanariadha lazima wawe makini na **vidonda vya wazi** na wanapaswa kumpa taarifa kocha au mkufunzi, n.k. Lakini hata hivyo makocha, maafiga na wachezaji wengine wanapaswa kuwa makini na vidonda vinavyotoka damu.
- **Wanariadha wanaotoka damu wanapaswa waondolewe mchezoni** na kudhibiti utokaji wa damu, kwa kufuata taratibu za kiulimwengu za tahadhari ya damu. Mchezaji asiruhusiwe kurudi mchezoni hadi pale damu inayotoka imedhibitiwa na kidonda kimesafishwa, vizuri, kimetibiwa na kufungwa vizuri.
- **Utambulisho wa mtu anayeishi na VVU lazima uwe wa siri.** Watu – wakiwemo makocha na wanariadha, ambao mtu anayeishi na VVU amearua kuwashirikisha hali yake ya VVU, ni lazima waheshimu usiri huu katika kila jambo na wakati wote, labda tu pale mtu amechagua kultweka wazi jambo hili.

Inawezekana na kwa baadhi ya maeneo kuna uwerekano kwamba wapo wachezaji ambao wanaishi na VVU au wameathriwa kwa UKIMWI. Wengi kati ya wanamichezo hawa wasingependa kufahamika ya kwamba wanaishi na VVU au wamepoteza mzazi mmoja au wawili kutokana na UKIMWI: au wangependa kuzungumzia hali hiyo waziwazi. **Hakikisha ya kwamba wanamichezo hawa wanajisikia kusaidiwa na kujumuishwa** katika klubu na kwamba hisia zao zinaheshimiwa. "Ni kwa jinsi gani tutawasaidia wanamichezo wenzeru wanaoishi au kuathiriwa na VVU?" ni swali linalohitaji kujibiwa na makocha na wanariadha.

Kama makocha na viongozi wa michezo tunahitaji:

- kuwa tayari **kupitia upya tabia zetu** zinazopingana na yale tunayotaka wachezaji wajifunze; kama vile mizaha inayonyanyapaa watu wanaoishi na VVU;
- **kuzungumza na wanariadha wote**, wakiwemo wachezaji wanaoishi na VVU kuhusu lishe na mapumziko ya kutosha. Hakikisha kuwa tahadhari za kiulimwengu kuhusu damu zinafuatwa wakati majeraha yanayosababisha damu kutoka yanapotokea; na
- kutambua na pia kuwa tayari **kutetea na kulinda hakiki** na matakwa ya wale walio na mahitaji makubwa, wakiwemo watu wanaoishi na kuathirthiwa na VVU.

Sehemu ya 5



Sehemu ya 5

"VVU havibagui. Watu wanabagua"

Kama wanariadha na wanamichezo tunahitaji:

- **kuwa rafiki wa kwelli.** Rafiki aliye na VVU yungali rafiki yako. Huwezi kupata VVU kwa kushiriki michezo, kushikana mikono au kufanya kazi pamoja;
- **kuwakubali watu.** Watu wanaoishi na VVU hawatafuti huruma zako bali msaadaa wako. Wanahitaji fursa ile ile ulio nayo kuishi maisha yao katika ukamilifu wake wote...pote ndani na nje ya uwanja wa michezo;
- **kujipatia taarifa sisi wenyeewe.** VVU vinaweza kuleta hofu kwa hiyo jipatia taarifa wewe mwenyeewe. Ikiwa utafanya hivyo basi utaona ya kuwa hakuna kitu cha kuhofia kuhusu watu wanaoishi na VVU. Fuata tu utaratibu;
- **tusiogope.** Hakuna haja ya kuwa na woga kuhusu mtu anayeishi na VVU. Mtendee mtu aliye na VVU vile vile kama ambavyo ungependa mtu akutendee endapo ungekuwa na VVU; na
- **kufuata maagizo ya kocha** ikiwa kuna kujeruhwa kuliikoambatana na damu.

Shughuli nyingine za kusaidia ushiriki wa watu wanaoishi na VVU:

- kufanya kazi pamoja na vijana wanaoishi na walioathiriwa na VVU ili kuwawezesha kukabiliana na uyanyapaa unaohusishwa na VVU;
- kuwashirikisha wanamichezo wa kike na kieme wanaoishi au kuathiriwa na VVU na UKIMWI kama wawezeshaji katika programu na shughuli zako za michezo.



"Ubaguzi unaweza kuzula watu kutumia uwezo walio nao. Usiwabaguzi watu wanaoishi na VVU."

Muaustralia Mshindi wa Medali ya Dhahabu ya Olimpiki, Michuano ya Mbio na Uwanjani

Kisanduku cha 6: Makocha na wanamichezo wakishirikiana na wanariadha wanaoishi na VVU

- wanariadha wanaoshi na VVU inapaswa waruhusiwe kushiriki katika aina zote za mashindano ya michezo;
- wanariadha wanaoishi na VVU inapaswa wafahamishwe juu ya hatari zote za kuweza kuwaambukiza watu wengine;
- haki za kutunziwa siri kwa mwanariadha anayeishi na VVU inapaswa ziheshimiwe;
- upimaji wa VVU wa kila mara kwa wanariadha usifanyike;
- miongozo ya kusitiza wanariadha wajepushe na kujidunga madawa ya kuboresha ufanisi wao katika michezo inapaswa ilmarishwe; na
- wanariadha wote inapaswa wapate ushauri nasaha kuhusu hatari za maambukizi ya VVU kwa njia ya kujamiliiana.

Sehemu ya 6



LA84



UCS

Sehemu ya 6

Mwitikio wa Mashirika ya Michezo katika mapambano ya VVU na UKIMWI

6.1 VVU/UKIMWI katika Sehemu ya Kazi

"Kila mmoja wetu, katika kiwango chetu binefsi, anaweza kufanya kitu fulani kuwua maambukizi zaidi ya VVU na kuepuka ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU."

Nawal El Moutawakel, Morocco, Mshindi wa Medali ya Dhahabu, Olimpiki Kuruka Vihunzi, Mita 400.

Wajibu mmojawapo wa Kamati za Olimpiki za Taifa, vilabu nya michezo, mashirika au shirikisho ni kuwa sawa na mwajiri. Inawezekana ya kwamba kuna waajiriwa katika shirika lako ambao wanaishi na VVU au warneathiriwa na UKIMWI. Wengi ya waajiriwa hawa wanaweza wasipende kujulikana ya kwamba wanaishi na VVU au ya kwamba wamepoteza marafiki au ndugu kwa UKIMWI. Wengine wangependa kulizungumzia kwa uwazi kabisa.



Mara nyingi itikio la awali kwa VVU na UKIMWI ni kile tunachoweza kuwafanya wengine kabla kwanza ya kuhakikisha ya kwamba nyumba yetu ipo sawa. Mashirika ya kimechezo yasijaribu tu kuhakikisha ya kwamba wachezaji wao wanallindwa dhidi ya maambukizi ya VVU na hawanyanyapai au kuwabagua watu wanaoishi na VVU na UKIMWI; ni lazima yahakikishe ya kwamba mahali pa kazi ni mazingira salama kujadili VVU na UKIMWI na si yenye kubagua. Kila mwaajiriwa anahitaji kuwa na ujuzi kuhusu UKIMWI, kama ilivyo shirika.

Hakuna mkakati wa VVU na UKIMWI wa mahali pa kazi ambao utafaa kwa kila shirika; kila shirika la michezo linahitaji kuzingatia mazingira yake na kutafuta njia suluhishi kama inavyotakiwa. Hata hivyo, inawezekana kutambua vipengele muhimu vinavyopaswa kuwemo katika mkakati wa mahali pa kazi.

Mwezi Juni 2001, Shirika la Kazi Duniani (ILO) liitengeneza **Kanuni ya Utendaji Juu ya VVU na UKIMWI katika Ulimwengu wa Kazi**⁹. Hatimaye, KOK liithibitsha Kanuni ya utendaji, ambayo ina kanuni za kimsingi za kuendeleza sera na miongozo halisi ambamo kutoka humo miitikio yenye nguvu inaweza kuendelezwa katika ngazi za kibia shara,¹⁰ kijumuia na kitaifa katika maeneo yafuatayo:

- kuzuia maambukizi ya VVU;
- utawala na upunguzaji wa makali ya matokeo ya VVU na UKIMWI katika ulimwengu wa kazi;

⁹ <http://www.ilo.org/public/english/protection/trav/visa/code/codesain.htm>.

¹⁰ Tazara Klamhatashanishii 1 sera ya UKIMWI ya Kamati ya Olimpiki ya Kijamhuri. Kamasi ya 1. Wajibu wa KOK.

Sehemu ya 6

- huduma na msaada kwa wafanyakazi wanaoishi na kuathirika na VVU na UKIMWI; na
- kuondoa unyanyapaa na ubaguzi kwa msingi wa kuwepo maambukizi ya VVU kwa mhusika kwa uhakika au kwa dhana.

Shirika lako la michezo linaweza kuwa na ujuzi juu ya UKIMWI kuitia shughuli zifuatazo:

Kazi ya Sera

- kuitia kwa makini Sera ya VVU/UKIMWI ya KOK (Tazama **Klambatanishi cha 1**), ambayo imenorodhesha shughuli maalum za KOT na kuona jinsi itakavyoweza kutekelezwa na jumuia yako ya michezo;
- kuandaa na kutekeleza sera ya VVU na UKIMWI ya mahali pa kazi kwa shirika lako;
- kuhakikisha ya kwamba maeneo mbalimbali yanayohusu jinsia katika masuala ya VVU na UKIMWI yanazingatiwa katika sera zozote zinezotengenezwa; na
- kuhimiza na kutoa msaada kwa utafiti juu ya unyanyapaa na ubaguzi katika nyanja za michezo.

Shughuli za Kuzuia maambukizi ya VVU

- kusaidia watu katika shirika lako kujifunza ukweli kuhusu VVU na UKIMWI;
- kujumuisha katika mipango ya mafunzo kwa ajili ya makocha, wasimamizi na wanariadha (mafunzo kwa wakufunzi) mafunzo ya ufahamu wa UKIMWI;
- kuhakikisha ya kwamba tahadhari za kimataifa kuhusu damu zinatekelezwa katika tukio la kujikata au kupata maambukizi ya ngozi katika uwania wa michezo; na
- kuendeleza, au pale inapowezekana, kutoa ushauri nasaha wa hiari (wa siri) na upimaji wa VVU.

Huduma na Msaada

- kuhakikisha ya kwamba watu wanaoishi na VVU wanaruhusiwa kushiriki katika michezo;
- kujifunza kuhusu kuwa wazi na kwenye msaada kwa watu wanaoishi na VVU katika familia zetu, vilabu na jumuia;
- kutambua kuwepo kwa usumbufu wowote unaohisi juu ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI na kujifunza ukweli kuhusu VVU na UKIMWI ili kwamba usiwaogope watu wanaoishi na VVU na UKIMWI;
- kusaidia chama cha jumuia kwa shughuli ambazo zinasaidia kufanya jumuia zetu kuwa salama kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI;
- kuepuka kauli katili na zisizojenga kuhusu kundi lolote la watu, wakiwemo watu wanaoishi na VVU na UKIMWI;
- kutumia imani zako za kidini kwa namna zenyenye kujali; na
- kushiriki katika shughuli za kuadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani na kuvali Utepe Mwekundu ni njia za kuongeza ufahamu na kuonyesha "mshikamano wa timu" na watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Utetezi

- kusaidia juhudzi za kufanya utetezi katika ngazi ya jumuia, kitaifa, au kimataifa, kwa mfano, upatikanaji wa tiba na kampeni dhidi ya unyanyapaa.

Sehemu ya 6

Ni muhimu kwamba unaziunganisha, shughuli na mipango yako na **mashirika ya UKIMWI ya Jumula**. Hayo yanaweza kusaidia katika mafunzo na katika kutoa vifaa vinavyohusu VVU na UKIMWI na vile vya kufundishia. Baraza lako la Michezo la Taifa na vyama husika, ikiwemo Kamati ya Olimpiki ya Taifa, vinaweza kuwa na mafunzo ya msingi ya VVU na UKIMWI, na vifaa. Pia uwe na mawasiliano na **Mabaraza ya UKIMWI ya Taifa** ili kwamba shughuli na ujumbe zinaratibiwa. Haya yanaweza kuwa yenye msaada katika kustawisha vikundi nya ushirikiano na kuwa na uwezo wa kutoa vifaa.

6.2 Sera ya UKIMWI mahali pa kazi?

Maamuzi ya kisheria bado hayajafikiwa ikiwa VVU na UKIMWI ni lazima vishughulikiwe kupitia sera pekee au kuwa sehemu ya sera kuu ya magonjwa sugu. Mashirika mengi yanaanza kwa kuandaa sera maalum ya VVU na UKIMWI kwa sababu wanahitaji kuitika kwa haraka na kwa wazi katika janga hili la UKIMWI na kwa sababu kuna vipengele kadhaa, hasa unyanyapaa na ubaguzi, ambaa ni wa kipekee katika VVU na UKIMWI. Hata hivyo, kwa wengi lengo kuu la mwisho ni kujumuisha hili na sera nydingine (k.m. magonjwa sugu, mafao ya kimatibabu sera za rasilimali watu). Ni kwei, kwa mashirika mengi, taratibu za kutengeneza sera iliyo kamiliika ya VVU na UKIMWI inaweza kuwa kichocheo cha kufanya marejeo kufahamu ubora wa maeneo yaliyoshirikishwa, kama vile mafao ya kimatibabu.

Ikiwa shirika lako la michezo litaamua kutengeneza sera ya VVU na UKIMWI ya mahali pa kazi, liongeze yafuatayo:

- malengo ya sera
- ufanuzi
- wajibu wa utekelezaji
- usiri
- migawanyo ya kijinsia
- taratibu salarna (kujaamiana au nyingezezo)
- mazingira ya kazi yenye hatari ya kuambukiza
- bima ya afya (mke, mwenza, na watoto)
- matibabu yaliyopo (magonjwa nyemelezi, patholojia, dawa za kuboresha maisha)
- ushauri nasaha na upimaji wa hiari
- kuajiri wafanyakazi wanaoishi na VVU
- kupima VVU na ajira
- habari na mafunzo
- malazi yanayofaa
- unyanyapaa na ubaguzi
- utetezi kwa upatikanaji wa matibabu klulimwengu.
- kusafiri
- kazi na chanjo
- ulemavu
- kukoma kwa ajira
- taratibu za manung'uniko na za kinidhamu

Nyaraka Rejea:

Kanuni ya utendaji ya VVU na UKIMWI katika Ulimwengu wa Kazi ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) (June 2001).

<http://www.ilo.org/public/english/protection/trav/aids/code/codemain.htm>

Kanuni ya utendaji inawakilisha juhudii za ILO kusaidia kupata kazi za kufaa na zenye usalama wa kijamii mbele ya janga na kuwa na mkaakati wa mpango wa mahali pa kazi.

Sehemu ya 6

Hii ina kanuni za msingi za kuendeleza sera na miongozo ya kiutendaji itakayo saidia kupatikana kwa matokeo bora katika ngazi ya kituo, jumuiya, na kitaifa.

Mwitikio wa Biashara kwa UKIMWI/Mwitikio wa Kazi kwa UKIMWI (mpango wa BRTA/LRTA)
Kituo cha Kudhibiti Magonjwa, Marekani (CDC).

<http://www.hivetwork.org/tools/business-managers.cfm>

Kisanduku cha Meneja kina nyenzo zote za sekta ya biashara inayohitaji kutengeneza programu kamili za za VVU na UKIMWI mahali pa kazi. Kisanduku kinapatikana kwa Kiingereza na Kispania.

Kufanya Kazi kwa Ubora: Muongozo kwa Asasi za Kiserikali zinazosimamia VVU na UKIMWI mahali pa Kazi. Shirikisho la UKIMWI Uingereza

<http://www.aidsconsortium.org.uk/Workplace%20Policy/workplaceintro.htm>

Muongozo huu unaangalia masuala makuu yanayohusika katika kuandaa mikakati wa utendaji mahali pa kazi na jinsi Asasi tofauti zisizo za kiserikali na mashirika ya kibashara yanavyofanyia kazi masuala haya. Inatoa pia muongozo kwa mambo makuu yallyomo katika mkakati wenye mafanikio na orodha ya nyaraka rejea.

Mpango wa Mahali pa kazi wa VVU/UKIMWI: Muongozo wa utendaji kwa Mameneja

http://www.fhi.org/en/HIV/AIDS/pub/guide/Workplace_HIV_program_guide.htm

Muongozo wa utendaji wa mahali pa kazi kutoka shirika la Family Health International, mradhi wa IMPACT ni ambaao unaweza kufanya kazi, hivyo unapelekea namna ya kutoa muongozo, ushauri kwa mameneja namna ya kutengeneza mipango ya mahali pa kazi katika nchi zinazoendelea. Haya mafunzo yanaelekezwa kwa uzoefu ulio wazi wa waaejiri katika UKIMWI mahali pa kazi.



Sehemu ya 6

6.3 Elimu ya UKIMWI kwa mwajiriwa

Ni muhimu kutoa mafunzo ya VVU na UKIMWI kwa wale walio katika **ngazi ya utawala** wa shirika klabla hujaanza kuelimisha wafanyakazi wengine walibaki. Mameneja lazima waelewe ukweli juu ya VVU na UKIMWI na chama chako cha michezo lazima kiweze kufanya yafuatayo:

- kuwa tayari kujibu maswali ya waajiriwa;
- kujuu wapi kumtuma mwaajiriwa ili kupata msada au taarifa za nyongeza;
- kuwa na uwezo kudumisha au kuendeleza msimamo wa chama cha michezo juu ya VVU na UKIMWI; na
- kuwaunga mkono na kuwapa moyo waajiriwa wao kuhudhuria vipindi nya mafunzo.

Unaweza kutumia shughuli hizo hizo kama zilivyoorodheshwa katika kurasa zinazofuata kwa wote mameneja na waajiriwa.

Vipindi nya Mafunzo ni wakati mzuri kuitia taarifa nyingi za msingi, kama slyo zote kuhusu VVU na UKIMWI, kuelezea sheria za nchi na sera za mashirika ya michezo na pia kupata taarifa juu ya huduma zinazohusika na VVU za mahala. Inapaswa vipindi viendeshwe angalau mara moja kwa mwaka na pale idadi kubwa ya waajiriwa wapya wanapoandikwa kazini, vipindi vingi nya mara kwa mara viandaliwe au kujumishwa katika programu elekezi zilizopo.

Vipindi nya mafunzo vinatakiwa kutoa **taarifa ya mawasiliano** kwa taasisi za kienyeji zinazotoa huduma za VVU na UKIMWI kama vile upimaji wa hiari na vituo nya ushauri, wanaoishi na VVU na UKIMWI na mashirika yanayoishughulisha na masuala ya UKIMWI. Pia itoe taarifa na ukurasa mmoja kuelezea hali halisi ya UKIMWI katika jamii ili kuwafanya watu wajue wapi waende wakiwa na maswali ya ziada.

Kwa kuwa michezo inahusika katika afya na uzima moja kwa moja, ni vyema kuhusisha **taarifa zinazo husiana na afya** katika kila kipeperushi pamoja na taarifa za VVU. Japokuwa si njia sahihi katika elimu kwa jamii. Vipeperushi hiyo vinatoa taarifa sahihi iliyotayarishwa ili kuelimisha jamii na hupunguza mwitikio mbaya wa jamii kama uwepo wa mwanamichezo aliye na VVU ukajulikana kwa umma. Wale wanaohusika na mwitikio mbaya wa umma kuhusu kuwepo mwanamichezo aliye na VVU wanaweza kufikiria, haja ya kuwa na mafunzo na elimu kwa jamii.

Kwa kiwango cha chini:

- waajiriwa wanapaswa washiriki katika **mafunzo rahisi ya maelekezo** juu ya VVU na UKIMWI pamoja na maonyesho ya namna ya kutumia kondomu za kike na kiume (Tazama kiambatanisho cha 4);
- waajiriwa wanapaswa washiriki katika **mafunzo** ili kuinua ufahamu juu ya watu wanaoishi na VVU na kuongeza ufahamu wa kila mtu kuweza kuambukizwa VVU; na
- kuonyesha mabango ya matangazo ya VVU na UKIMWI mahali pa kazi kwa bidii sana.

Kurasa zifuatazo zinaonyesha namna ya kuvunja ukimya kwa kuanza kazi na muhtasari wa shughuli juu ya:

- maambukizi ya VVU;
- matumizi ya komdomu;
- upimaji na ushauri wa hiari (kwa siri);

Sehemu ya 6

- unyanyapaa na kutengwa; na
- kutengeneza mazingira tegemezi

Rejea Sehemu ya 4 Nini unachopaswa kujua, Sehemu ya 5 Michezo na VVU na Kiambatanishi cha 4 Kondomu.

6.3.1 Kuvunja ukimya :

Huku kuvunja ukimya kuwafanye watu wafikiri na kuzungumza! Hiki ndicho kiini cha kuzuia VVU na itaongeza ufahamu juu ya tabia mionganini miwa wafanyakazi.

Lifanye liwe jambo la kufurahisha kwa watu. Kama inaweze kana, uliza maswali siku kadhaa kabla ya wakati, au jioni kabla matokeo hayaletwa, au labda kabla ya chakula cha mchana au kabla ya mapumziko ili kukupa muda mwingi wa kukusanya matokeo.

Hatua ya 1:

Waambie watu kuandika majibu ya maswali utakayo uliza kwa sauti. Fafanua kuwa karatasi za majibu zitakusanywa mwishoni mwa zoezi, lakini majibu yatakuwa ni siri na hayatakuwa na majina.

Hatua ya 2:

Uliza maswali yote au baadhi ya haya maswali au yote. Unaweza kuamua kuacha baadhi ya maswali na/au ukaongeza.

- Ulijamiliana kwa mara kwanza ukiwa na umri gani? Kama hukumbuki umri halisi, unaweza kukisia (iwapo watu watakuuliza una maana gani "kujamiliana," waambie ni juu yao wao wenyeve kuarmua!)
- Katika umri gani ultumia kondomu ya kiume/kike kwa mara ya kwanza? (kama hujawahi kutumia sema sijawahi)
- Unaweza kujisikia jasiri na kuonyesha namna ya kutumia kondomu ya kiume/kike?
- Uliwahi kufanya mapenzi ukiwa umeleva pombe au madawa ya kulevyo?
- Kama uko (au ulikuwa) katika ndoa au mahusiano, ulishawahi kufanya mapenzi nje ya ndoa au mahusiano uliyonayo (siyo na mumeo/mkeo/mpenzi)?
Kama umeolewa (au uliwahi kuolewa) au uko katika mahusiano, ulishawahi kuwa na mazungumzo yenye maana na mpenzi wako juu ya VVU, pamoja na masuala yanayohusu kuaminiana na athari zake?
- Huwa unabeba kondomu kila wakati ukisafiri?
- Ulishawahi kuugua ugonjwa/magonjwa ya zinaa?
- Tangu ulipofahamu juu ya VVU, ulishawahi kufanya mapenzi yasiyo salama na mtu ambaye hujui hali yake hasa kama ameambukizwa VVU?
- Ulishawahi kupima VVU?
- Kama ulishawahi kupima, tangu upime mara ya mwisho, ulishawahi kufanya mapenzi bila kondomu na mtu ambaye hujui hali ya afya yake?
- Je, wewe una VVU, huna VVU, au hujui hali ya afya yako?

Sehemu ya 6

Inawezekana pia ikawa vyema kuwauliza watu kujitambua kama ni wanaume au wanawake na kuonyesha majibu kwa jinsia na chunguza tofauti.

Hatuu ya 3:

Maswali yakishajibiwa, kusanya karatasi za majibu. Yapange majibu kisha yawasilishe kwa washiriki.

Dokezo namna ya kuwasilishe majibuz:

- Onyesha muainisho baina ya wanaume na wanawake;
- Onyesha habari inayohusu swali moja na jingine kwa mfano, wastani wa tofauti katika miaka kati ya mzoefu wa kwanza wa mapenzi na mzoefu wa kutumia kondomu;
- Onyesha kama kuna waliojibu kuwa hawajapima VVU na bado wanasema hawana VVU;
- Onyesha kama kuna watu wanaosema tangu wapime afya zao mara ya mwisho, wamefanya ngono isiyo salama na mtu ambaye hawakujua afya yake na bado wanasema hawajaambukizwa VVU.

Hatuu ya 4:

Zungumzia kuhusu matokeo juu ya namna ambavyo washiriki wako katika hatari ya kuambukizwa VVU.

Hii hufanywa vizuri kwa kugawana taarifa na kuwauliza watu kuelezea taarifa hizo na kuchunguza wao wenyewe.



Sehemu ya 6

6.3.2 Maambukizi ya VVU

Rejea Sehemu ya 4 Nini unapaswa kujua na Sehemu 5 Michezo na VVU.

1. Mambo ya kujifunza kwa ujumia

Kwa muhtasan elezea njia ambazo VVU huambukizwa, chagua moja au zaidi katika mambo yafuatayo:

- waujize watu waseme njia za msingi za maambukizi ya VVU;
- mfano, mtaalamu wa VVU aonyeshe kwa ufupi jinsi VVU vinavyoambukizwa na namna inayyoathiri nchi;
- muombi mtu anayeishi na VVU na UKIMWI aongee. Mara nyingi watu wanaoishi na VVU ni wazuri kuelezea hali halisi ya kuishi na VVU.

2. Hali za utata (Maelezo yapo katika mabano)

Kisa cha 1

Mtu anayeishi na VVU anasaidia kuandaa chakula wakati wa sherehe ya wafanyakazi. Akiwa anakata, vitunguu moja kwa moja kwenye sufuria ya mchuzi, kwa bahati mbaya akajikata kidole na matone ya damu yakadondonokea kwenye mchuzi.

(**Hakuna hatari: joto lilioko kwenye mchuzi litaua virusi.**)

Kisa cha 2

Mtu anayeishi na VVU anakwenda kwenye sherehe ya kumuaga mtu anayeondoka. Kila mtu anambusu kwaheri anayeondoka na anayeishi na VVU anambusu pia.

(**Hakuna hatari: kubusu hakuwezi kuambukiza VVU hasa busu la kawaida ambayo haina mbadilishano wa majimaji ya mwiliini!**)

Kisa cha 3

Mtu anahudhuria katika chakula cha jioni arba kuna kilevi au pombe. Baada ya muda, watu wawili wanaamua kuondoka na kurudi katika chumba cha hotel na kuanza kufanya ngono. Kati yao hakuna aliye na kondomo na wanaendelea kufanya ngono. Baada ya tendo mmoja wao anagundua kilichotokea na kwa angalifu lakini anafuta sehemu zake za siri kwa kileo.

(**Hatari kubwa: kusafisha baada ya ngono hakuzui maambukizi ya VVU. Ngono salama inazula.**)

Kisa cha 4

Wanamichezo wawili wanasaferi pamoja. Kwa sababu ya kukosa hoteli, wanalazimika kuchangia chumba pamoja. Asubuhi mmoja wao anagundua kuwa amesahau mashine ya kunyolea na anahitaji kunyoea kwa kuwa wana mkutano wa muhimu. Anaazima wembe wa kunyolea kutoka kwa mtu mwingine.

Sehemu ya 6

(Hatari ndogo: VVU vinaweza kuishi nje ya mwili katika majimaji kwa muda mfupi, japo si ndani ya damu iliyokauka. Tukio hili linaonyesha hatari kwa kiwango cha chini.)

Kisa cha 5

Mtu anayeishi na VVU anasafiri kwenda kuangalia mchezo na ajali ya gari inatokea. Anayeishi na VVU anaumia na kuvuja damu. Mtu mwininge anamsogelea na kujaribu kuzuia damu kutoka kwa kufunga vidonda na kitambaa safi.

(Hakuna hatari: hasa ikiwa yule anayemsaidia hana majeraha au vidonda. Kugusa damu hakuwezi kusababisha maambukdzi ya VVU, kwa asili damu hutoka nje ya mwili na haitaingia ndani ya mwili wa yule anayetoa msaada.)

6.3.3 Matumizi ya kondomu

Rejea taarifa katika Kiambatanishi cha 4. Kondomu.

1. Shughuli za kujifunza kwa ujumla:

- Onyesha kondomu ya kiume na kike: mwishoni mwa shughuli ya kujifunza, watu wawe na uwezo wa kutumia kondomu zote za kiume na kike;
- Ukweli kuhusu kondomu, maoni na uzushi wa uongo: kumruhusu kila mmoja kutenganisha ukweli, maoni na uzushi wa uongo kuhusu kondomu;
- Kushauriana juu ya matumizi ya kondomu: kuwaruhusu watu kuongea kwa pamoja namna wanavyoweza kushauriana na wenza wao kutumia kondomu.

2. Kushauriana juu ya matumizi ya kondomu

Hatua ya 1:

Anza kwa kueleza kwamba wakati mwininge mwenza mmoja anaweza kutaka kutumia kondomu, lakini mwininge anaweza asitake kufanya hivyo. Kipindi hiki kitakuwa ni nafasi ya kufanya maigizo juu ya baadhi ya matukio yanayoweza kujitekeza katika mazingira haya.

Hatua ya 2:

Wagawe watu katika vikundi vidogovidogo na waambie wachague kati ya haya yafuatayo:

- "Lakini, mpenzi, ngono kwa kondomu siyo ngono hasa."
- "Lakini hatuwezi kuwa na uhakika ya kwamba kondomu haitapasuka!"
- "Sipendi kutumia kondomu kwa sababu zinaweza kupotelea kwenye uke wangu au mkunduni"
- "Lakini nimemeza vidonge siwezi kupata mimba!"
- "Lakini nimesikia kondomu zina VVU na zinasababisha ugonjwa!"
- "Kwa nini tutume kondomu wakati sote tu waaminifu kwa kila mmoja wetu, je, hatuko hivyo?"
- "Lakini ngono haina raha ukutumia kondomu!"

Sehemu ya 6

- "Tukitumia kondomu kila wakati tunapofanya ngono tutafisika! Kondomu zinagharimu pesa nyingi!"
- "Kondomu zitanisababishia kuwashwa na maumivu."
- "Nikitumia kondomu, sijisikii kuwa karibu na wewel!"
- "Kondomu ni ndogo kwa uume wangu! Zinabana sana na zinaniumiza!"
- "Kondomu zisizo bora ndizo zinazoletwa nichini kwetu, kwa nini tuzitumie?"
- "Kondomu zinazua mzunguko wa damu na zitaukaba uume wangu."

Waweke watu wafanye igizo mwenza mmoja akianza kwa kutumia moja ya sentensi hizo hapo juu (au zingine ambazo watu wanaona zinaweza kujitokeza) na mwininge akijaribu kushauri matumizi ya kondomu. Waambie wafurahie.

Hatua ya 3:

Katika kusanyiko la pamoja omnia igizo moja kutoka kila kundi ili lichezwe.

Hatua ya 4:

Hitimisha kwa mjadala, ikiwemo uchunguzi au 'mbinu' za namna ya kujadiliana kuhusu kutumia kondomu.

6.3.4. Ushauri nasaha (na wa siri), na kupima kwa hiari

Waulize watu wajibu "ndiyo" au "hapana" kwa maswali yefuatayo. Baada ya watu kujibu maswali kila mmoja, ongoza mjadala kwa kutoa majibu sahihi na hakikisha kwamba kila jibu limeeleweka. Sababu zinaainishwa chini ya maswali.



1. Mara nyingi watu huamus kupima VVU iwa sababu wana wasiwasi na tabia ambayo inaweza kuwa imewaweka hatarini.

Kwelli

Kuwa katika mazingira ya kuambukizwa ni moja ya sababu ya msingi inayopelekea watu kuarmua kupima. Nia ya kulinda afya za wengine na kuzula hofu inayosababishwa na "kutokujua" ni sababu nyingine.

2. Hakuna umuhimu wowote wa kupima, kwani ikiwa nimeambukizwa itanitia alama ya kuwa ninalishi na VVU, lakini kwa uhakika hakuna zaidi ninachoweza kufanya.

Si kwelli

Kupima VVU inaweza isiwe rahisi, lakini ina faida. Leo, watu wanaoishi na VVU wanaweza kuendelea kuwa na afya nzuri kwa muda mrefu kwa sababu ya kuhudumiwa vyema na matibabu. Pia, kujua halii yako kunakufanya uchukue hatua ya kuwalinda wengine na maambukizi.

3. Kipimo cha VVU kinaweza kukuonyesha ya kwamba una UKIMWI

Si kwelli

Kipimo cha VVU kinaweza tu kukuonyesha kama umeambukizwa VVU kwa kugundua kingamwili, ya virusi ambazo mwili wako utatengeneza kama utakuwa umeambukizwa. Kumbuka kuwa, huchukua hadi miezi sita tangu VVU kulingia mwilini ili kuwepo kingamwili za kutosha kugundulika. Kama mtu ana kingamwili za VVU, maana yake ni kwamba ameambukizwa VVU.

Sehemu ya 6

Kipimo cha VVU hakiwezi kukueleza kama una UKIMWI ni daktari wako tu ndiye anayeweza kuthibitisha. Ni muhimu kukumbuka ya kwamba watu wengi wanaoishi na VVU huonekana na hujisikia kuwa na afya njema kwa angalau miaka mitano hadi kumi ya maambukizi ndipo wanapoweza kuanza kuonyesha dalili zinazohusika na maradhi ya UKIMWI.

4. Kuwa na dalili kama kutoka jasho usiku na kupungua uzito inaweza kumaanisha ya kwamba nimeambukizwa VVU.

Kweli

Lakini dalili hizi zinaweza kusababishwa na magonjwa mengine na inatakiwa kuchunguzwa na daktari. Njia pekee ya kujua kama umeathirika ni kupima. Watu wenye VVU mara nydingi hawaonyeshi dalili kwa miaka mingi. Usisubiri, kushangaa na kuwa na wasiwasi kuhusu hali yako na VVU nenda kapirme.

5. Mwenza wangu hakuonekana na VVU baada ya kupima, kwa hiyo hii ina maanisha sijaambukizwa.

Si kweli

Majibu ya mwenza wako si kipimo ya kwamba umeambukizwa VVU. Njia pekee ya kujua hali yako ya VVU ni wewe mwenyewe kupima afya yako.

6. Kama nilifanya ngono isiyo salama na mtu ambaye hali yake ya VVU haljulikani kwangu ninatakiwa kufanya kipimo cha VVU.

Kweli

Vipimo vya VVU vinashauriwa kwa watu ambao warnefanya ngono isiyo salama (hawakutumia kondomu) iwe kwa mkundu au ukeni. Wakati kuna hatari kidogo kutokana na ngono ya mdomoni, ukilinganisha na ngono ya kupitia mkunduni au ukeni.

7. Kama nilichangia sindano na mtumia madawa ya kujidunga au nilifanya ngono isiyo salama na anayetumia madawa kwa kujidunga sindano natakiwa kupima VVU.

Kweli

Vipimo vya VVU vinashauriwa kwa wenza wa watumiao madawa kwa kujidunga (kwa wake, wenza wa ngono, au wenza wa kujidunga sindano)

8. Kama nimeongezwa damu kutoka chanzo nisichokuwa na uhakika nacho, ninatakiwa niplimwe VVU.

Kweli

Inashauriwa kupima VVU kama unaongezewa damu au sehemu za damu kutoka chanzo usichokuwa na uhakika nacho, hasa kama uliongezewa damu kabla usambazaji wa damu katika nchi yako haujambatana na utaratibu wa vipimo vya VVU.

9. Kama ninapima VVU, majibu yanafahamishwa kwa wengine.

Si kweli

Upirmaji wa VVU ni siri na kituo chochote cha kupimia lazima kiheshimu usiri. Wewe peke yako ndiye wa kuamua nani wa kumshirikisha majibu yako.

10. Huduma za kitabibu kwa utaratibu hupima VVU kabla ya kumuajiri mfanyakazi na tena wakati wa vipindi vya uchunguzi wa afya

Si kweli

Upirmaji wa VVU siyo sehemu ya uchunguzi wa afya kwa ajili ya ajira na haipaswi kufanyika kama desturi. Ili kupima lazima uombe kupimwa katika kituo cha kupima chenyeh sifa zinazohitajika.

Sehemu ya 6

6.3.5 Unyanyapaa na ubaguzi

Mambo ya jumla ya kujifunza

1. Igizo

Tumia hadithi ya kweli au ya kutunga au uchunguzi kifani unaohusu VVU na UKIMWI katika jumua. Wafanye watu wabuni majukumu na wayaigize. Kwa mifano, igiza tukio ambapo wafanyakazi wawili, mmoja anaishi na VVU na mwiningine muoga kushirikiana na mtu mwenye VVU. Zungumzia jinsi ambavyo mfanyakazi mwenye VVU anavyojsikia kufanya kazi katika mazingira ya kutengwa na kwa nini mtu mwiningine anamuogopa. Elezea ujuzi mpya, mitazamo, hisia na maadili.

2. Unyanyapaa wa kidini

Bila kutaja imani au dini yoyote, waambie watu waandike kwenye kadi moja ya rangi, namna ambavyo dini au mashirikia ya klimani yananyapaa watu wanaoishi na VVU. Katika kadi ya rangi nyiningine, waambie waandike namna ambavyo dini au taasisi za kidini zinavyosaidia kuzuia VVU na ambavyo zimesaidia watu wanaoishi au walioathiriwa na VVU. Zikusanye kadi na uzipange. Kwa ufupi zungumzia matokeo mazuri na mabaya ya jinsi ambavyo dini na taasisi za kidini zimekuwa katika suala la VVU na UKIMWI.

3. Makala za Habari

Kwa kipindi fulani, kusanya makala kutoka kwenye magazeti na majorida yanayoelezea tabia na mwenendo kuhusu VVU na UKIMWI, watu wanaoishi au walioathiriwa na VVU na kuhusu makundi ya watu walio katika hatari ya kuambukizwa VVU au wanaochukuliwa ya kwamba wapo katika hatari kubwa (kama wanaume wafanyao mapenzi na wanaume, wanaofanya kazi mbali na makwao, madereva wa malori, wachimba madini wahamiaji, watumia madawa kwa kujidunga sindano na makahaba.)

Wasilisha kutokana na makala au acha watu wasome sehemu ya makala hizo. Elezea namna ambavyo vyombo vya habari vinaathiri au vinavyoelezea mitazamo na vinavyoweza kuathiri mitazamo yetu wenyewe. Kuhusu VVU na UKIMWI na watu wanaohusika na VVU. Jadili ni nini tunachowea kufanya ili kubadili tabia na mitazamo yetu.



4. Mdahaio wa wazi au mgongano wa mawazo

Maelezo kuhusu VVU yaandalie kablia ya wakati. Watu wawekwe katika kundi la wanaokubali na kundi la wasiokubali na wabishane kwa kila elezo. Wale wanaotetea hawahitaji kukubali binafsi na wanaweza kukataa kama hawajarithika wao wenyewe. Pamoja na mengine yaliyopo maelezo yafuatayo yanaweza kutumika;

- Inakupasa kila wakati kumueleza mpenzi wako hali yako ya VVU kablia ya kufanya ngono.

Sehemu ya 6

- Inapaswa kondomu zipatikane sehemu zilizo wazi.
- Inapaswa wanawake waweze kukataa kufanya mapenzi na wafanyakazi wenzao wa kieme.
- Kila wakati amini kuwa mwenzi au mpenzi wako ni 100% mwaminifu kwako katika masuala ya mapenzi.
- Watu wapimwe VVU kabla hawaaja riwa kufanya kazi.
- Watu wanaoishi na VVU wajisikie huru kuelezea hali zao kwa wafanyakazi wenzao kwa makini.
- Michezo iwe wazi na ichezwe na watu wa mitazamo tofauti katika mapenzi.
- Waalimu wa michezo wenye VVU waruhusiwe kuwafundisha vijana.

Mchezo wa kugonganisha mawazo uruhusu majadiliano ya kina, juu ya mitazamo na imani, kuhusu VVU na UKIMWI na shughuli za ngono.

Unaweza ukatumia namna mbalimbali tofauti za mgongano wa mawazo kama ifuatavyo: weka alama za "Kukubali na Kukataa" sehemu tofauti za chumba, gawa chumba kwa kamba sakafuni. Baada ya kusoma maelezo tofauti kwa sauti waulize watu kupiga kura kwa kwenda kule kunakomaanisha mtazamo wao. Ikiwa wanakubali au kukataa, waende karibu na alama kadiri inavyowezekana. Lakini wanaweza kuchagua kuwa katikati ya zote mbili. Waambie waaeleeze ni kwa nini wana wazo fulani kuhusu uchaguzi wao.

5. Shughuli zingine ya kufanya:

- jihushe na kamperi za kuzuia unyanyapaa wa VVU mahali unapoishi;
- tambua lugha, nyimbo, mikao ya kimichezo na desturi zinazonyanyapaa na hamasisha lugha mbadala zinazojali na zisizohukumu; au
- fanya kazi ya kutengeneza mabango ya kuzuia kuenea kwa VVU na unyanyapaa ukishirikiana na wanamichezo katika eneo unaloishi.

6.3.6 Kutengeneza mazingira

1. Kubungua Bongo

Waongoze watu kubungua bongo juu ya jinsi chombo chako cha michezo na wafanyakazi wenzako wanavyoweza kwa njia bora kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa watu wanaoishi na au kuathiriwa na VVU.

2. Kuandika taarifa za Utetezi

Watu wafanye kazi katika makundi madogo madogo ili kutengeneza taarifa bora za utetezi zinazoweza kutumika zitakazotumika kuonyesha namna ambavyo chombo cha michezo kinawasaidia watu wanaoishi au walioathiriwa na VVU. Uliza kila kundi kuandaa ujumbe mmoja. Jumbe hizi zitawezza kutumika baadaye kwa mabango ya matangazo yanayoandaliiwa katika eneo husika, katika barua pepe, na katika kamperi za UKIMWI za mahali.

Sehemu ya 6

3. Hofu juu ya VVU na UKIMWI, na juu ya watu wanaoishi na VVU

Waambie watu waandike kwa siri kwenye kadi bila kutaja majina yao hofu zozote walizo nazo kuhusu VVU na UKIMWI au watu wanaoishi na VVU. Kisha kusanya kadi na uzipange katika makundi kutokana na aina ya hofu. Elezea kundi moja baada ya jingine, kwa kuelezea namna ambavyo watu wanaweza kujilinda wenyewe na VVU na kuondoa dhana potofu zozote. Angalia kwa makini kila hofu watu wanayoweza kuwa nayo juu ya watu wanaoishi na VVU ili kuweza kuelezea vyema unyanyapaa na ubaguzi uliopo.

4. Mchezo wa kuweka alama

Watu wawekewe alama kwa maneno yanayochukuliwa ya kwamba ni ya kunyanyapaa kama vile, anayelishi na VVU, mama asiyolewa, msagaji, shoga, mtumia dawa za kulevya, n.k.. Alama zibandikwe mgongoni ili mti asiiione alama yake ni nini. Mtu mwingine aeleze namna waliobandikwa alama wanayochukuliwa na jami na mwenye alama fulani ajaribu kukisia alama yake mwenyewe, kutokana na maoni na maswali atakayouliwa.

Kupitia zoezi hili watu wanaweza kujifunza namna ambavyo kuwawekea watu wengine alama kunavyoweza kusababisha kuweka alama na kutenga watu na namna ambavyo hili linaweza kuathiri hisia za wengine.

5. Maneno na misemo

Waaambie watu kwa siri bila kutaja majina, waandike maneno na misemo kwenye kadi wanayo jihuisha au wanayosikia kuhusu VVU au UKIMWI. Waeleze wafikie mahali ambapo wanadhani ni lugha inayokubalika. Lengo la zoezi hili ni kuangalia namna ambavyo maneno na semi zinavyoweza kutia alama, unyanyapaa na zaidi kumuumiza mti ambaye amielengwa pamoja na yule anayeyaeneza. Chunguza kadi hizo pamoja na washiriki na mjadiliane maneno yanayo wawakea watu alama, na ambayo yanaumiza na ni hatari, muone yalikuwa na malengo gani na kadhalika. Jadilianeni kwa nini watu huyatumia na nini kifanyike kutoa elimu juu ya tabia ya VVU na UKIMWI na juu ya makundi ya watu wanaoijihuisha na VVU na UKIMWI.

6. Kupambana na Unyanyapaa na Ubaguzi

Waache watu wafikiri jinsi ambavyo warmewahi kunyanyapaliwa au kutengwa katika maisha yao kwa sababu ya asili yao, dini, elimu, jinsia, na muelekeo wao wa kijinsia, utaifa, hali ya kiuchumi, hali ya VVU, au sababu nyingine. Halafu waambie waandike kwenye kadi walivyojisikia kutokana na ubaguzi na unyanyapaa walifanyiwa. Kusanya kadi na uzipange katika makundi kutokana na sababu za kutengwa. Kwa ufupi elezea athari za kutengwa na unyanyapaa. Halafu eleza nini kinaweza kufanyika katika michezo kuondoa unyanyapaa na ubaguzi wa aina yoyote pamoja na unyanyapaa na ubaguzi unaohusiana na VVU.


7. Shughuli nyingine

- tengeneza na aandaa mazingira mazuri yanayozingatia VVU na UKIMWI katika shirika lako;
- tengeneza na tekeleza sera ya VVU na UKIMWI mahali pa kazi;

Sehemu ya 6

- hamasisha na saidla zaidi utafiti dhidi ya kuryanyapaa na kubaguliwa katika michezo na tumia matokeo ya tafti hizo kutengeneza utaratibu na sera, kuendeleza uwazi na kukubalika;
- wahusisha wanamichezo wanaume na wanawake wanaoishi au walioathirika kwa VVU na UKIMWI kama wataalamu katika mipango na shughuli zako za michezo;
- hakikisha makocha ni mahiri juu ya UKIMWI. Wao wataonyesha umahiri wao kwa kuingiza maswala yanayohusu VVU na UKIMWI katika elimu yao ya ukocha;
- onyesha mabango juu ya kuzuia maambukizi ya VVU;
- toa elimu ya msingi juu ya UKIMWI kwa wafanyakazi na familia;
- gawa vipeperushi vinavyoelimisha juu ya maambukizi na kuzula maambukizi ya VVU;
- karibisha taasisi za nje ili kuelezea au kutoa taarifa kuhusu VVU na UKIMWI;
- unganisha taarifa juu ya maambukizi na kujikinga VVU katika shughuli na mipango yako ya kila siku;
- yafahamu mashirika yanayotoa huduma za VVU na UKIMWI kama upimaji wa hiari, vituo vya ushauri nasaha, mashirika ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI na mashirika yanayotoa huduma za UKIMWI katika eneo lako;
- ongeza mwamiko ili wachezaji na jumuiya waweze kupata huduma kama huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto pale zitakopatikana au fanya mamlaka ziwajibike kama huduma hizi hazipo;
- jumuisha vipengele kuhusu VVU na UKIMWI kwenye kijarida chako na kwenye tovuti na wavuti yako;
- wezesha kupatikana kwa kondomu na vilainishi.

Sehemu ya 7



Sehemu ya 7

Mwiitikio wa Makocha, wakufunzi na viongozi kwa VVU na UKIMWI

7.1 Kuanzisha Kazi ya vikundi ya VVU na UKIMWI

Kazi kwa ajili ya vikundi mbalimbali ya rika tofauti zinazoelezwa katika kurasa zinazofuata zimetengenezwa kwa ajili yako na wachezaji wako ili kujifunza kuhusu VVU, pamoja na jinsi gani ya kujikinga wenye na wengine na maambukizi, pamoja na kuwaheshimu watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Kisanduku cha 7: Makundi tofauti ya rika yako tayari kwa viwango tofauti vya taarifa

Umri kabla ya ujana : miaka 9 hadi 12

Umri huu ni kipindi cha mabadiliko na kukua kwa haraka. Hii hupelekeea kujihusisha sana na mwili, mwonekano, kuwa ‘kawaida’, pamoja na hamu kubwa ya kutaka kujua kuhusu ngono. Baadhi ya watoto katika umri huu huingia katika kipindi cha ubalehe na kuvunja ungo. Mabadiliko ya tabia na kukua kijinsia (kama kutoka matiti, kuota kwa mavuzi, kupariuka kwa matako, sauti nene) huanza katika kilele cha ubalehe. Wasichana wanaweza kukua kijinsia haraka kuliko wavulana. Mashoga na wasagaji huanza kujua mwelekeo wao wa kijinsia katika umri huu na wanaweza kupata hofu kubwa, kuchanganyikiwa na kutengwa katika dunia ya wenyewe mwelekeo wa kuvutiwa na mtu mwenye jinsia tofauti. Vikundi rika huwa ni muhimu. Watoto huzipirna tabia walizojifunza waliopokuwa nyumbani wakilinganisha mtazamo wa vikundi vyao. Watoto hupitia katika shinikizo kubwa la kijamii la kuambatana nayo.

- **Tambua** ya kwamba watoto wapo katika kilele cha utoto na ubalehe;
- **Watoto wanahamu kubwa ya kujua kuhusu ngono, hivyo taarifa sahihi zinatakiwa na ndipo wanaweza kuelewa ya kwamba kujamilaana kunaweza kuwa na madhara, pamoja na kuambukiziwa VVU na mimba;**
- **Wafundishe watoto** kuhusu kwenda hedhi, kondomu (tazama kiambatanishi 4) afya ya uzazi, kujikinga maambukizi ya magonjwa ya zinaa na VVU na maamuzi sahihi kuhusu kufanya ngono;
- **Fikiri kufundisha** kuhusu matumizi ya kondomu na sindano salama- hii haitaleta matokeo ya vijana kufanya ngono au kujaribu madawa, bali itasaidia kuinda usalama na afya zao. Wanaweza kuelewa maelezo yote kuhusu maambukizi ya VVU na na kujikinga;
- **Kumbuka** kwamba tamaduni nyingi huweka msisitizo kwa vijana chipukizi kadiri milli yao, homoni na hulka zinavyobadilika. Hiki ni kipindi cha kuwaeleza maadili kuhusu mahusiano ya kijinsia, kutumia madawa na mambo mengine kwa mazungumzo. Wasikilize kwa makini na uwaeleze unavyojisikia kuhusu mambo haya;
- **Washauri** vijana kutokutumia pombe na dawa za kulevyia na uwe mfano mzuri wa kuigwa.

“Nimi si muathirika. Ni mjumbe.”

Arthur Ashe anayeishi na VVU, Bingwa wa mchezo wa Tenisi.

Sehemu ya 7

Vijana : miaka 13 hadi 18

Kupevuka huanza na kukua haraka kulingana na mabadiliko katika utendaji wa homoni. Unaishia katika kukua kwa uzazi na mifumo ya mapenzi pale ubalehe unapokoma na utu uzima kuanza. Huu unategemea jarnii na taratibu zake pamoja na mtu anavyojojisikia. Vijana wanaweza kujaribu ngono na madawa ya kulevyia. Vijana pia wanatafuta wasiri. Baadhi ya wasichana wanaweza hata kujaribu kupata mimba ili hitaj lao la kuwa na wasiri litimie, wakifikiwa kwamba " Mtoto atakuwa mtu mmoja anayenipenda sana". Vijana wanaweza kufurahia mafanikio yao ya utu uzima na majukumu kama vile kuwa na kazi

- **Vijana kati ya miaka 15 na 24 wapo katika hatari kubwa ya kuambukizwa VVU.** Milli yao bado inapevuka, na kuweza kupata maambukizi ya VVU; hasa wasichana wanaobalehe na kina mama vijana;
- **Kumbuka kuwasikiliza vijana,** uwaruhusu wao kuzungumza zaidi;
- **Wafundishe vijana kwa undani na taarifa sahihi** kuhusu ngono, maambukizi ya VVU na kuzuia maambukizi na namna ya ngono salama. Vijana wanaweza na wanahitaji kujifunza na kuelewa kwa mapana taarifa za VVU na UKIMWI walizonazo watu wazima;
- **Thibitisha** namna ilivyo vyema vijana wakitenda mambo sahihi kuliko kuwakosoa wakifanya vibaya;
- **Watie moyo** vijana wasijihushe na ulevi na utumiaji wa madawa ya kulevyia na wawe mfano wa kuigwa;

VVU na UKIMWI ni mada ngumu kwa kila mtu. Zinaamsha masuala ya ngono, tofauti za kijinsia, ushoga na utumiaji dawa za kulevyia na majadiliano yanayozihusu (hizo mada) yanawezza kuzusha maoni makali na kuonyesha mahitaji ya taarifa zaidi. Kwa hiyo kama mkufunzi na mtua habari, jambo la kwanza unatakiwa **uvee unaridhika na hali yako ya kijinsia.** Hii inahusisha mambo kama ni nini kuwa mwanaume au mwanamke; tabia zako za kijinsia, mwelekeo wako wa kijinsia matumizi yako ya madawa au pombe, unavyo wachukulia wanaume na wanawake; imani yako kuhusu kuacha kabisa ngono , ndoa ya mke moja, ndoa ya mke mmoja na matumizi ya kondomu; msingi wako wa kidini; unarmazamo gani kuhusu kazi ya ukahaba, ikiwa unatembelea makahaba; na unafikria nini kuhusu watu wanaoishi na VVU.

Hii inatakiwa kufikiri sana na kujiuliza maswali mengi. Ni vizuri kuzungumza na wengine. Na utakapovunja ukimya utashangaa kuona jinsi watu walivyo tayarif kuongelea masuala ya ujinsia. **Zungumza na wakufunzi wengine, marafiki, na walio wa rika lako.** Ni mpaka utakapoona umeridhika na unajisikia unaweza kujibu maswali kwa uhakika na kwa ushahidi ndipo utakapoweza kuzungumza na kundi la vijana ambao wanaelewa mambo fulani kuhusu ngono na dhana potofu nyiningine za kushangaza.

Kabla ya kuanza utatakiwa kutafuta **sheria za nchi** zinasema nini kuhusu VVU na UKIMWI na **nini sera ya VVU na UKIMWI** ya Kamati ya Olympiki ya Taifa na chama chako cha mchezo na ni taarifa gani, sera ipi na shughuli ambazo Kamati ya Olympiki ya Taifa imezitengeneza. Hizi zinaweza kutoa muongozo, au hata kutoa athari katika ufundishaji juu ya VVU na UKIMWI. Ushirikiano na **Baraza la UKIMWI la Taifa** unatakiwa ili shughuli na taarifa ziratibiwe.

Kwa kuwa michezo moja kwa moja inaathiri afya na uzima, ni vyema **kuongeza taarifa zinazohusu**

Sehemu ya 7

afya katika safu ya vipeperushi, pia taarifa kuhusu VVU. Japokuwa si njia sahihi katika elimu kwa jamii, vipepeperushi kama hivi, vinatoa taarifa sahihi ili kuelimisha jamii na kupunguza mwitikio mbaya wa jamii, iwapo uwepo wa mwanamichezo aliye na VVU ukajulikana kwa umma. Wale wanaohusika na mwitikio mbaya wa umma kuhusu kuwepo kwa mwanamichezo aliye na VVU wanaweza kufikiria haya ili kuwa na mafunzo na elimu kwa jamii kwa kiwango cha kawaida.

Inashauriwa **kutafuta ruhusa ya wazazi** kabla ya kuendesha elimu kuhusu VVU na UKIMWI. Hii itawalinda nyote, wewe na chama chako cha michezo dhidi ya matokeo yasiyopendeza. Wewe na chama chako cha michezo kwa kushirikiana na wazazi muweze kufanya uamuji iwapo wachezaji wataweza kujitoa katika shughuli zinazohusiana na VVU kama wakitaka.

Kisanduku cha 8: Mpango wa viongozi katika mafunzo, Swaziland

Mpango wa viongozi katika mafunzo, (LIT) Swaziland, ukisaidiwa na Chama cha michezo ya Olympiki Swaziland, na Chama cha jumuia ya Michezo ya Madola na Michezo Jumuiya ya Madola Kanada wakieleza umuhimu wa **kuwawezesha vijana katika jumuia zao kupitia michezo**, ili kupambana na VVU na UKIMWI kwa kuimarisha msingi wa elimu ya vijana na kuimarisha misingi sita ya tabia ambayo ni uaminifu, heshima, uwajibikaji, uadilifu, haki na uraia.

Maiengo ni **kutoa taarifa za VVU na UKIMWI kwa vijana waliko vijijini**, kutumia michezo ili mafunzo kuwa ya furaha, kuwafundisha na kuwawezesha viongozi wa vijana katika jumuia, kutengeneza vituo vya "Michezo kwa Wote"; kuzifanya jamii zhusike katika michezo na kutoa waalimu wa baadaye wa michezo na watawala.

Mafunzo juu ya uongozi, ukufunzi wa michezo, stadi za maisha na kuzuia maambukizi ya VVU yanatolewa - mwishoni mwa wiki - kwa viongozi wa vijana waliochaguliwa kwa wiki tano. Vituo vya michezo kwa wote vinajengwa na viongozi wanafundishwa vifaa vya vituo na njia za ubuni fu kwa jamii kuzalisha fedha na kuzitumia kwa ajili ya vituo. Hii inawafanya vijana kuendesha programu zao wenye we za burudani na kutoa nafasi kwa vijana kufahamiana na kuzijua njia za kuzuia maambukizi ya VVU. Viongozi pia ni mfano wa kuigwa kwa jamii.

Mpango mdogo ni **Siku maalumu ya Michezo**, wakati wote washiriki hukumbushwa nguzo sita ambazo huondoa muelekeo, kutoka kushindwa na fujo kwa kuheshimu michezo, kumtambua upya 'mshindii' na kusitiza juu ya kujaza nafasi ya hisia.

Kwa kuwa mpango wa mafunzo kwa viongozi unahusisha mafunzo ya viongozi wa vijana ili kutekeleza shughuli za msingi za viungo vya mwili kama michezo na michezo iliyounganishwa, inadhariwa kuwa hii ni hatua ya awali katika kuanzisha mipango ya juu kwa viongozi. Maendeleo yake yanamchukua kiongozi kijana katika msingi wa mpango wa mafunzo kwa viongozi; kuwaandaa kwa ajili ya kukua kuelekea utawala maalum katika michezo au kuhitimu katika ukufunzi iwe ni haruu kwa kiongozi. Wapo jumla ya vijana 16 waliohusishwa, wakiwa na umri kati ya miaka 14 na 25.

Sehemu ya 7

Mwishoni mwaka 2004 muhula wa pili kwa vijana 40 ulianza. Mpango wa mafunzo kwa viongozi umeonegeza mafunzo kwa vitendo ambapo wanafunzi huandaa Siku ya Michezo vijiji. Zaidi ya yatima 400 na watoto walio katika mazingira magumu walihuduria Siku ya Michezo ambapo walishiriki katika shughuli za elimu ya afya na michezo. Yalikuwa ni mafunzo ya uzoefu yenyewe maaana kwa wanafunzi wa mafunzo kwa viongozi pia furaha na siku ya kupata elimu kwa walishiriki.

7.2 Kwa hiyo unajisikia tayarī, utaihusisha namna gani timu?

Ni vyema kutumia nafasi yako kama mkufunzi kudhibiti majadiliano. Baadhi ya taratibu za msingi zitasaidia kwa mfano; taarifa za binafsi zikitolewa na mwanachama wa timu au wewe zibakie katika kikundi, kusive na lugha za kudharauliana, taarifa za siri kuhusu hali ya VVU ya mtu mwiningine isitolewe ndani ya kundi, unyoshaji wa mikono kuuliza maswali au kutoa changamoto, maswali yawenye ni ya kuhusu wote siyo kuuliza watu kuhusu hali zao kihusu ujinsia wao binafsi. Pata makubaliano katika kanuni hizi na nyininge kutoka kwa wachezaji.

Kisanduku cha 9: Kanuni za msingi.¹¹

VVU vinaathiri hulka zetu za ujinsia, ulinzi na imani zetu katika mahusiano na hali za baadaye. Ni muhimu **kanuni za kuaminiana na tabia** kutengenezwa wakati wa kushiriki katika kikundi. Katika vikundi ambapo watu wanataka kuongea kuhusu hisia zao binafsi na mada nyeti, wanatakiwa kujihis kufanya hivyo bila ya kuchekwa au kunyaamazishwa na bila woga kwa watu wengine kufahamu. Wanakikundi ni kipi kitawafanya wajisikie salama na starehe katika kikundi. Kadiri wanachama wa kikundi wanavyotoa maoni, kiongozi ahakikishe kuwa kikundi chote kinakubaliana kabla haijawa kamuni ya kikundi. Ikisha kubalika kanuni za msingi ziandikwe. Hizi zinaweza kurekebishwa au kuongezwa kadri kikundi kinavyoongezeka.

Kanuni za msingi zinazoweza kutumika:

- **Usiri;**
- **Kuheshimiana;** wanakikundi wanatakiwa kusikilizana bila kukatishina na waongee mmoja baada ya mwiningine;
- **Lugha;** wanakikundi wakubaliane kutumia lugha inayoelewaka na wote wasitumie maneno yanayoweza kuudhi;
- **Tabia ya kutohukurumiana;** wanakikundi wajiepushe kuhukumu hisia, maoni na tabia, za watu wengine, labda kama maoni hayo si ya kuheshimiana; na
- **Wanakikundi wawataarifu viongozi kama hawawezi kuhudhuria.**

Wanakikundi wana haki ya kutegeMEA ya kuwa watakaloisema litabaki kuwa siri; vinginevyo hawatafikisla ya kwamba wanaweza kuongea kwa uhuru. Lazima wajue ya kwamba majina yao hayataflikishe kwa watu wengire bila ya idhini yao. Ni muhimu kwa kwa kila mmoja katika kikundi chako kuwa na uelewa mmoja kuhusu usiri na kwamba una maana gani.

Inasaidia kuyandika haya na kuweka mahali panapoonekana ambapo mukutano unafanyika.

- **Unaloona hapa.**
- **Unalosikia hapa.**
- **Tafadhalli lla che libakie hapa!**

¹¹ Kanuni za msingi zinazoweza kutumika Inasaidia kusika katika Mawazo wa Kimataifa wa Watu wanacheki za VVU/UICMWI (ONP+). Mawazo; Kusika vikundi vya kujidhi na kusika kwa mafadiliko. Kitabu kwa watu wanacheki za VVU: <http://www.gppplus.net/progresa.html>

Sehemu ya 7

Moja ya wajibu wako wa msingi ni kujuu ni **kiwango kipi cha ufahamu au dhana potofu** vijana wanaweza kuwa nazo kuhusu VVU na UKIMWI, magonjwa ya zinaa, ngono na madawa ya kulevyo. Kwa kutumia kivunja ukimya hapo chini uwafanye watu wastarehe na ndipo utakuwa na ufahamu juu ya wanayoyajua na wasiyojua.

Japo **mchezo** huu kidogo hautafurahisha mwanzoni na kusababisha vicheko, utasaldia kufanya kila mimoja kuongelea sormo la ujinsia.

- Kiambie kikundi "kabla hatujaanza, nataka kujuu maneno yote ya mitaani mnayojuu yanayohusu ngono"
- Kadri watu wanavyo yatoa maneno, yaandike katika ubao. Itasaidia kuyaeleza kwa ukweli na kwa wazi, kama vile "sljawahi kusikia hili!" au "tulikuwa tukitumia hili".

Majadiliano haya yanaweza **kuzua hisia** ndani ya wanakikundi. Katika jamii zingine, watu wengi watamjua mtu fulani anayeishi na VVU au UKIMWI hasa katika nchi nyingi za Afrika na visiwa vya Karibeani, wakati huo huo katika jamii zingine hii inaweza kuwa si jumbo la kawaida. Ni vema kukisia ya kwamba ingalau kuna mtu mimoja katika kikundi aliye na uzoefu na VVU. Kuongelea maswala ya ngono kunaweza pia kuzua mijadala kuhusu ubakaji na mapenzi baina ya baba na binti yake au mama na mwanawewe pamoja na uzoefu wa kujamiihana baina ya wachumba. Unatakiwa kutambua uwezekano wa kuwapo haya na unatakiwa **kuwa mwangalifu unapopanga shughuli na majadiliano**. Upo katika nafasi nzuri kuanzisha hali ya huruma, heshima na usalama.

Jenga tabia ya kujiheshimu. Kuwasifu vijana mara kwa mara, kuweka malengo ya uhakika na kujali matakwa yao ni njia sahihi za kuwasaidia kujiheshimu wenye. Na hii ni muhimu kwa sababu wakati vijana wanapojsikia mahiri wenye, wanaweza kuhimili zaidi ushawishi wa rika, wa kufanya mapenzi kabla hawajawa tayari na kujiepusha na madawa ya kulevyo. Kwa ufupi si rahisi wakajihuisha na tabia ambazo zitawaweka katika hatari ya kupata VVU.

Njia moja ya kuanzisha majadiliano ni kwa kutumia **sanduku la maswali**. Hii inafanya maswali ya vijana kujibiwa bila wao kufedheheka kwa kwa kuyaaliza kwa sauti. Gawa vipande vya karatasi, na muorobe kila mtu aandike maswali yoyote anayoweza kuwa nayo kuhusu VVU, UKIMWI, ngono, madawa ya kulevyo, pombe n.k. Kusanya na vitie kwenye sanduku. Unaweza ukayajibu maswali moja kwa moja au ukaacha sanduku wazi ili yeoyote aweze kuongeza maswali. Unaweza kujibu maswali katika kipindi hiki au katika kipindi kinachofuata.

Ni Juu yako namna vipindi vinavyoendeshwa na mara ngapi vinafanyika. Lengo ni kuwazoesha wachezaji kuhusu VVU na UKIMWI na kuvunja vizuizi vya majadiliano. Inashauriwa kuwa shughuli au majadiliano juu ya VVU, UKIMWI, ngono au kutumia kileo yafanyakie mara moja kwa wiki au kama timu haikutani mara kwa mara, itumie nusu saa wakati wa mazoezi.

Wengi wenu mtakuwa na mahitaji tofauti, kwa hiyo **badilisheni na mtumie taarifa ili kukidhi hali na mazingira yenu**, kama vile rasimili zilizopo, idadi ya washiriki na umri wa wanavikundi. Moja ya mwelekeo wa thamani na unaofurahisha katika kujifunza, ni kujuu 'namna ya kufanya' wewe mwenye vyelelewe na vileyile pamoja na watu wengine. Unaajifunza kwa kuangalia namna ambavyo vitu vimfanywa kabla kwa kuboresha na kubadilisha mbinu ili kukidhi mahitaji yako. Ubunifu huu

Sehemu ya 7

ulio wazi wa mafunzo ni muhimu kwa waalimu wa michezo na wakufunzi. Hata hivyo kutafuta njia za kufanya mambo ni ufunguo wa kupambana na UKIMWI na kuimarisha ubora wa maisha katika jumuia zetu.

7.3 Kutafakari juu ya Vipindi

Itaweza kusaidia **kupata tathmini**, kutoka katika kundi. Njia moja ya kufanya ni kuandika moja ya yafuatayo kabla hawajaondoka;

- Kitu ambacho nimejifunza;
- Kitu ambacho kimenifurahisha;
- Kitu ambacho kingeboreshwa.

Baada ya kipindi inaweza kusaidia kama ukiwaza juu ya hilo kuona unaweza **kujifunza nini kwa ajili ya kazi za baadaye** na kuhusu ujuzi wako.

- Je, kila mtu allionekana kuelewa, nini kilichokuwa kinaendelea na taarifa zilizo kuwa zinatolewa?
- Je, kuna aliyeona zoezi linaudhi au la kudhalilisha? Je, nini kifanyike kukwepa hili?
- Je, wanakikundi wepi walionekana kufurahia na kwa nini?
- Je, kuna aliyeuliza swali uliopata ugumu wa kujibuu?



Sehemu ya 7

Shughuli Hatua ya 1

Umri unaopendekezwa: miaka 10 hadi 12

Sehemu hii ya mtaala inahusu kumalizia shughuli 5 kati ya 10. Rejea sehemu ya 4 Nini unachopaswa kujua na Sehemu ya 5 Michezo na VVU na kocha wako. Usisite kumuuliza kocha wako kwa msaada.

1. Tengeneza kitabu chenye picha¹² ili kuwashirikisha wenzako. Ongeza mada zifuatazo:

- Mwili wa mwanaadamu;
- Majimaji ya mwili yaliyo na VVU ya kutosha kuambukiza VVU kutoka mtu mmoja hadi mwiningine;
- Tabia za hatari zinazoweza kusambaza virusi kutoka mtu mmoja hadi mwiningine;
- Njia tatu za kujikinga na maambukizi ya VVU.

Shirikisha wenzako kusoma kitabu na fanya mabadiliko yatakayosaidia wengine kuelewa taarifa vizuri. Shirikisha familia na wanajamii yako.

2. Tengeneza bango la tangazo lenye picha za shughuli unazoweza kuzifanya salama na mtu anayelishi na VVU au UKIMWI. Ongeza yafuatayo:

- Shughuli na watu wengine wa michezo¹³;
- Shughuli na marafiki;
- Shughuli nyumbani.

Shirikisha bango lako na kundi lako, familia na marafiki. Waambie waongeze shughuli katika bango lako.

3. Tafuta kufahamu ni nini shule au jamii yako inachokifanya Siku ya UKIMWI Duniani (tar. 1 Disemba) na ujihusise. Hakikisha unatanya watu wengine kufahamu ni nini kinachoendelea. Leta taarifa ya shughuli za Siku ya UKIMWI Duniani kwa kilabu yako ya michezo.

4. Unaweza kuwafanya watu katika jamii yako au shule kufahamu kuhusu VVU na UKIMWI kwa:

- Kuweka bango kuhusu VVU na UKIMWI;
- Tengeneza na kugawa tepe nyekundu kumi;
- Andika hadithi kuhusu unavyofikiria jinsi ambayo ingekuwa kuwa na rafiki au mwanafamilia anayelishi na VVU au UKIMWI;
- Weka orodha ya mahali katika jamii yako ambapo unaweza kupata taarifa za ziada nyingi kuhusu VVU na UKIMWI.

¹² Kitabu chenye mfupi kuhusu maelezo kuhusu jambu fulani: Kinaweza kutumiwa na mbeza kuelezea nini amachokisema wanapojadiliana na marafiki na familia yake.

¹³ Inawezekana kujadili kuhusu majeraha yanayotokene wakati wa kucheza na damu ikiwepo. Zungumza namna ya kushughulikia haya bila ya kuongeza hofu ya VVU.

Sehemu ya 7



Utepe mwekundu

Utepe mwekundu ulanza kama juhudzi za msingi zenyeharaki za kuonyesha kuwasadia watu wanaoishi na VVU au UKIMWI, na matokeo yake hakuna utepe mwekundu maalum, na watu wengi hujitengenezea wenyewe. Leo utepe mwekundu ni alama ya klimatalifa kuelimisha kuhusu VVU na UKIMWI na unavalwa na watu mwaka wote mzima na hasa wakati wa Siku ya UKIMWI Duniani. Ni alama ya matumaini. Matumaini kwamba utafutaji wa kinga na dawa ya kuzua UKIMWI itafanikiwa na hali ya maisha ya watu wanaoishi na UKIMWI inaboreshwu. Pia ni ujumbe wa kutia moyo kwa watu wanaoishi na walioathiriwa na VVU na UKIMWI.

Kutengeneza tepe zako nyekundu, pata tepe nyekundu za kawaida kama sentimeta 1.5 upana na kata katika vipande kwa urefu kama sentimita 15. Halafu, kunja kwa juu kwa umbo la "V" iliyopinduliwa na weka pini katikati ambayo utaitumia kubana utepe kwenye nguo yako.

5. Tengeneza orodha namna watu wanaoishi na VVU au UKIMWI wanavyohudumiwa katika Jumula yako.

Wapi mtu anayeishi na VVU au UKIMWI atakwenda kupata msaada?

- Je, kuna hospitali au kliniki maalumu katika jumula yako?
- Je, kuna umoa wa kijumuia unaosaidia watu wanaoishi na VVU au UKIMWI na familia zao?
- Ni msaada kiasi gani familia zinatakiwa kutoa ikiwa mtu mmoja anaugua UKIMWI au maradhi mengine?

6. Tengeneza bango kuhusu nini watu wanaoishi na VVU au UKIMWI wanahitaji kuwasaidia kuishi salama au kuwa na hali njema kama wakiugua. Fikiria:

- Unahitaji nini kuendelea kuwa mzima au kupata nafuu kama ukiugua (kwa mfano maji safi, malazi, mavazi, na mtu wa kukuangalia)
- Ni nini vitu vya ziada mtu anayeishi na VVU au UKIMWI anahitaji ili aendelee kuwa mzima (dawa, chakula bora na watu wa kuwasaidia)

Shirkisha wenzako katika kundi na pia mtu mwininge – ndugu, mwalimu, rafiki.

7. Onyesha namna UKIMWI unavyoweza kuathiri watu wengi wa tofauti. Chora tofauti za UKIMWI. Fikiria watu tofauti wanaoweza kuwa na VVU au UKIMWI au kuwa na uhusiano nao, kwa mfano mwanaume, mwanamke, mtoto, mtu fulani kijana au mzee, watu wa rangi na dini tofauti. Shirkisha michoro yako kwenye kundi lako na mijadiliane.

8. Fikiria Jinsi ilivyo kuishi wazi na VVU au UKIMWI

- Orodhesha sababu zinazofanya watu wasipende wenzao kujua ya kwamba wanaishi na VVU au UKIMWI.
- Ni nini vikwazo katika jumula yako kuwa wazi ya kwamba unaishi na VVU au UKIMWI?

Sehemu ya 7

Jadiliana na kikundi chako.

9. Je, kuna **yeyote anayeishi wazi na VVU au UKIMWI** katika jumuia yako au nchi au mtetezi wa haki za watu wanaoishi na VVU na UKIMWI?

Muandikie barua kumtia moyo katika jukumu hilli gumu. Washirikishe wenzako barua hiyo katika kundi na uwaombe kusaini barua hiyo. Muombe kocha akusaidie kumtumia mtu huyo.

Kwa nini?

Kwa kujua namna ambavyo VVU havisambazwi unaweza kupunguza woga wako juu ya UKIMWI. Utaweza pia kutoa uangalizi na faraja, bila woga wa mtu aishiye na UKIMWI.

Namna Gani?

Kwa kila picha andika kile ambacho watu wanafanya. Utajifunza ya kwamba. VVU havieniezwi kwa mojawapo ya njia hizi.



Sehemu ya 7

Shughuli: Hatua ya 2

Umri unaopendekezo: Miaka 13 hadi 15

Sehemu hili inahusu kufanya shughuli 5 kati ya 12. Rejea **Sehemu ya 4 Nini unachopaswa** kujua na **Sehemu ya 5 Michezo na VVU** pamoja na kocha wako. Usisite kumuuliza kocha wako ukihitaji msaada zaidi.

1. Tengeneza kitabu cha picha^{} na shirikisha wenzako.** Zikiwemo mada zifuatazo:

- Mwili wa mwanaadamu, wa mwanaume na mwanimke;
- Majimaji ya mwili wa mwanimke aliyeambukizwa VVU yaliyo na wingi wa virusi ya kutosha kusambaza VVU kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwiningine;
- Maji maji ya mwili wa mwanaume aliyeambukizwa na VVU ambayo yana wingi wa virusi ya kutosha kusambaza VVU kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwiningine;
- Tabia za hatari zinazoweza kusambaza virusi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwiningine;
- Njia za kujikinga na maambukizi ya VVU.

2. Tengeneza bango la picha au orodha ya mambo unayopenda kufanya na marafiki. Pamoja na:

- Shughuli unazofanya na wawulana tu;
- Shughuli unazofanya na wawulana na wasichana;
- Shughuli unazofanya na wasichana pekee.

Onyesha orodiha yako kwa kikundi. Zungumza namna ambavyo shughuli hizi zinavyokufanya ujisikie vizuri. Waombe wengine, kama marafiki waongeze shughuli zinazokufanya wajisikie vizuri. Shirikisha picha au orodha hiyo na elezea hisia zako kwa familia yako na wenzako.

3. Zungumza na klongozi wa kundi, au mtu mzima katika familia yako au jumulia kuhusu mahusiano salama. Muulize kuhusu ujuzi unaohitaji katika mahusiano utakao kulinda dhidi ya maambukizi ya VVU. Jadiliana hili na watu wachache katika kundi lako. Kuwa mfano kwenye kundi lako kwa kuonyesha, kusema hapana kwa mtu anayekulazimisha kufanya jambo unalojua si sahihi au ambalo hutaki kulifanya.

4. Orodhesha huduma au sehemu za kutoa huduma ya Afya katika jumulia yako ambapo wawulana wanaweza kupata taarifa na huduma kuhusiana na kuzula VVU na magonjwa ya zinaa. Zungumza na mwanaume katika moja ya taasisi hizo kuhusu huduma wanaume wanazopata. Shirikisha kundi lako, taarifa hizo. Tafuta muda ingalau mara mbili kushirikisha rafiki zako katika jumulia yako.

5. Tengeneza bango kuhusu matumizi ya kondomu kuzula VVU. Uongeze taarifa kuhusu haya yafuatayo:

- Jinsi matumizi ya kondomu yanavyoweza kuzula magonjwa ya zinaa;
- Taarifa juu ya wapi kondomu zinapopatikana;

^{**}Kitabu chenye mfululizo wa picha na maelezo kuhusu jambo fulani: Kinawenza kutumiwa na mchezaji kuelezea nini anachokisema wanapojadiliana na marafiki na familia yake.

Sehemu ya 7

- Hatua za namna sahihi ya kutumia kondomu;

Tumia tangazo hili katika maonyesho Siku ya UKIMWI Duniani

6. Unaweza kufanya watu katika jumuia yako au shule kuelewa kuhusu VVU na UKIMWI kwa:

- Kuwapa tepe nyekundu na maelezo ya maana ya alama hii;
- Tayarisha tangazo la kuonyesha kuhusu VVU na UKIMWI katika jumuia yako;
- Omiba awepo mzungumzaji kuzungumza na kundi au shule yako kuhusu kuzuia maambukizi ya VVU;
- Tengeneza orodha ya mashirika katika jumuia yako ambayo unaweza kupata taarifa na ushauri juu ya kuzuia mimba na kujikinga na magonjwa ya zinaa.

7. Tafuta kujua ni nini shule au jumuia yako inafanya kwa ajili ya Siku ya UKIMWI Duniani (1 Disemba) na ushiriki. Hakikisha unawafahamisha watu wengine wajue kilichopangwa. Toa ripoti kwenye timu yako ya michezo kuhusu matokeo ya shughuli za Siku ya UKIMWI Duniani katika jumuia yako.

8. Tengeneza orodha ya namna ambavyo watu wanaoishi na VVU na UKIMWI huangaliwa katika jumulya yako. Ni wapi mtu mwenye VVU na UKIMWI atakwenda kwa ajili ya msaada? Jibu mengi ya maswali yafuatayo kadiri unavyoweza:

- Je, kuna hospitali au kliniki maalumu kwa watu wanaoishi na VVU au UKIMWI katika jumuia yako?
- Je, kuna chama chochote cha jumuia kinachosaidia watu wanaoishi na VVU au UKIMWI na familia zao?
- Je, serikali inafanya nini kuwasaidia watu wanaoishi na VVU au UKIMWI au watu wenye magonjwa yanayotishia uhai wao?
- Kama hakuna huduma maalum kwa VVU au UKIMWI; matibabu gani yananapatikana kwa watu wenye magonjwa yeyote makubwa?
- Je, ni nani anatoa huduma? Madaktari, wauguzi, wanaojitelea au familia?

Shirkisha kikundi chako ulichoifunza na waulize kama wanajua huduma zozote kwa watu wanaoishi na VVU au UKIMWI au magonjwa yoyote mengine.

9. Wazia unamfahamu fulani anayeishi na VVU au UKIMWI – ndugu, mwanafunzi mwenzako. Andika habari kuhusu mtu anayekuambia ya kwamba anaishi na VVU au UKIMWI. Elezea jinsi utakavyowatia moyo na kuwa rafiki yao. Shirikisha kikundi chako kwa habari hili.

10. Wazia jinsi ilivyo, kuwa wazi ya kuwa unaishi na VVU au UKIMWI.

- Tafuta kama kuna yeyote anayeongea wazi wazi kuhusu kuishi na VVU au UKIMWI. Je, kuna habari zozote? Watu wanazichukulaje?
- Orodhesha sababu zinazofanya watu wasipende wengine kujua ya kuwa wanaishi na VVU au UKIMWI. Ni nini vikwazo katika jumuia yako kuishi wazi na VVU au UKIMWI? Jadiliana na kundi lako.

Sehemu ya 7

- Je, kuna yejote anayeishi wazi na VVU au UKIMWI katika jumuia yako au nchi au mtetezi wa haki za watu wanaoishi na VVU au UKIMWI? Muandikie barua kumtia moyo katika jukumu hili gumu. Washirikishe wenzako barua hiyo katika kundi na waombe waisaini barua hiyo. Muombe kocha wako akusaidie kumtumia mtu huyo.

11. Jadiliana maonevu bila sababu na kundi lako. Kwa kuanza, fikiri mambo haya;


- Maonevu ni nini?
- Ulishawahi kuona mtu akikuonea tu? Kwa nini? Umri wako, dini, rangi ya ngozi yako au sababu zingine? Ulijisikiale?
- Ungejisikiale kama ukisikia mtu anatukanwa au kuitwa mtjina kwa vile tu ni wa tofauti?

Shirikisha maoni yako kwenye kundi. Jadilaneni na mpate mkakati pamoja kujianaa kupambana na chuki zinazoelekezwa kwenu na wengine. Fanyeni mazoezi pamoja ya kuwa mfano wa kuigwa.

12. Tengeneza bango la tangazo kuwahimiza watu kuwapa huduma watu wanaoishi na VVU na UKIMWI na si kuwabagua. Kama Desemba 1 inakaribia, lifanye tangazo kuwa la Siku ya UKIMWI Duniani. Waonyeshe wenzako. Tafuta sehemu katika klubu yako na ulionyeshe bango hilo.

"Jibeshimu. Kapime Na uwe mwaminifu"

Roy Simmons, Marekani, Mchezaji wa Zamani wa New York Giants, Ligi ya Taifa ya Mpira wa Miguu – Anayeishi na VVU.



Sehemu ya 7

Shughuli: Hatua ya 3:

Umri ulio pendekezwa: miaka 15 na zaidi:

Sehemu hii ya mtaalaa inahusu kumalizia shughuli 8 kati ya 15. Rejea Sehemu ya 4 Nini unachopaswa kujua na Sehemu ya 5 Michezo na VVU na kocha wako. Usisite kumuuliza kocha wako ukihitaji msaada.

1. Tengeneza kitabu cha picha¹⁵ ili kushirikisha wenzako. Ongeza mada zifuatazo

- Mwili wa mwanaadamu - mwanaume na mwanimak;
- Maji maji ya mwili wa wanaume na wanawake yaliyo na VVU vya kutosha kueneza maambukizi kutoka mtu hadi mtu;
- Tabia hatarishi zinazoweza kueneza virusi kutoka mtu hadi mtu;
- Jinsi kujidunga madawa kwa sindano kunavyoongeza hatari ya kuenea VVU;
- Jinsi magonjwa ya zinaa yanavyoongeza hatari ya kuenea VVU;
- Athari za ulevi kwa tabia na jinsi unavyoongeza hatari ya kuenea VVU;
- Maamuzi ya Afya kuhusu ngono na dawa za kulevyia kuzuia kuenea kwa VVU;
- Matumizi sahihi ya kondomu kuzula kuenea kwa VVU na magonjwa mengine ya zinaa.

Shirkisha kitabu chako na timu yako na fanya marekebisho yoyote, yatakayosaidia wengine kuelewa vizuri yaliyomo. Shirkisha marafiki walio nje ya timu yako na familia yako.

2. Kuna huduma za afya ya uzazi au klinik za mpango wa uzazi au mashirika katika Jumula yako zinazotoa taarifa na huduma kuhusiana na kuzuia mimba na magonywa ya zinaa pamoja na VVU? Wasiliana na moja ya mashirika haya na ujadiliane nayo kuhusu huduma wanazoweza kutoa kwa vijana. Ukipishikina na kocha wako **mwalike mshauri** aje azungumze katika moja ya kipindi na mwambie aongeze haya yafuatayo:

- Namna kondomu inavyozula mimba na magonjwa ya zinaa.
- Onyesha kwa mifano namna ya kutumia kondomu kwa usahihi- (tazama **Kiambatanishi 4**).
- Ni nafasi nzuri kwa kundi kuuliza maswali kuhusu upatikanaji wa kondomu, matumizi ya kondomu, kuzuia magonjwa ya zinaa, mimba na mahusiano.
- Mwalike mwanaume kutoka katika familia au jumuia yako kwenye mkutano huu.

Angalizo kwa Kocha: Mwishoni mwa kipindi hiki, waombe wana kikundi kutoa maoni yao kwa maandishi au kuongea namna wanavyojsikia kuhusu kutumia kondomu kwa siku za usoni, Je, wanadhania wanajua kutumia kondomu; je, wanadhania wenza wao watatumia kondomu; wanaweza kupata kondomu? Mshirikishe mshauri majibu na tengeneza mikakati ya ziada kuimarishe au kuongeza matumizi ya kondomu.

3. Tafuta ni wapi watu wanaweza kupata huduma ya ushauri nasaha wa hiari na upimaji katika jumuia yako. Unaweza kujaribu kwenye Kituo cha ya Umma kwa jambo hili au ofisi ya afya ya serikali, Angalia masuala yafuatayo:

¹⁵ Kibao chanzo nafakizo wa picha na muzito inhusi jumbo fulani: Kinowesta kuhusu na nichozaji kusolea nini unuchokiona waazapojulisa na mafiti na familia yako.

Sehemu ya 7

- Je, kuna gharama?
- Kuna usiri gani katika majibu? Nani ataarifiwe kama mpimwaji ameonekana ana maambukizi?
- Je, ushauri unatolewa kabla na baada ya kupima?

Kutokana na ulichojifunza, kuna ugumu katika kupimwa? Shirikisha kikundi chako yale ulijojifunza.

4. Kuna mashirika katika jumula yako yanayowasaidia watu wenyewe matatizo yatokanayo kwa pombe na madawa? Orodhesha mashirika haya. Wesiliana na mojawapo ya mashirika haya na uulize huduma wanazotoa. Shirikisha kundi lako taarifa hizi. Muombe mtoe huduma ya afya kutoka katika shirika mojawapo azungumze katika mikutano wa kikundi kuhusu matatizo ya matumizi ya pombe na madawa ya kulevya katika jumula yako na mikakati ya kuzuia matumizi ya madawa ya kulevya na pombe. Waalike wanajumuiya wengine katika mikutano huu.

5. Andika mfuatano wa maigizo mafupi au michezo ya kuigiza inayohusu kuweka mipaka ya mahusiano ya kimapenzi. Kwa mifano, rafiki yako anakuambia anamlazimisha rafiki yake wa kike wafanyi ngono. Amemtishia kuvunja uhusiano iwapo atakataa kufanya naye ngono. Anataka kusubiri mipaka aolewe ndipo afanye ngono.

6. Anzisha michezo ya kuigiza ambayo:

- Unamwambia wazi rafiki yako ikiwa anataka kusubiri kufanya ngono lazima aheshimu hilo;
- Wapenzi wanashaurina kutumia kondomu wanapofanya ngono. Ongeza uchaguzi alionao mtu iwapo mwenzake anakataa kutumia kondomu;
- Rafiki anakukaribisha dawa za kulevya,

Waombe kikundi chako wacheze mchezo wa kuigiza pamoja na wewe na kufanya mazoezi ili muutumie mchezo katika matukio ya Siku ya UKIMWI Duniani katika jurnuia yako.

7. Unaweza kuwafanya watu katika jumua yako au shule kuelewa juu ya VVU na UKIMWI kwa:

- Kampeni ya utepe mwekundu katika klubu yako ya michezo;
- Andaa tukio katika klubu ya michezo au jumua na wageni rasmi kutoka shirika la UKIMWI;
- Onyesha igizo shulenii linahusu masuala ya mahusiano na kushurina kuhusu ngono salama;
- Toa taarifa kuhusu wapi wapi unaweza kupata huduma za afya ya uzazi na uzazi wa mpango;
- Toa taarifa kuhusu matumizi sahihi ya kondomu (tazama kiambatanishi cha 4) na namna ya kupata kondomu katika jumula yako;
- Orodhesha huduma zilizopo kwa watu wenyewe matatizo ya madawa na vileo.

8. Tengeneza bango kuhusu kondomu kwa ajili ya klubu yako ya michezo au jumua wakati wa Siku ya UKIMWI Duniani. Mapendekezo yawe na:

- Wapi unaweza kupata kondomu katika jumuiya yako;
- Maelezo sahihi kuhusu matumizi ya kondomu;
- Onyesha namna sahihi ya kutumia kondomu; (tazama kiambatanishi cha 4)

Sehemu ya 7

- Nafasi kwa wageni katika onyesha kujaribu matumizi sahihi ya kondomu;
- Kama inawezekana, gawa kondomu za bure kwa wageni.

9. Tafuta ni nini shule au jumuiya yako inafanya Siku ya UKIMWI Duniani (1 December) na ushiriki. Hakikisha unawajulisha watu wengine nini kinachoendelea. Lete taarifa ya shughuli za Siku ya UKIMWI Duniani katika klabu yako ya michezo.

10. Tafuta wapi katika jumuiya yako panapotoa huduma za kutunza na kuwasaidia watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Ni wapi mtu anayeishi na VVU au UKIMWI anaweza kwenda kupata msaada? Jibu mengi ya maswali haya kadiri unavyoweza:

- Je, kuna hospitali au klinikii maalum kwa ajili ya waishio na VVU au UKIMWI katika jumuiya yako?
- Je, kuna vyama vyovote vya kijumuia vinavyowasaidia watu wanaoishi na VVU au UKIMWI na familia zao?
- Je, kama hakuna huduma maalumu za VVU au UKIMWI, huduma gani zinapatikana kwa ajili ya watu wenye magonjwa hatari?
- Je, ni nani anayetoa huduma? Madaktari, manesi, familia au wanaoijitelea?

Shirikisha kundi lako ulichojifunza na waulize kama wanajua huduma yoyote kwa watu wanaoishi na VVU au UKIMWI au magonjwa mengine. Kama kuna watoa ushauri wataalamu au au huduma za kijamii karibu, waulize ni jinsi gani klabu yako inavyoweza kusaidia – labda kwa kuwatemebelea au kuwasidia watu wanaoishi na VVU au UKIMWI au kujitolea katika shirika la kijamii au kliniki. (Hakikisha umeruhusiwa na mlezi au mzazi wako). Shirikisha uzoefu ullaona kwa timu.

11. Zungumza na mtoe huduma katika jumuiya yako – nesi, mshauri au mwanafamilia anayemhidumia mgonjwa. Waulize kutoa huduma kukoje, ugumu wake na falida zake. Fikiria kama ungependa kufanya kazi ya kutoa huduma za afya au la, na kwa nini. Mwandalie mtoe huduma zawadi. Shirikisha kundi lako uzoefu wako.

12. Fikiria ikoje kuwa wazi kuwa unaishi na VVU au UKIMWI.

- Angalia kama kuna mtu ye yeyote anayeongea wazi wazi kuwa anaishi na VVU au UKIMWI. Kuna habari yoyote? Watu wanachukuliale habari hizi?
- Orodhesha sababu zinazowafanya watu wasiwe wazi ya kuwa anaishi na VVU au UKIMWI. Ni nini vikwazo katika jumuiya yako kuwa wazi kuhusu VVU au UKIMWI? Jadiliana na kundi lako.

Kama kuna ye yeyote katika jumuiya yako au nchi anayejulikana ya kuwa ana UKIMWI, waandikie barua kuwatia moyo katika kazi yao ngumu. Shirikisha kundi lako na waombe wengine kuisaini pamoja na wewe. Muombe kiongozi wako akusaidie kuituma kwa mtu huyo.

Sehemu ya 7



Sehemu ya 7

13. Jadili Uonevu na namna ya kuukabili. Kwa kuanza fikiria mambo haya:

- Uonevu ni nini?
- Ulishawahi kuona mtu akikuonea tu? Kwa nini? umri wako, dini, rangi ya ngozi yako au sababu zingine? Ulijisikiaje?

Tengeneza bango dhidi ya chuki kwa watu wanaoishi na VVU au UKIMWI. Kama 1 Desemba ipo karibu lifanyi bango liwe la Siku ya UKIMWI Duniani. Lionyeshe bango lako kwenye kundi. Tafuta mahali pa kulionyesha bango lako kwenye klabu ya michezo au shulen.

14. Ongea na chama cha kijamii kinachojishughulisha na masuala ya UKIMWI waulize ni mabadiliko yapi yanayotakiwa katika jumuiya yako ili kusaidia watu wanaoishi na VVU au UKIMWI. Andika barua fuli au ombi na omiba kundi lako kuweka sahihi pamoja nawe. Mpe mfanya kazi wa chama cha kijamii kuipeleka kwa wanaotoa maamuzi.

"Nilidhani UKIMWI ni kitu kinachowapata mashoga na watumiaji madawa ya kulevyo. Mtu kama mimi ninayependa wanawake na mwenzye pumzil - hawesi kupata UKIMWI."

Tommy Morrison, anayelishi na UKIMWI bondia wa uzito wa juu, 1996.

15. Wakati mwiningine ni vigumu kusema "hapana" kwa ngono au kuchelewesha ngono? Miongozo iliyopo hapa chini inaweza kukusaidia kwa maamuzi:

Andika kwenye sanduku (R) kwa yale rahisi kuyafanya na (N) yale utakayoona magumu kuyafanya:

- | | |
|--|--|
| <input type="checkbox"/> 1. Kwenda kwenye sherehe na matukio mengine na marafiki. | <input type="checkbox"/> 8. Jiepushe kutembea na watu wanaoweza kukulazimisha kufanya ngono. |
| <input type="checkbox"/> 2. Amua utakwenda umbali gani (katika mapenzi) kabla ya kuwa katika hali ya kulazimishwa. | <input type="checkbox"/> 9. Uwe mwaminifu tangu mwanzo, kwa kusema hutaki kufanya ngono. |
| <input type="checkbox"/> 3. Amua kiwango cha pombe au madawa kabila ya kuwa katika hali ya kulazimishwa. | <input type="checkbox"/> 10. Jiepushe kutembea na watu ambao huwezi kuwaamini. |
| <input type="checkbox"/> 4. Epuka kuangukia katika maneno na mabishano ya kimpenzi | <input type="checkbox"/> 11. Jiepushe kuwepo mahali ambapo huwezi kupata msaada. |
| <input type="checkbox"/> 5. Uwe na uhakika na kikomo chako – usitoe muashirio unaochanganya kwa mfano, kufanya mambo kana kwamba unataka mapenzi wakati hutaki kufanya mapenzi. | <input type="checkbox"/> 12. Usikubali kupata msaada wa kusafiri katika gari kutoka kwa watu usio wajua au usiowaamini. |
| <input type="checkbox"/> 6. Kuwa mwangalifu juu ya hisia zako; hali ikiwa si nzuri, ondoka. | <input type="checkbox"/> 13. Usikubali zawadi na pesa kutoka kwa watu usiowafahamu vizuri. |
| <input type="checkbox"/> 7. Jihushe katika shughuli (kwa mfano michezo, vilabu, burdani). | <input type="checkbox"/> 14. Jiepushe kwenda chumbani kwa mtu wakati hakuna mtu mwiningine. |
| | <input type="checkbox"/> 15. Tafuta njia za kuonyesha hisia za upendo zaidi ya kujamiiiana. |



KUMBUKUMBU

Jaribio la VVU na UKIMWI

Jaribio la VVU na UKIMWI limeandaliiwa ili kujaribu elimu ya msingi kuhusu VVU na UKIMWI. Linaweza kupewa kundi lolote katika makundi matatu ya umri. Unaposahihisha jaribio, una nafasi ya kusahihisha imani zisizo sahihi mionganii mwa jumuii ya wanamichezo na inaweza kutumika kuchoechea majadiliano.

1. Kwa kukadiria watu wangapi wameambukizwa VVU duniani?

- 3.5 millioni
- 25 millioni
- 33 millioni

2. Unaweza jumuii na anayeshi na VVU?

- Kwa namna wanavyofanya
- Wanaonekana kuchoka na kuwa na afya mbaya
- Huwezi kutambua

3. Hatari ya maambukizi ya VVU kwenye michezo ni

- Juu
- Ya kati
- Ya chini

4. Unaweza kupata VVU kwa kuchangia kikombe na aliyembukizwa?

- Hapana
- Ndiyo
- Iwapo hutaosha kikombe

5. Wadudu wanaweza kuambukiza VVU?

- Ndiyo
- Hapana
- Mbu pekee

6. Majimaji ya mwilini ya aina ngapi katika mwili wa mtu anayelishi na VVU yana VVU vya kutosha kuambukiza?

- 2
 - 4
 - 6
- Yataje

7. Kama unacheza michezo na kujikata, unatakiwa....

- Uendelee kucheza
- Ondoka uwanjanini na omba msaada wa matibabu
- Muombe mchezaji mwiningine kusaidia kuzuia kuvuja kwa damu

Jaribio

8. Kipi kinakulinda zaidi dhidi ya maambukizi ya VVU?

- Vidonge vya uzazi wa mpango
- Kondomu
- Kufira

9. Nini dalili maalum za UKIMWI?

- Upele kutoka kichwani hadi is kidole cha mguuni
- Kuonekana umechoka na kudhoofu
- Hakuna dalili maalum za UKIMWI

10. VVU ni...

- Virusi
- Bakteria
- Fangasi

11. Je, kuna tiba ya UKIMWI?

- Ndiyo
- Hapana

12. Siku ya UKIMWI Duniani huadhimishwa lini?

- 1 Januari
- 1 Juni
- 1 Disemba

13. Kuna tofauti kati ya VVU na UKIMWI?

- Ndiyo
- Hapana
- Hapana kiasi

14. Kwa kukadiria, asilimia ngapi ya walioambukizwa VVU ni wanawake?


- 19%
- 46%
- 74%

15. Duniani kote, ni umri upi una maambukizi makubwa ya VVU?

- miaka 0 – 14
- miaka 15 – 24
- miaka 25 – 34

16. Kondomu kubwa zaidi ni....

- Pana
- Ndefu
- Vyote, ndefu na pana



Jaribio

17. Mtu anayeishi na UKIMWI, anahitaji umfanyile...

- Umkwepe mitaani
- Umpe uangalizi na uelewa kadiri unavyoweza
- Umlaumu kwa sababu ya kuumwa kwake

18. Makocha na wakufunzi wanaowatibu wachezaji waliojeruhiwa au kukwaruzika wanatakiwa...

- Wazitumie taulo na bandeji kama ikibidi
- Kutumia tahadhari za kiulimwengu za damu
- Kutokufanya chochote

Jaribio

Majibu ya Jaribio

1. Milioni 33
2. Huwezi kujua
3. Ya chini
4. Hapana
5. Hapana
6. Nne – Shahawa, Majimaji ya ukeni, Damu na maziwa kutoka matitini
7. Ondoka uwanjani na ormba msalada wa matibabu
8. Kondomu
9. Hakuna daili maalumu za UKIMWI
10. Virusi
11. Hapana
12. 1 Desemba
13. Ndiyo
14. 46%
15. Miaka 15 – 24
16. Vyote
17. Mpe uangalizi na uelewa kadiri uwenzavyo
18. Kutumia tahaadhari za kiulimwengu za damu



Faharasa

FAHARASA

Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) – Ni hatua ya mwisho ya maambukizi yanayosababishwa na virusi ya UKIMWI (VVU). Mtu anayeishi na VVU anaonekana na kujisikia mwenye afya muda mrefu kabla ya dalili za UKIMWI kuonekana. Hata hivyo, VVU hudhoofisha kingamwili mpaka ambapo mwili hauwezi kupambana na magonjwa na maambukizi kama vile nimonia, kuhara, vivimbe kansa na magonjwa mengine.

Dawa Za kuboresha Maisha Na Kupunguza Kasi ya VVU (ARV) – dawa zinayzotumika kutibu maambukizi ya VVU. Inafanya kazi kinyume na maambukizi ya VVU kwa kupunguza kasi ya kuzaliwa kwa VVU ndani ya mwili lakini dawa hizi si tiba.

Kondomu – ni namna pekee ya kinga ambayo inaweza kusaidia kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa, ikiwa ni pamoja na VVU na kuzuia mimba. Kwa kawaida kondomu za kiume hutengenezwa kwa mpira wa latex na huwa za maumbo tofauti, ukubwa na rangi na zinatakiwa kutumiwa na vilainishi vya majimaji. Pia kuna kondomu ya kike ambayo hutumiwa na mwanimke na huvaliwa kwa kuingizwa ukeni na kuenea.

Virusi vya UKIMWI (VVU) – Hiki ni kirusi ambacho husababisha UKIMWI. Kinashambulia kingamwili dhidi ya maambukizi.

Punyeto – ni kujamsha mwenyewe uume au uuke kiasi cha kufikia kilele. Punyeto si mbaya kimwi, kijinsia au kihisia na inaweza kuwa nzuri kwako. Kitabibu punyeto inachukuliwa kuwa njia ya kawaida ya kijinsia.

Magonjwa nyemelezi – Ni magonjwa yanayosababishwa na wadudu kama bakteria, vimelea ambaa baadhi yao hawasababishi magonjwa kwa watu walio na kingamwili imara.

Ngono ya Mdomo – Ni kutumia mdomo kuamsha sehemu za siri za mtu mwingine, inachukuliwa kuwa ni njia yenye hatari kidogo katika maambukizi ya VVU.

Ngono penyezi – Ni wakati uume unaingia ukeni au mkunduni, mwa mwanimke au mwaniamke. VVU vinaweza kuambukizwa iwapo kondomu haitumika wakati wa kuingiliana.

Watu Wanaoishi na VVU na UKIMWI – Neno hili linatumika kuonyesha ushahidi ya kwamba VVU vimepatikana katika damu ya mtu fulani.

Utepe Mwekundu – Ni alama ya kimataifa kuelimisha kuhusu VVU na UKIMWI na huvaliwa na watu mwaka mzima hasa Siku ya UKIMWI Duniani. Matumaini kwamba utafiti wa kinga na tiba ya kuzuia UKIMWI utafanikiwa na hali - maisha ya watu wanaoishi na VVU yataboreshwa. Pia Utepe Mwekundu ni ujumbe wa kuwatia moyo watu wanaoishi na walioathiriwa na VVU na UKIMWI.

Ngono Salama – hii inahusu kuchukua tahadhari inayopunguza uwezekano wa kuambukiza au kuambukizwa magonjwa ya zinaa pamoja na VVU unapofanya ngono. Kutumia kondomu vyema na kwa uthabiti inachukuliwa ni kufanya ngono salama.

Faharasa

Magonjwa ya Zinaa – Kama jina linavyojeleza ni maambukizi kuitia tendo la ngono. Baadhi ya dalili za kuambukizwa ni njia ya mkojo kuwaka moto au kuwasha, hasa unapokoja au kama njia ya mkojo inatoa ukijani, manjano, povu, damu au harufu mbaya. Kutumia kondomu kunaweza kuzula magonjwa ya zinaa kama vile kisonono na klamadia ambayo kama yasipotibila yanaweza kuwa na madhara makubwa kiafya.

Tahadhari za Kimataifa Ya Afya Kujikinga na Damu - ni viwango rahisi vya kudhibiti hatari ya magonjwa yanayoambukiza kutohana na damu. Tahadhari za kimataifa ya kujikinga inahusu matumizi ya kinga ya kuzuia kama vile glavu, joho, aproni, vazi la usoni au machoni ambayo linaweza kupunguza hatari ya kuambukizwa kwa ngozi [mucous membrane] ya mfanyakazi wa afya. Kwa kuongezea inashauriwa kuwa wafanyakazi wote wa afya wachukue tahadhari ya kujiepusha na majeraha yanayoweza kusababishwa na sindano, visu au nyembe za kupasulia na vifaa vyenye ncha kali. Kanuni hii inatumika kwenye damu, majimaji ya mwili yenye damu, shahawa na majimaji ya ukeni. Kanuni hii haitumiki kwenye kinyesi, kamasi, kohoz, jasho, machozi, mikojo na matapishi labda kama kuna damu. Haitumiki kwenye mate mpaka mate yaonekane na damu au kwenye fizi ambako uwezekano wa damu kuwepo kwenye mate ni mkubwa.

Nongo Nzembe – ni tendo la kujamiana bila kutumia kondomu. Hii inamuweka kila mtu katika hatari ya kuambukiza au kuambukizwa magonjwa ya zinaa ikiwamo VVU.

Siku ya UKIMWI Duniani – Inafanya kila mwaka tarehe 1 Desemba, ni siku ya kimataifa, kitaifa na kijumui kuungana dhidi ya UKIMWI na kuwatia moyo watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Kiambatanishi cha 1

Kiambatanishi cha 1

Sera ya VVU/UKIMWI ya Kamati ya Olimpiki ya Kimataifa.

Dibaji

Janga la VVU/UKIMWI limechukua maisha ya mamilioni ya watu kupita wakati wowote katika historia ya mwanaadamu. Inakadiriwa ya kwamba kiasi cha watu milioni 25 wamekuwa kwa UKIMWI tokea mwaka 1981 wakati VVU/UKIMWI ulipogunduliwa kwa mara ya kwanza. Kwa ujumla kiasi cha watu milioni 70 wameambukizwa VVU, virusi vinavyosababisha UKIMWI na watu milioni 42 kwa sasa wanaishi na VVU/UKIMWI. Mamilioni wengine wameathirika na mlipuko huu.

Kwa mujibu wa UNICEF, asilimia 33 ya wale wanaishi na VVU/UKIMWI wana umri chini ya miaka 25, jambo linalofanya kuwa chanzo kikuu cha kuperomoka kwa maendeleo ya uchumi na misingi ya kijamii na mshikamano katika jamii nydingi zilizoathirika. Izingatiwe ya kwamba jamii zinategemea kundi hili la umri katika maendeleo ya kiuchumi na ushindani katika michezo.

Umoja wa Mataifa unatabiri ya kwamba japo kwa kitovu cha janga hili ni Afrika Kusini mwa Sahara, dalili zinaonyeshesha ya kwamba kwa sasa linahamia Asia na Ulaya Mashariki labda hatua za kiutendaji za dhati zichukuliwe. Moja ya malengo ya Milenia ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa yaliyoazimiwa na Baraza Kuu la 55 inakusudia kuzuia na kuanza kubadili mwenendo wa maambukizi ya VVU/UKIMWI ifikapo mwaka 2015.

Inatambulika ya kwamba kulikibili janga la VVU/UKIMWI utahitaji mtandao mpana wa shughuli zinazoratibiwa unaofikia sekta zote, pamoja na serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali.

Kwa hiyo mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI ni moja ambayo Umoja wa Olimpiki unapaswa kushughullikia kwa kujilinga na ushirika wa kimataifa kulnua mwitikio wa kiulimwengu dhidi janga hili. Zaidi ya hayo KOK ni ya kipekee kwani ni shirika moja linaloleta pamoja idadi kubwa ya shirkisho mbalimbali za kimataifa za michezo na vijana kutoka duniani kote na huandaa tamasha la michezo kubwa na maarufu zaidi duniani.

Utangulizi

Mamilioni ya vijana wamekuwa bila kuelewa uwezo wao kamili, ukiwemo ule wa kushiriki katika michezo iliyoandalialiwa. Umoja wa Olimpiki unatambua athari za kijamii na kiuchumi zilizoletwa na janga hili katika jamii ya michezo. Kwa hivyo ni wakati wa kuleta pamoja majimbo yake kuongeza nguvu katika juhudhi za kiulimwengu. Kwa uhakika kuna haja ya kuanzisha njia mpya na ushirika wa kuongeza mwitikio wa dunia kwa janga hili. Sauti mpya yenye nguvu na mtetemo lazima isikike ili kuongeza mwitikio wa kiulimwengu kwa janga hili. Sauti hili ni ile ya Umoja wa Olimpiki.

KOK inatambua ya kwamba kushuka kwa uchumi na kuanguka kwa misingi ya urala katika baadhi ya nchi zilozoathirika bila kuepukika inaathiri michezo. Inatambua ya kwamba vyama vya michezo vitakabiliwa na ukweli ya kwamba wanamichezo, makocha, wasimamizi wa michezo na wanaojitolea wataugua na kufa.

Kiambatanishi cha 1

Kuna hisia ilioenea ya kwamba janga la VVU/UKIMWI ni ambalo KOK lazima ilishughulikie kwa kujunga na jumuia ya kimataifa katika kupambana kwa kutumia mtandao wake mkubwa, uwezo wake na baadhi ya rasilimali zake.

1. Wajibu wa KOK

KOK ina jukuru la haki, na kama inavyotakiwa na Kanuni yake yenyewe kuweka michezo kwa ajili ya kuhudumia binadamu. Ulimwengu wa michezo haukutengana na ulimwengu uliobaki. Michezo inafundisha stadi za maisha, inajenga kujiheshimu na kujiamini, yote ambayo yanaweza kutumika kupambana na kuenea kwa VVU.

KOK itakuwa mstari wa mbele katika mchango wa Umoja wa Olimpiki juu ya mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI iwa kuongeza nguvu na kutoa rasilimali. Itahamasisha majimbo yake kushiriki kikamilifu katika juhidi hizi.

Mara kwa mara, KOK itashiriki katika shughuli za kuelimisha kuhusu VVU/UKIMWI. Pia itakuwa kama sera yake kutoa matamko ya kuunga mkono mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI katika matukio ya kumbukumbu kama vile Siku ya UKIMWI Duniani.

KOK inakubaliana na "Kanuni ya Utendaji juu ya VVU/UKIMWI na ulimwengu wa kazi" ya Shirika la Kazi la Kimataifa. Kanuni hii, pamoja na mambo mengine, inataka kusiwe na ubaguzi wala unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.

2. Uhusiano wa KOK na mashirika mengine

KOK si shirika la afya wala taasisi ambayo kwa desturi inashughullikia masuala ya kijamili. Kwa hiyo KOK, itashirikiana na mifumo ya kitaalamu iliyopo ya mashirika makubwa yaliyo tayari kazini, haswa mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo tayari ina makubaliano nayo ya kushirikiana. Pia itatafuta ushirikiano mpya pamoja na mashirika makubwa kama vile Benki ya Dunia katika jambo hili.

3. Fursa zilizo wazi kwa KOK

KOK itaturnia nafasi ya Michezo miwili ya Olimpiki, Kambi ya Olimpiki ya Vijana na Siku ya Kukimbia ya Olimpiki, katì ya mambo mengine, kubeba na kueneza dhamira muhimu na ujumbe wenyewe habari za VVU/UKIMWI na utetezi kwa kuchapisha vijarida na nyenzo zingine za elimu kwa wanariadha. Kambi ya vijana ya Olimpiki inawaleta pamoja vijana kutoka pande zote za dunia ambapo Siku ya Kukimbia ya Olimpiki ni tukio la kipekee la michezo la kiulimwengu kwa watu wa kawaida.

KOK itahamasisha Vyama vya Dunia na Mabara vya KOT kujumuisha elimu ya VVU/UKIMWI katika shughuli zao.

KOK itazihimiza KOT na miundo yake kufanya kazi bega kwa bega na mashirika ya kitaifa na kimataifa ya kudhibiti UKIMWI katika jambo hili. Imezingatiwa kwa kipekee kuwa katika nchi zote zilizolengwa, mashirika ya kitaifa, hii ikiwemo serikali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, na pia mashirika makubwa, tayari warneanzisha mipango ya kuratibu mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI

4. Wajibu wa Kamati za Olimpiki za Kitifa

KOK itazihimiza kwa bidii KOT na miundo yake kuweka mitandao yao na rasilimali za kishirika na nytingeza kwa ajili ya matumizi ya juhudii za kitaifa zenye malengo ya kupunguza na hatimaye

Kiambatanishi cha 1

kubadili mwenendo wa janga la VVU/UKIMWI. Katika mwisho huo, KOK inazihimiza KOT na miundo yake kuongeza mipango ya mafunzo ya vipindi vya ufahamu wa VVU/UKIMWI kwa makocha, wasimamizi na wanariadha.

KOT hasa zinahimizwa kuhamasisha wanamichezo maarufu kushiriki katika kampeni za VVU/UKIMWI kama mfano wa kuigwa.

KOK inahimiza KOT, miundo yake na majimbo yake kushiriki katika uwezeshwaji kuzipa kujamini kunakotakiwa na zana ili ziweze kuchangia ipasavyo katika mapambano dhidi ya janga hilli. Pia KOT zinahimizwa kushiriki vyema katika shughuli za kuadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani na siku nyingine za kumbukumbu za matukio ya kitaifa.

5. Washirika na wafadhili

KOK inatambua kuwa umaskini, ukosefu wa elimu, ujnga na ukosefu wa usawa wa kijinsia kama baadhi ya sababu kuu zinazochangia kuenea na madhara ya VVU/UKIMWI. Kwa hiyo KOK itafanya juhudhi maalum kuendeleza elimu na kuanzisha mipango ya kuondoa umaskini kwa vijana na wanawake katika jamii zinazoendelea na itawahamasisha washirika wake na wafadhili kujiunga na Umoja wa Olimpiki katika juhudhi hizi.

KOK itashirikiana na washirika, wafadhili na mashirika husika ya kimataifa kutengeneza nyenzo maalum kwa ajili ya kutumika wakati wa mipango ya mafunzo kwa vijana, watu wa michezo na wanamichezo.

Hitimisho

Janga la VVU/UKIMWI linaleta tishio la kweli na halisi kwa uwepo wa mwanadamu, maendeleo na usalama wake. Ukweli kwamiba hasa linalenga na kuwadhoofisha vijana, wanaotengeneza uti wa mipango ya Umoja wa Olimpiki, unaifanya KOK kuguswa. Kwa hiyo KOK hailazaimishwi tu na mguso huo bali Kanuni yake yenye we inayoitaka michezo iwekwe katika huduma ya mwanadamu, kushiriki katika mapambano ya kiulimwengu ya kuzuia na kubadili mlipuko wa VVU/UKIMWI.

Kiambatanishi cha 2

Kiambatanishi cha 2

Habari ya Milipuko wa UKIMWI kwa eneo¹⁶

Milipuko wa VVU na UKIMWI Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mwaka 2008 kadiri la watu milioni 1.9 wanaoishi na kusini mwa jangwa la Sahara wamepata maambukizo mapya ya VVU, na kufanya idadi ha watu wanaoishi na VVU kufikia milioni 22.4. Wakati kiwango cha maambukizi mapya ya VVU Afrika kusini mwa jangwa la Sahara yamepungua polepole - idadi ya maambukizi mapya mwaka 2008 yaliyadiriwa kuwa 25% pungufu kuliko wakati janga hili ilipofikia kilele mwaka 1995 - idadi ya watu wanaoishi na VVU Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara iliongezeka kiasi mwaka 2008, kwa sehemu fulani kulisababishwa na kuboreshwa kwa maisha kulikochipukia kutohana na ubora wa dawa na ubora wa upatikanaji wa tiba kwa wanaoishi na VVU.

Kiwango cha maambukizi kisichobadilika kwa watu wazima (15-49) kilipungua kutoka 5.8% mwaka 2001 hadi 5.2% mwaka 2008. Mwaka 2008 kadiri ya watu milioni 1.4 walikuwa kutohana na sababu zinazohusiana na UKIMWI katika Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara. Idadi hii inawakilisha kushuka kwa 18% ya viwango vya vifo vinavyosababishwa na VVU katika kanda hii tangu mwaka 2004. Ngono ya watu wa jinsia tofauti imekuwa ni njia kuu ya kueneza VVU Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara, huku kiasi kikubwa cha maambukizi yakiendelea kwa watoto wanaozaliwa na wanaonyonyeshwa. Hata hivyo kama mijadala huu unavyoelekeza, ushahidi wa hivi karibuni kutohana na elimu ya magonjwa ya milipuko kwa kukadiria uwiano wa maambukizo mapya kwa kuzingatia njia ya maambukizi katika Mashariki, Kusini, na Magharibi ya Afrika imoonyesha kuwa milipuko katika kanda hutofautiana kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyoleveka kabla, kukiwa na kiasi kikubwa cha maambukizi mapya yanayotokea mionganoni mwa wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenza na wanaotumia madawa ya kujidunga kwa sindano katika nchi nyingine. Ushahidi uliojitekeza unathibitisha kupanda kwa kiwango cha VVU kisicho badilika mionganoni mwa wafanyao biashara ya ngono, ingawa mchango wa biashara ya ngono kwenye maambukizi mapya ya VVU hutofautiana kikanda.

Milipuko wa VVU na UKIMWI Asia

Mwaka 2008, watu milioni 4.7 walikuwa wakiishi na VVU Asia, pamoja na watu 350,000 waliopata maambukizi mapya mwaka 2008. Milipuko huu ulifiki kilele miaka ya kati ya 1990, na baadae kadhia hili ya wanaoishi na VVU kwa mwaka ilipungua kwa zaidi ya nusu. Kikanda milipuko huu ulilibaki palepale bila kupungua vala kuongezeka tangu mwaka 2000. Mwaka 2008 kadiri ya vifo 330,000 vinavyohusiana na UKIMWI vilitokea Asia. Wakati idadi ya vifo vinavyohusiana na UKIMWI Kusini na Kusini Mashariki ya Asia mwaka 2008 ilikadiria kuwa 12% pungufu zaidi kuliko vifo vya 2004, kiwango cha vifo vya waliozaliwa kinaendelea kuongezeka, huku idadi ya vifo viliviyotokea mwaka 2008 kuwa mara tatu zaidi ya mwaka 2000.

¹⁶ UNAIDS (July 2004) Rapor ya Janga la UKIMWI. Dicieni, Geneva (Switzerland), <http://www.unaids.org/bangkok2004/report.html>.
UNAIDS – (Dec 2004) Tazidi iliyu rekohishwa kuhusu janga la UKIMWI, <http://www.unaids.org/wad2004/report.html>.

Kiambatanishi cha 2

Mlipuko wa jangwa la Asia linatofautiana sana, likiwa na njia mbalimbali za maambukizi zilizotawala katika sehemu mbalimbali za kanda. Idadi ya watu waangalifu - kimsingi wanaotumia madawa ya kudunga na wafanya bashara ya ngono na wateja vao wamechangia kiasi kikubwa cha maambukizi ya VVU, muendelezo wa maambukizi kwa wenzi wa kike wanaotumia madawa na wateja wa wafanya bashara ya ngono unaonekana wazi kabisa. Zaidi ya hapo, takwimu zinazoendelea kukusanywa zimeelekeza: kiwango cha juu kabisa cha maambukizi mionganoni mwa wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao na watu wa jinsianyingine.

Mlipuko wa VVU na UKIMWI Amerika ya Kusini.

Mwaka 2008, maambukizi mapya 75,000 ya VVU yalitokea Amerika ya Kusini na Magharibi na Ulaya ya kati kwa pamoja, ikifanya jumla ya idadi ya watu wanoishi na VVU katika kanda hizi kuwa milioni 2.3.

Mlipuko hutofautiana kwa kiasi kikubwa katika sehemu kubwa ya nchi za Ulaya na Amerika ya Kaskazini. Mwelekeo ulio wazi ya kuongeza maambukizi mionganoni mwa wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao umejidhihirsha wazi katika nchi nydingi.

Mlipuko wa VVU na UKIMWI Visiwi vya Karibeani

Ingawa inachangia kiasi kidogo sana cha maambukizi ukilinganisha na mlipuko katika dunia nzima - 0.7% ya watu wanaishi na VVU na 0.8% ni maambukizi mapya mwaka 2008. Visiwa vya Karibeani vimeathirika kiasi kikubwa na VVU kuliko kanda yoyote nje ya Afrika kusini mwa Sahara, ikiwa ya pili yenye watu wazima wengi wenye kiwango cha maambukizo kisichobadilika cha VVU (0.1%).

Mwaka 2008, watu 240,000 walikuwa wanaishi na VVU katika Visiwa vya Karibeani, pamoja na watu 20,000 ambao walipata maambukizi mapya mwaka 2008.

Mlipuko wa VVU na UKIMWI Ulaya Mashariki na Asia ya Kati

Mwaka 2008, watu milioni 1.5 wa Ulaya Mashariki na Asia ya Kati walikuwa wakiishi na VVU pamoja na watu 110,000 ambao walipata maambukizi mapya mwaka 2008. Ulaya Mashariki na Asia ya Kati wanawekwa kundi moja kwa sababu ya kuwa karibu na kufanana kwa tabia za ilipuko yao. Milipuko katika kanda hii kimsingi husababishwa na maambukizi wakati wa kutumia madawa ya kujidunga.

Mlipuko wa VVU na UKIMWI Oceania

Mwaka 2008, maambukizo mapya ya VVU 3,900 yametokea katika kanda ya Oceania na kufanya idadi ya watu wanaoishi na VVU kuwa 59,000. Njia za maambukizi hutofautiana kwa sana katika kanda hii. Ngono kati ya wanaume na wanawake ndio njia ya maambukizi ya VVU na UKIMWI inayoongoza kwa ujumla nichini Papua New Guinea, wakati wanaume wanaofanya ngono na wanume wenzao wanaonekana kuchangia kadiri ya nusu ya mlipuko wa tarifa katika mataifa mengine madogo ya Pasifik. Katika mataifa makubwa ya Australia na New Zealand, wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao ndio njia kuu ya maambukizi kwa kiwango cha maambukizo kilichoenea na kuathiri.

Maambukizi wakati wa kutumia madawa ya kujidunga imechangia kiasi kidogo katika mlipuko huu huko Oceania, kwa sehemu fulani kwa sababu ya kufuata mapema utaratibu wa kupunguza madhara kwa kutumia ushahidi taarifa nichini Australia na New Zealand.

Kiambatanishi cha 2

Mlipuko wa VVU na UKIMWI Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini

Mwaka 2008, kadiri ya watu 35,000 mashariki ya kati na Afrika ya Kaskazini waliambukizwa VVU na vifo 20,000 vilivyohusiana na UKIMWI vilitokea. Jumla ya idadi ya watu waliookuwā wakiishi na VVU katika kanda hii mwishoni mwa mwaka 2008 ilikadiriva kuwa 310,000. Majanga katika Mashariki ya kati na Afrika ya Kaskazini yamejikta zaidi miengoni mwa watumiaji wa madawa ya kujidunga, wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao, na wafanya biashara ya ngono na wateja wao. Ambao wako tofauti na u taratibu huu wa kawaida ni Djibuti na Sudani Kusini ambako pia maambukizi hutokea kwa watu wa kawaida.

Mlipuko wa VVU na UKIMWI Amerika Kaskazini, Ulaya Magharibi na Kati

Mwaka 2008, maambukizi mapya 75,000 yalitokea Amerika Kaskazini na Ulaya Magharibi na kati kwa pamoja, na ku fanya idadi ya watu wanaoishi na VVU katika kanda hizi kuwa milioni 2.3.

Mlipuko u tofautana sana katika nchi nyingi za Ulaya na Amerika Kaskazini. Njia ilio wazi ya kuongeza maambukizi miengoni mwa wanaume wanaofanya ngono na wanaume wenzao imejidhiliishwa wazi katika nchi nyingi.



Kiambatanishi cha 3

Kiambatanishi cha 3

Habari kutoka kastika Tovuti

Avert (Zuia)

<http://www.avert.org>

Inatoa taarifa mbalimbali, pamoja na taarifa za msingi kuhusu VVU, UKIMWI na ujinsia pamoja na maeneo maalum kwa vijana na sehemu za elimu, vijarida na mitihani kwa vijana na watu wazima.

Kanuni ya Utendaji ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu VVU/UKIMWI na dunia ya kazi.

<http://www.ilo.org/public/english/protection/trav/aids>

Kanuni hii pamoja na mambo mengine inataka kusiwe na kubaguliwa au kunyanyapaliwa kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Kamati ya Olimpiki ya Kimataifa

<http://www.olympic.org/>

Tovuti rasmi ya Umoja wa Olimpiki.

Piga Teke UKIMWI: Kwa Michezo ya Mwendo na Shughuli za Michezo

Kitabu kinonyesha njia, mbalimbali za namna ya kujumuisha elimu ya VVU na UKIMWI na kazi katika shughuli zako za michezo, katika masomo yako ya elimu ya viungo na klabu yako ya michezo. Mapendekezo kadhaa yanatolewa kuhusu wapi kuongeza shughuli nyingine za kufurahisha na kuelimisha kama vile maigizo, shughuli za watoto, majadiliano n.k. Inaelezea taarifa za msingi kuhusu VVU na UKIMWI. Msisitizo unatolewa katika stadi muhimu za maisha zinazohusu kuzuia maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Kipate kitabu hiki kutoka kwenye mtandao:

http://www.norad.no/default.asp?MARK_SEARCH=YES&SEARCH_ID=77&V_ITEM_ID=1028

Penda Maisha (Love Life)

<http://www.lovelife.org.za>

Penda maisha ni mipango wa kitaifa kwa vijana wa kuzuia maambukizi ya VVU nchini Afrika Kusini. Taarifa na ushauri kuhusu mada zinazohusu elimu ya uzazi kwa vijana na wazazi hutolewa.

Haki ya Kucheza (Right To Play)

<http://www.righttoplay.com/>

Haki ya kucheza ni shirika la hisani linalotumia michezo na mipango ya michezo, kuhimiza maendeleo ya kifaya ya kimwilli, kijamii na kihisia kwa watoto wanaoishi katika mazingira yenyewe fursa duni. Haki ya kucheza imejengwa katika imani ya kwamba michezo ina nguvu ya kusaldia kutengeneza jumulia salama zenyewe watoto wenye afya bora. Kila siku tunashuhudia matokeo mazuri ya michezo kwa watoto wa wakimbizi, watoto waliokuwa wapiganaji vitani na watoto walio katika hatari ya kuambukizwa VVU na yatima katokana na UKIMWI.

Kiambatanishi cha 3

Chama Cha Kimataifa cha Kiswidi cha Elimu Ya Uzazi (RFSU-The Swedish Association For Sexuality Education-International)

<http://www.rfsu.se>

Inatoa elimu ya ujumla kuhusu elimu ya uzazi na hak. Vikiwemo vijitabu na nyenzo nyingine.

Mwilli (The Body)

<http://www.icc-cricket.yahoo.net/the-icc/social-responsability/overview.php>

Hazina ya taarifa kamili za VVU na UKIMWI.

Baraza la Mchezo wa Kriketi la Kimataifa (International Cricket Council)

<http://www.icc-cricket.com/icc/unaid>

Juhudi za uhamashajii kuhusu VVU na UKIMWI.

Shirikisho la Kimataifa la vyama vya Msalaba Mwekundu na Mwezi Mwekundu (The International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies)

<http://www.ifrc.org/what/health/hivaid/index.asp>

Kampeni ya kuzuia unyanyapaa.

Mpango wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa wa VVU na UKIMWI (UNAIDS)

<http://www.unaids.org/en/default.asp>

Habari na taarifa kuhusu mlipuko na mikakati ya kukabiliana na UKIMWI duniani.

UNICEF Sauti za Vijana (UNICEF Voices of the Youth)

<http://www.unicef.org/voy>

Ina taarifa sahihi, narnna ya kuwa salama, kupima VVU na matibabu, habari za kweli za kimaisha, chemsha bongo, maswali na mchezo: "Ungefanya Nini?"

Mtandao wa Habari kwa Vijana Ulaya na Asia ya Kati (Young People's Media Network in Europe and Central Asia)

<http://www.unicef.org/magic/bank/case025.html>

Duniani pote, watoto na vijana huchangia katika vipindi mbalimbali vya television, radio, magazeti, tovuti na njiu nyingine za habari kufanya sauti zao kusikika na kuyaweka matumaini yao na haja zao katika uso wa umma. Tovuti ya MAGIC ni mwitikio wa UNICEF kwa Changamoto ya Oslo, ya mwaka 1999 inayowataka wataalamu wa habari, wakufunzi, serikali, mashirika, wazazi, watoto na vijana wenye kuhusu umuhimu wa vyombo vya habari kufanya dunia mahali pazuri kwa watoto.

Hazina ya Ki-Elekroniki ya Elimu Rika kwa Vijana (YPeer Youth Peer Education Electronic resource)

<http://www.youthpeer.org/>

Hazina ya ki-elektronik ya elimu kwa vijana ni Tovuti yenyewe lengo la kuunga mkono maendeleo ya elimu rika kwa vijana katika Ulaya ya Mashariki na Asia ya Kati. Ni uvumbuzi wa pamoja wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo ya Afya na Ulinzi kwa vijana Ulaya na Asia ya Kati na Kamati ndogo ya Elimu Rika.

Kiambatanishi cha 3

Michezo ya Jadi Zambia (Zambia traditional games)

Nyaraka hii ni matokeo ya Michezo kwa vitendo (SIA – Sport in Action). Shirika liliopo nchini Zambia linalojishughulisha na maendeleo kupitia mradi wa michezo, na linazo taarifa juu ya chanzo, maelezo na uruhiru wa michezo ya jadi nchini Zambia. Nyaraka hii pia ina falsafa na utaratibu wa kuendesha shughuli za viuongo na michezo kwa watoto. Inajumuisha njia zaidi za kuunganisha michezo ya jadi ya kizambia na Elimu ya Afya na Uraia inayotoa nafasi kwa washiriki hasa watoto kupewa taarifa na ujuzi kuhusu VVU na UKIMWI na vileo, pia haki na wajibu wa watoto.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Sport in Action

P. O. Box. 38373

Lusaka, Zambia

Tel +260 1 232146

FAX +260 1 232147

email: sia@zamtel.zm

CUAHA

<http://www.cuaha.info>

CUAHA (Umoja wa Makanisa yanayopambana na VVU na UKIMWI Mashariki na Kusini mwa Afrika) ni mtandao ambao kazi yake kuu ni kuunganisha makanisa na kujenga makubaliano ya pamoja kuhusu masuala ya VVU na UKIMWI. Kwa kujenga uwemo na kubadilishana mawazo na uzoefu, mtandao husaidia makanisa na mashirika ya kiimani kujenga Programu za kukabiliana na mlipuko. CUAHA ina ushirikiano imara na kamati ya Olimpiki ya Kimataifa na imechukua jukumu kusambaza vifaa Mashariki na Kusini mwa Afrika.

ZUIA VVU

http://www.sportingpulse.com/assoc_page.cgi?c=2-4052-0-0-0&sID=86454

Programu ya Mafunzo ya Michezo kwa walio mbali juu ya VVU (ZUIA UKIMWI) hutumia nguvu ya michezo kutoa elimu na utambuzi juu ya VVU na maambukizi ya magonjwa ya ngono kwa wanaume na wanawake vijana Pasifikasi. Ushirikiano wa kukuza. Programu ya VVU na UKIMWI kwa jumuiya ya michezo ya Pasifikasi ilianzishwa kati ya SEKRETARIETI YA UONGOZI YA FORUM Visiwa vya Pasifikasi na WAKFU wa UKIMWI wa visiwa vya Pasifikasi/Kamati ya Taifa ya Olimpiki ya Oceania na Sekretarieti ya jumuiya ya Pasifikasi katika muundo wa kamati ya Kimataifa ya Olimpiki wa sera ya kuzuia VVU na UKIMWI. Matokeo ya ushirikiano huu ni kuanzishwa rasmi kwa ZUIA VVU Machi 2008 katika mkutano mkuu wa kamati ya Olimpiki ya Taifa ya Oceania, Nadi, Fiji na imekuwa ikifanya kazi sana tangu hapa.

Kiambatanishi cha 4

Kiambatanishi cha 4

Kondomu

Kwa nini ninahitaji kutumia kondomu?

Kondomu ndiyo njia pekee ya klinga ambayo inaweza kusaldia kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa pamoja na VVU na kuzuia mimba.

Kuwa tayari, kuchagua kondomu iliyo sahihi.

Idadi kubwa ya aina tofauti za kondomu sasa zinapatikana. Kinachoitwa haswa kondomu ni **kondomu ya 'kiume'**, kifuniko kinachofunika uume wa mwanaume na ambacho kimefungwa upande mmoja.

Kwa sasa pia kuna **kondomu ya kike** inayotumiwa na mwanamke na inaingizwa ndani ya uke wake. Hufuata uke na inasaidia kuzuia mimba na magonjwa ya zinaa pamoja na VVU. Kondomu za kike zinapatikana katika nchi nyngi, japo si kwa wingi duniani kote. Kondomu ya kike zipo za aina tofouti katika nchi tofouti.

Je, kondomu zimetengenezwa na nini na zipo za maumbo gani?

Kwa kawaida kondomu hutengenezwa kwa mpira maalum wa **aina ya latex**. Kondomu zipo za maumbo tofauti. Nyngi zina kisehemu cha kuzuia manii kwenye ncha kwa mbele na zingine hazina hiki kisehemu. Zingine zimetengenezwa kwa cha kuzula kuongezwa vitaaluma au vipele ambavyo vinaweza kuongeza hisia kwa wenza wote. Kondomu pia hutengenezwa kwa rangi mbalimbali. Kondomu zingine zina harufu nzuri ya kufanya ngono ya mdomo kuwa ya starehe zaidi.

Ulainishwaji wa kondomu pia unatofautiana. Kondomu zingine hazilainishwi kabisa na zinalainishwa kwa aina ya silikon, na kondomu zingine zina vilainishi vya majimaji. Vilainishi kwenye kondomu vina lengo la kuifanya kondomu kuwa rahisi kuvaliwa, starehe zaidi kutumia na kupunguza uwezekano wa kupasuka.

Kondomu ya kike imetengenezwa kwa ngao au pochi ya mpira ya urefu wa kama sentimeta 17 (au Inch 6.5). Kila mwishoni mwa kondomu kuna kiduara kinachonyumbulika. Mwishoni kulikochongoka, kiduara laini huingizwa ukeni ili kuishikilia kondomu. Katika sehemu ya wazi ya ngao kiduara hukaa nje ya mlango wa uke. Kiduara hiki kinatoa muelekeo wakati wa kuingiliana na pia huzuia ngao isifunike ndani ya uke.

Kuna vilainishi vya aina ya silikon ndani ya kondomu ya kike, lakini vilainishi vya ziada vinaweza kutumika. Unaweza kutumia vilainishi vyenye asili ya petroli katika kondomu ya kike. Kondomu hazina dawa ya kuua shahawa. Kondomu za kike zisitumike wakati mmoja na kondomu za kiume kwa sababu msuguano kati ya kondomu hizi mbili unaweza kusababisha mpasuko.

Vipi kuhusu ukubwa wa kondomu za kiume?

Kondomu zimetengenezwa kwa **urefu na upana, tofauti, na wazalishaji** tofouti hutengeneza za ukubwa tofauti. Hakuna kiwango cha urefu kwa kondomu, japo zile zilizotengenezwa kwa mpira wa asili hutanuka ili kuenea katika uume uliyosimama. Upana wa kondomu pia unaweza kutofautiana.

Kiambatanishi cha 4

Baadhi ya kondomu zina upana mdogo kiasi ili "kuenea –" vizuri, na wakati, zingine ni pana zaidi. Watengenezaji wa kondomu wamegundua kwamba marefu na mapana tofauti yanatakiwa kwani ukubwa wa uume hutofautiana.

Nerbo za uzaishaji wa kondomu pia unatofautiana kwa kila nchi, hivyo utatakiwa kufanya uchunguzi wako mwényewe juu ya nerbo tofauti za kondomu.

Kwa hiyo ni wakati gani wa kutumia kondomu?

Unatakiwa kutumia kondomu mpya kila wakati unapofanya tendo la ngono. Kamwe, usitumie kondomu moja mara mbili. Vaa kondomu baada ya uume kusimama na kabia ya mgusano wowote haujatokea kati ya mwenzio na uume wako.

Unatumiaje kondomu ya kiume?



Kwanza, kila mara angalia tarehe ya mwisho ya kutumika juu ya pakiti – kama tarehe ilionyeshwa imekwishapita, kondomu isitumike. Kondomu zinaweza kupasuka ikiwa hazikutunza inavyopaswa. Zinaweza kuathiriwa na joto na mwanga.¹⁷ Kwa hiyo, ni bora usitumie kondomu iliyokuwa imewelkwa katika mfuko wako wa nyuma, pochi ya kuweka fedha, au kisanduku cha kuweka glavu katika gari yako. Fungua pakiti kwa uangalifu, lakini kamwe usitumie mkasi au kisu! Toa kondomu kwenye pakiti, ukiwa mwangalifu hasa kama umevaa pete na/au kama una kucha ndefu au zenyé ncha kai, ili usipasue kondomu.



Weka kondomu iliyoviringishwa kwenye kichwa cha uume ulodisa kama kondomu haina kisehemu mbeleeni, finya ncha ya kondomu kiasi cha kuacha nafasi ya nusu inchi ya kukusanyia manii. Kama mwanaume hajatahiria, basi, kunja govi kwa nyuma kabia ya kuvala kondomu. Ifinye hewa toka katika ncha ya kondomu kwa kutumia mikonio mimoja na kunjua kondomu kwa kufuatisha uume kwa kutumia mikonio mwinguine



Kwa uangalifu ivishie kondomu katika uume ULIODISA mpaka iwe imekunjuka yote na/au uume wote urmekunika. Hakikisha ya kwamba, hakuna hewa ndani ya kondomu (ncha ya kondomu inatakiwa iwe "ime'egea" au "inaonekana tupu"). Kama unataka kutumia vilainishi nya ziada, vipako nje ya kondomu. Lakini daima tumia vilainishi nya majlmai (kama vle mafuta ya KY au Liquid Slik) kwa kondomu za mpira wa latex, kwani vilainishi nya mafuta vitawezza kusababisha kondomu za latex kupasuka. Mwanaume anayevaa kondomu si lazima awe ndiye anayejivalisha kondomu – itakuwa jambo zuri kwa mwenza wake kufanya hivyo.

¹⁷ Kondomu zinaweta kujenda kwa haujatokeza inavyopaswa. Zinaweta haujatokeza na joto na mwanga. Kwa hiyo, ni bora usitumie kondomu iliyokutunza kati ya nafiki wako wa nyuma, pochi ya kuweka fedha, au kisanduku cha kuweka glavu katika gari yako.

Kiambatanishi cha 4



Mara tendo la ngono linapomalizika (kumbuka unahitaji kondomu moja kwa kia tendo) ondoa kondomu kwa kushika kitako chake na kuichomoa ukiwa mwangalifu kutoruhusu manili yasiguse mikono yako. (Kwa kawaida hii ni rahisi kufanya katika uume haisi kuliko katika mfano wa uume, kwani umwagaji wa manii utatumika kama kilainishi na uume hautakuwa umedisa!)



Funga fundo mwishoni mwa kondomu na utupe kondomu iliyotumika katika utaratibu unaofaa – kwa mfano, katika pipa la takataka, kuliko kuitupa nje ya dirisha. Usisukume kondomu kwa maji kwenye choo, kwani linaweza kuziba choo! Watu wengine hukumbuka namna ya kuitupa kondomu kwa kuzingatia "K 3": kutupa jalalani, kuzika na kuchoma.

Wakati gani unaitoa kondomu ya kiume?

Itoe kabla uume haujalegea, na uishikilie kondomu katika shina la uume unapoivua, ili manii yasitapakaee. Kondomu itupwe kwa uangalifu, kwa mfano, lvingirishwe kwenye karatasi ya shashii na kuitupa kwenye pipa la taka. Usisukume kondomu kwa maji chooni – ni mbaya kwa mazingira.

Unafanya nini ikiwa kondomu ya kiume inapasuka?

Iwapo kondomu itapasuka wakati wa kufanya ngono, basi utoe uume haraka na ubadili kondomu. Wakati ukiendelea kufanya ngono mara kwa mara ikague kondomu kuhakikisha ya kwamba haijapasuka au kuteleza na kutoka. Kama kondomu imepasuka na unahisi kuwa manili yametoka nje ya kondomu wakati wa kufanya ngono, basi ufikirie kupata kinga ya dharura kwa mfano kidonge cha kutumiwa asubuhi inayofuata.

Namna ya kutumia kondomu ya kike



Hii ni kondomu ya kike. Ina kiduara katika kia ncha.

Kiambatanishi cha 4



Hatua ya kwanza ni kubonyeza kiduara "cha ndani" ili uweze kuklingiza, kama vile mtu anavyofanya kwa kizua mimba.



Kisha, ingiza kondomu ndani ya uke (au mkundu bila kiduara cha ndani) Hii hufanyika vile vile kama mwanamke atakavyoingiza kisodo au kizua mimba.



Sukuma kondomu ya kike ndani ya uke kiasi kwamba kiduara cha ndani kiko kwenye mlango wa kizazi. Umbo la asili la uke kwa kawaida huishikiila vizuri mahali pale. Kumbuka kwamba kondomu ya kike inaweza kuingizwa ukeni hata masaa manane kabla ya kufanya ngono.



Ni salama sasa kufanya ngono ya kuingilia. Hakikisha kuwa uume unaingia ndani ya kondomu ya kike na siyo nje katikati ya kondomu ya kike na ukuta wa uke. Sehemu za nje ya viungo vya uzazi vya kike na kiume sasa zimelindwa.



Tendo la ngono likima izika, zungusha kondomu ya kike na hvute kultoa nje. Itupe kondomu kowa kuwajibika na kwa njia inavyofaa – iweke kwenye pipa la taka, ichome au izike. Usiisukume kwa maji chooni kwani inaweza kuziba choo.

Kiambatanishi cha 4

Je, kutumia kondomu kuna matokeo mazuri?

Kama ikitumiwa vyema, kondomu ni bora katika kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU wakati wa kufanya ngono. Kutumia kondomu pia kunatoa kinga dhidi ya magonjwa mengine ya zinaa na kuzuia mimba.

Je, ninawezaje, kumshawishi mwenza wangu tutumie kondomu?

Inaweza kuwa vigumu kuzungumza kuhusu kutumia kondomu. Lakini usiruhusu **kutahayarika kuwa hatari kwa afya**. Mtu unayefikiri kufanya naye ngono anaweza aslikubali mara ya kwanza unaposema ya kwamba unataka kutumia kondomu. Hapa chini **kuna baadhi ya maoni yanayoweza kutolewa na baadhi ya majibu yake unayoweza kutumla**.

UDHURU	JIBU
Je, huniamini?	Kuamini siyo hoja, watu wanaweza kuwa na maambukizi bila kujua
Haitareheshi vizuri kwa kutumla kondomu	Nitajisikia starehe zaidi, nikilwa na starehe zaidi, nitaweba kufanya ujisikie vizuri zaidi
Nikivaa kondomu sidisi	Nitakusaidia kuweza kuivaa, ili uweze kudisa
Sina kondomu	Ninayo
Ninaogopa kumwambia atumie kondomu Anaweza akafikiria simuamini	Kama huwezi kumuambia, inawezekana humuamini.
Ni juu yake... ni uamuzi wake	Ni afya yako. Inapaswa pia uwe uamuzi wako!
Ninatumia dawa za majira, huhitaji kondomu	Kwa kila njia ningependa kuitumia itasaidia kutukinga na maambukizi tusiyojua tunayo.
Haina msisimko na siwezi kisikia chochote	Labda kwa njia hiyo utadumu kwa muda mrefu zaidi, na hiyo italeta maana ya kuitumia
Kuivaa kunaharibu starehe yote	Si hivyo ikiwa nitakusaidia kuivaa
Ninadhani hunipendi kabisa	Ninakupenda, lakini shatarisha maisha yangu kuthibitisha hilo
Nitatoa nje kwa wakati	Wanawake wanaweza kupata mimba na magonjwa ya zinaa ikiwemo VVU vinaweza kuambikizwa kabla ya kumwaga shahawa
Lakini ninakupenda	Hivyo utatusaidia kujilinda wenywewe
Kwa mara hii tu	Inahitaji kufanyika mara moja tu

Kuna sababu nyingi za kutumia kondomu unapofanya ngono. Unaweza kujadiliana na mwenza wako kuona anafikiria nini.

Kiambatanishi cha 4

Sababu za kutumia kondomu

- Kondomu ni kinga pekee ambayo pia inasaidia kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa yakiwemo VVU ikitumiwa vyema na kila wakati.
- Kondomu ni moja ya njia thabitii za kupanga uzazi zikitumiwa vyema na kila wakati.
- Kondomu hazina madhara ya kitabibu kama njia nyingine za kupanga uzazi zilivyo.
- Kondomu zinapatikana katika maumbo mbalimbali, rangi, harufu, msokotano na ukubwa tofauti ili kuongeza raha ya kufanya ngono.
- Kondomu zinapatikana kwa wingi katika vilabu vya pombe, maduka ya madawa, maduka makubwa na madogo.
- Kondomu ni rahisi kuzitumia. Kwa mazoezi kidogo, zinaweza pia kuongeza kujiamini katika starehe ya ngono.

Vidokezi vya kujiamini

Hivi ni baadhi ya vidokezi vinavyoweza kukusaidia kujiamini sana kuhusu kutumia kondomu.

- **Weka kondomu tayari kila wakati.** Kama mambo yakianza kupamba moto- utakuwa tayari. Si jambo nzuri kujikuta inakulazimu unatoka nje kwenda kununua kondomu wakati usiofaa – ukiwa katika mahaba mazito- unaweza usiende kununua.
- **Usiljsikie albu unaponunua kondomu.** Kwa lolote, jivune, inaonyesha ya kwamba unawajibika na unajiamini na wakati ukifika yote itakuwa ya thamani. Inaweza kufurahisha zaidi kwenda kununua kondomu ukiwa na mwenza au rafiki yako. Siku hizi katika nchi nyingine, unaweza kununua kondomu kwa siri kupitia kwenye mtandao.
- **Zungumza na mwenza wako kuhusu kutumia kondomu kabla ya kufanya ngono.** Inaondoa wasiwasi na albu. Kukubaliana kutumia kondomu kabla ya kuwa katika mahaba itawafanya nyote mjiamini zaidi.
- Kama hujawahi kutumia kondomu, njia nzuri ya kujifunza namna ya kuzitumia ni **kujaribu kuzivaa mwenyewe**. Haichukui muda mrefu kabla hujawa mzoefu.
- Kama unajisikia ya kwamba kondomu inatibia hisia za mahaba, **basi jaribu kuanza kuzitumia unapofanya mapenzi**. Inaweza ikaleta msisimuko mkubwa kama mwenzsi wako akikusaidia kuivaa au kama mkifanya hivyo pamoja.

